# Nipashe

Ijumaa Julai 19, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579974

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Anayepumua kwa mashine muda wote aomba msaada

UKURASA 4


BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Uchumi China waporomoka baada ya miaka 27

TARI Ilonga kumaliza shida ya mafuta nchini

UKURASA 13

# Wadau watoa ya moyoni sakata Kinana, Makamba

• **Viongozi** wa dini, wasomi washauri hatua za kuchukua kumaliza kinachoendelea... *Endelea ukurasa 2*



“Kinana na Makamba wamuone Rais Magufuli au waende mahakamani kupata suluhu.

**Dk. Benson Bana**



“Sidhani kama inaelekea mahali pazuri mpasuko kwa viongozi wakubwa kama hao. Watanzania tunahitaji amani si malumbano.

**Anna Henga**



“Kama jambo hili litaendelea katika sura hiyo, maana yake mustakabali wa chama na taifa unakuwa haukai vizuri.

**Sheikh Alhad Mussa**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**WANUNUZI WANASWA UTOROSHAJI WA MADINI**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amefanya ukaguzi na kuwakamata wanunuzi wa dhahabu 12 wanaodaiwa kununua...

UKURASA WA 5

**MSHTAKIWA AOMBA KORTI KUKIRI KUUA BILA KUKUSUDIA**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili Joseph Mahende ya mauaji ya mke wake, Mosi Kitaleti, umeiomba...

UKURASA WA 7

**UTARATIBU MPYA USAJILI, UTOAJI HATIMILIKI ARDHI**

SERIKALI imesema itaanza kufanya usajili na utoaji wa hatimiliki za maeneo pamoja na nyaraka zote katika ngazi...


## Kiama wahalifu daftari la mpigakura

UKURASA 3



UK.2

## JPM aagiza uchunguzi wa kina waliobambikwa kesi


MICHEZO **SILAHA SIMBA SC HAZIKAMATIKI** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wanunuzi wanaswa utoroshaji wa madini

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amefanya ukaguzi na kuwakamata wanunuzi wa dhahabu 12 wanaodaiwa kununua madini nje ya masoko yaliyoidhinishwa na serikali wilayani Kahama.

Imedaiwa kuwa wanunuzi hao walikuwa wanajihusisha na utoroshaji wa madini ya Tanzania kupitia nchi za Kenya na Uganda, wakikwepa kulipa kodi ya serikali.

Vilevile, waziri huyo ameagiza kuwekwa ndani kwa maofisa madini wanaodaiwa kushiriki katika utoroshaji wa madini na kuandaa taarifa za uongo kwa serikali.

Katika ukaguzi huo uliolenga kuwakamata wanunuzi wa madini wanaokwepa kodi uliofanyika katika Halmashauri ya Msalala, wanunuzi 12 walikamatwa wakituhumiwa kununua dhahabu nje ya masoko yaliyoidhinishwa.

Biteko alisema wale wanaoiba madini na kukwepa kulipa kodi ya serikali kwa kununua madini nje ya masoko, wataishia jela na saa ya kunyakuliwa kwao imewadia.

Alidai kuwa kati ya wanunuzi 12 waliokamatwa, imebainika mmoja wao ndani ya wiki mbili, amenunua dhahabu kwa Sh. milioni 300 na mwingine ndani ya wiki tatu amenunua dhahabu ya Sh. milioni 241.

Alisema sekta ya madini ina mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi endapo kutakuwapo na ushirikiano na kutumia fursa ya kuuza madini kwenye masoko ili kodi stahiki za serikali zilipwe.

# Wadau watoa ya moyoni sakata Kinana, Makamba

**Na Waandishi Wetu**

WASOMI na viongozi wa dini wametoa maoni yao kuhusu sakata la makatibu wakuu wastaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba, kuliandikia barua Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu Wastaafu wa chama hicho.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, wawili hao waliandika barua kwa baraza hilo lililo chini ya uenyekiti wa Rais mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, wakilalamika kuhusu tuhuma za kumhujumu Rais Magufuli zilizotolewa dhidi yao na mtu anayejiita mwanaharakati huru.

Tayari baraza hilo limeshawajibu wawili hao, likieleza kuwa suala lao lilipaswa kushughulikiwa kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa kwenye katiba ya chama hicho badala ya kukimbilia kwa baraza.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu suala hilo, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. George Kahangwa, alisema barua ya viongozi hao inaonyesha kutokuaminiana ndani ya chama hicho na kwamba viongozi hao wastaafu wameleta somo jipya kwa jamii ya sasa.

"Hii inaonyesha kutokuaminiana ndani ya chama na bahati nzuri wote ni wazee na wakati fulani ni jukumu lao kujengeana imani.

"Siijui katiba yao vizuri lakini nadhani panapotokea tatizo ni muhimu apatikane mtu wa katikati atakayesimama kama msuluhishi.

"Kwa hiyo, kuwaambia waende kwa viongozi waliopo sasa ambao ndiyo kama upande wao wa pili si sawa na hawakukosea kuileta 'public' (kwa umma) kwa sababu yule kijana (anayetuhumiwa kuwachafua) tayari aliwatuhumu hadharani," alisema. Mhadhiri mwingine katika Idara ya Sayansi ya Siasa ya UDSM, Dk. Benson Bana, akizungumza na Nipashe jana, aliwataka Makamba na Kinana kumwona Mwenyekiti wa chama hicho, Rais John Magufuli, ili kupata ufumbuzi wa suala lao.

Dk. Bana alisema njia iliyotumiwa na makatibu wakuu wastaafu wa CCM hao kuandika waraka na kuachia hadharani, haiwezi kuwapa matokeo mazuri.

"Wangemwona Rais ambaye ndiye mwenyekiti wa CCM ama

INAENDELEA UK. 8



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), Godfrey Simbeye, akizungumza wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la kwanza la Biashara kati ya Tanzania na Uganda, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damasi Ndumbaro na Balozi wa Tanzania nchini Uganda, Dk. Aziz Mlima. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# JPM aagiza uchunguzi wa kina waliobambikwa kesi

**Na Beatrice Moses**

RAIS John Magufuli ameagiza Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama kutembelea magereza yote nchini ili kubaini na kuwaachia huru mahabusi wanaosota rumande kwa kubambikwa kesi.

Alitoa agizo hilo jana wilayani Kongwa mkoani Dodoma alipozungumza na wakazi wa wilaya hiyo ikiwa ni siku tatu tangu afanye ziara ya kushtukiza kwenye Gereza Kuu la Butimba jijini Mwanza.

Akiwa katika gereza hilo, Rais Magufuli alibaini kuwapo kwa changamoto ya msongamano wa wafungwa na mahabusu kunakosababishwa na ubambikaji wa kesi na mahabusi kutofikishwa mahakamani. Kutokana na ziara hiyo ya Rais Magufuli gerezani huko, juzi mahabusi 200 waliachwa huru ikiwa ni hatua ya utekelezaji uliofanywa na wizara hiyo ikiihusisha Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali. "Walikwenda pale Butimba na kuwasilikiza kwa zaidi ya saa saba, kisha waliwaachia watu 75," Rais Magufuli alisema.

Alibainisha kuwa mahabusi wengine walioachwa huru ni 100 kutoka Bariadi, Mugumu Serengeti (52), Tarime (6), Bunda (24) na Kahama (43). Rais Magufuli alisema wako mahabusi wamewekwa mahabusu kwa makosa ya kuonewa na wengine kesi zao halisi zingefikishwa mahakamani mapema, wangehukumiwa kifungo cha miezi sita jela lakini wameonewa kwa kukaa rumande kwa zaidi ya miaka minane.

Akifafanua zaidi kuhusu changamoto hiyo, Rais Magufuli alimtolea mfano mahabusi aliyemkuta kwenye Gereza Kuu la Butimba ambaye alikamatwa akiuza mafuta ya magendo, akakamatwa na kuombwa rushwa ya Sh. milioni moja na aliposhindwa kutoa, alijikuta akipelekwa mahakamani na kushtakiwa kwa kesi ya mauaji.

"Siwezi nikatawala nchi ya machozi, haya yataniumiza, siwezi, watu wanasikitika, wapo kwenye unyonge wa kuonewa," Rais Magufuli alisema.

Kiongozi wa nchi huyo aliwaonya askari polisi wanaowabambika kesi wananchi, akiwataka wawe na hofu ya Mungu. Rais Magufuli alisema miongoni mwa mahabusi walioachwa huru juzi, ni askari polisi wanane waliokuwa wanatuhumiwa kushiriki katika utoroshaji wa dhahabu na ameagiza warejeshwe kazini.

"Hata kwa kuwaona tu unaweza ukajua kwenye macho yao, DPP amewaachia, nimeamua warudishwe kazini kwa sababu walikuwa wameshafukuzwa," alisema.

"Lakini liwe fundisho kwa watu wanaopenda 'virushwarushwa', waache kuwapambikiza kesi, siyo kitu kizuri, lazima tumwogope Mungu." Rais Magufuli pia aliupongeza uongozi wa Wilaya ya Kongwa kwa kutenga eneo kwa ajili ya jeshi kuwa Mkoa wa Dodoma ni makao mkuu ya nchi na suala la kuwa na kambi za jeshi haliepukiki.

Rais Magufuli pia alieleza sababu za kutohamia kwake mkoani Dodoma kwa wakati aliokusudia, akisema ni kutokana na kuugua kwa mama yake.

"Hata mimi ilikuwa nihamie (Dodoma) lakini bahati mbaya wakati najiandaa kuhama, mama yangu aliugua... kwa hiyo, inabidi nimhudumie, lakini mara nyingi nimekuwa nikija hapa Chamwino, tunataka ndoto hii itimie kwa vitendo," alisema.

Akiwa wilayani Kongwa jana, Rais Magufuli alitoa mchango wa Sh. milioni tano kusaidia ukarabati wa Shule ya Msingi Sagala iliyoezuliwa na kimbunga hivi karibuni.

Rais pia alitumia nafasi hiyo kuwahamasisha viongozi wa serikali, dini na siasa kuchangia ukarabati huo, akifanikisha kukusanywa zaidi ya Sh. milioni sita, mabati 252 na mifuko ya saruji 300.

Awali, Mbunge wa Kongwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, alipongeza mafanikio ambayo serikali ya tano imeyapata na kueleza changamoto zinazowakabili wananchi wa Kongwa.

Ndugai aliiomba serikali kuliboresha eneo lililotumiwa kuhifadhi wapigania uhuru wa nchi za Afrika, kujengwa kwa kambi ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) na kukarabatiwa kwa Uwanja wa Ndege wa Kongwa ili uwe wa akiba.

# Kiama wahalifu daftari la mpigakura

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema mpigakura atakayejiandikisha vituo zaidi ya kimoja na ikathibitika wakati huu wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura lililoanza jana katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, wajiandae kuchukuliwa hatua za kisheria.

Pia, amezionya asasi zote za kiraia zilizopata vibali vya kutoa elimu ya mpigakura kutoa elimu hiyo kwa wananchi kwa kuzingatia mwongozo wa elimu ya mpigakura uliotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana katika Uwanja wa Mandela, Manispaa ya Moshi, wakati akizindua zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura lilioanza jana hadi Julai 24, mwaka huu mkoani Kilimanjaro.

Baada ya hapo uboreshaji utaendelea kwa siku saba katika maeneo mengine ya Tanzania Bara kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na NEC.

"Hakuna mtu atakayeachwa katika kujiandikisha na hakuna mtu atakayeruhusiwa kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 pasipo kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura na kuwa na kadi ya mpigakura.

"Lakini pia kama ambavyo wamesema 'wana msanja' (kikundi cha utamaduni wa ngoma za asili), hairuhusiwi kujiandikisha vituo zaidi ya kimoja na ikithibitika hivyo lile lile lililosemwa na msanii wa msanja, tuta...(wanamalizia wananchi wakisema, watasweka ndani).

Waziri Mkuu alieleza kuwa uboreshaji huo unafanyika wakati mwafaka kuwa maandalizi ya uchaguzi mkuu mwakani 2020 yamekaribia na kwamba serikali itaendelea kuiwezesha NEC ili kukamilisha uboreshaji wa awamu zote mbili kwa mujibu wa sheria.

"Leo (jana) tunaanza na tukishamaliza, tutafanya mapitio tena, wale ambao watakuwa wamesahauliwa, wale ambao walikuwa na dharura watapata fursa ya kujiandikisha. Na katika uandikishaji wewe mtendaji huna haja ya kujua anatoka chama gani ili mradi ni Mtanzania, yuko mbele yako mwandikishe ili aweze kutimiza haki yake, suala la chama atajua yeye mwenyewe."

**AONYA ASASI ZA KIRAIA**

"Nimeambiwa kuwa Tume imetoa vibali vya kutoa elimu ya

INAENDELEA UK. 8

## NBC yatoa bil.2/- kukopesha wastaafu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetoa mikopo yenye jumla ya kiasi cha Sh.billioni 2.1 kwa wastaafu tokea ilipozindua huduma ya mikopo ya wastaafu Juni mwaka jana.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi, Mkurugenzi wa Wateja Binafsi, Gaudence Shawa, katika uzinduzi rasmi wa Tawi jipya la Benki hiyo la Tegeta Kibo Commercial Complex, alisema benki hiyo imewatambua wastaafu kama kundi muhimu la kiuchumi.

"NBC tumewatambua wastaafu wanaopokea pensheni kama kundi la kiuchumi ambalo lina uwezo wa kuchangia katika uchumi wa taifa letu kwa kuwezeshwa kifedha," alisema.

"Kikwazo kikubwa, kwa siku za huko nyuma, ilikuwa kutokuwapo kwa bima ya mikopo kwa watu waliovuka umri wa miaka 60, sasa ipo bima inayowakinga wastaafu waliovuka umri huo nchini," aliongeza Sabi.

Alifafanua kwamba kwa kutambua umuhimu wa wafanyabiashara wadogo na wa kati, mwaka 2016, uongozi wa benki hiyo waliunda kurugenzi maalum ya kuhudumia wateja hao na hadi Machi mwaka huu benki hiyo imeshatoa jumla Sh. bilioni 155 kama mikopo kwa wafanyabiashara 3,000 nchini.

Aliongeza kwamba benki hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) ambalo ni Benki tanzu ya Benki ya Dunia imefanya mapitio ya kina ya utaratibu mzima wa utoaji wa mikopo katika kundi hilo ili kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi wa viwanda nchini.

Shawa alifafanua kwamba benki hiyo imewawezesha wateja binafsi takribani 27,000 kwa mikopo isiyokuwa na dhamana yenye thamani Sh. 337,000 kati ya hao asilimia 53 ni watumishi wa serikali na asilimia 47 ni kutoka sekta binafsi.

"Azma ya benki hii ni kuwakuza wafanyabiashara wadogo hadi wafikie hatua ya kuchangia katika uchumi wa Tanzania na katika kutimiza lengo hilo benki hii imezindua klabu za biashara zijulikanazo kama 'Business Clubs" katika mikoa mbali mbali nchini," alisema.

Alisema dhumuni la kuanzisha klabu hizo ni kuwajengea uwezo wafanyabiashara hao kwa mafunzo maalum ya kuendesha biashara zao kwa njia ya kisasa na kuongeza uzalishaji, faida na tija ya uendeshaji.

Shawa aliongeza kwamba mafunzo hayo yanaratibiwa na benki hiyo kwa kushirikiana na taasisi kadhaa kama vile Mamlaka ya Biashara Tanzania, Kituo cha Uwekezaji (TIC), Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO), Chama cha wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Pamoja na mambo mengine, hadi kufikia Disemba mwaka jana, benki hiyo ilikuwa imetoa mafunzo hayo kwa takribani wafanyabiashara 7,000 na lengo ni kuwafikia zaidi ya 1,000.

## Ukaguzi wa miradi, viwanda nchi nzima

**Na Mwandishi Wetu,** RUVUMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) litaajiri watendaji wa muda katika kanda zake zote nchini ili kuharakisha ukaguzi wa miradi na viwanda kuanzia ngazi za kata.

Pia urasimishaji wake hali itakayosaidia utunzaji wa mazingira na pia kuongeza mapato kupitia tozo mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, kwenye ziara yake ya Kanda ya Kusini kwenye mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma katika ukaguzi wa miradi na kuzungumza na maofisa mazingira ili kubaini changamoto zao katika utekelezaji wa sheria na kanuni za mazingira, alisema watendaji wa muda watasaidia kuharakisha zoezi hilo.

"Kumekuwa na ongekezo la viwanda na miradi katika maeneo mbalimbali hapa nchini ambayo kwa asilimia kubwa NEMC haiitambui na hivyo tumejipanga kufanya ukaguzi nchi nzima ili kubaini ni miradi gani na viwanda vilivyopo vimesajiliwa na visivyosajiriwa vipate utaratibu," alisema.

Alisema kuna umuhimu wa kusajili miradi ili ifanyiwe Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA) ambapo itapelekea mwenye mradi kuendeleza biashara yake kwa kufuata sheria na kanuni za mazingira pasipo kuleta athari katika mazingira kutokana na mradi wake.

"Zoezi hili litasaidia sana kuongeza mapato ya baraza kupitia tozo za kila mwaka kwa wenye miradi, hii itatokana na kupata orodha kamili ya miradi na viwanda nchini kupitia ukaguzi utakaofanywa hivi karibuni," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema kuongezeka kwa mapato ndani ya baraza kutasaidia utekelezaji wa uhakika wa majukumu ya NEMC kwa kutatua changamoto mbalimbali ikiwamo upungufu wa wafanyakazi na pia vitendea kazi na kuongeza ufanisi wa baraza.

"Naamini kwa hatua hii itapelekea miradi mingi kusajiliwa na ufuatiliaji wa karibuni wa maendeleo ya miradi hiyo sambamba na utunzaji wa mazingira unatekelezeka kama sheria na kanuni za mazingira inavyotaka," alisema.

Dk. Gwamaka aliongeza kuwa kuongezeka kwa mapato ya NEMC kutachangia pia ongezeko la gawio Serikali Kuu ambapo fedha hizo zitakwenda kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa reli ya kisasa na mingineyo mingi.

"Mikakati ya baraza ni kuhakikisha kwanza sheria na kanuni za mazingira zinaeleweka miongoni mwa wadau na zinafuatwa," alisema na kuongeza kuwa baraza limejipanga na kujizatiti kufikia malengo yake.

Alisema elimu elekezi itaendelea kutolewa ili kuwajengea uwelewa wananchi juu ya sheria za mazingira na umuhimu wa utunzaji wa mazingira na athari zake kama mazingira hayatatunzwa vizuri kutokana na shughuli za kibinadamu.

Dk. Gwamaka ameelezea pia mafanikio ya ziara yake kanda ya kusini ambako mbali ya kukagua miradi ameweza kujionea changamoto mbalimbali wanazo kabiliana nazo maofisa mazingira katika maendeleo husika.


SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




TAIFA STARS VS KENYA

JULAI 28, 2019 • UWANJA WA TAIFA

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

MAKAO MAKUU
Ghorofa ya 4, Jengo la PSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni Taasisi inayojitegemea ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA inawajibu wa kuzidhibiti sekta hizi kiufundi na kiuchumi. Mamlaka ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida ya halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/No | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Lead Oil (T) Ltd S.L.P 10422 Arusha | Kiwanja Namba 424, Kitalu "E", Eneo la Unga Limited, Wilaya ya Arusha Mjini, Mkoa wa Arusha | Yusuph Ahmed Mohamed (Kenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 2. | General Petroleum Limited S.L.P 106132 Dra es salaam | Kiwanja Na. 289/290, Kitalu "T", Eneo la Miburani, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es salaam | Qazi Imran Khan (Raia wa Pakistani) | Leseni ya kutengeneza vilainishi |
| 3. | Sinohydro Corporation Limited S.L.P 70589 Dar es salaam | Kiwanja Na. 428, Mtaa wa Karume Road, Eneo la Kawe, Wilaya ya Kinondoni, Jiji la Dar es salama | Hou Zhenyu (Raia wa China) | Leseni ya Kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 4. | Benedictine Abbey Ndanda S.L.P 25 Ndanda | Kiwanja Na. 21, Kitalu "D", Eneo la Ndanda Mission, Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara | Aron Holela (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 5. | Goba Mchigani - Madale Petrol Station S.L.P 62032 Dar es salaam | Kiwanja Na.248, Kitalu "B", Madale, Wilaya Kinondoni, Dar es salaam | Aneth Biteya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha mafuta |
| 6. | Hemed Barakat Salehe S.L.P193 Kilwa | Mtaa wa Kibo, Eneo la Lukuledi, Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara | Hemed Barakat Salehe (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha mafuta |
| 7. | Gibaso Holding Co. Limited S.L.P 8623 Dar es salaam | Kiwanja Na. 2003, Kitalu "A", Kisewe, Eneo la Chamazi, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es salaam | Joseph Kyalo Mwita (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha mafuta |
| 8. | Lira Oils Limited S.L.P 7305 Dar es salaam | Kiwanja Na. 85, Kitalu "D", Eneo la Chanika, Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es salaam | Ester Urasa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha mafuta |

215330402

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa juu.

# Mateso ya kuishi na mashine yamlazimu kuomba msaada

**Na Beatrice Shayo**



HAMAD Awadhi (28), anaishi kwa mateso ya kulazimika kutumia mashine ya kumsaidia kupumua (oxygen) muda wote hali inayomfanya aombe msaada kwa wafadhili wa kumwezesha kulipia gharama za umeme na gesi ya mashine hiyo ili aendelee kuishi.

Awadhi alikuwa amelazwa kwa matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili – Mloganzila na wiki iliyopita aliruhusiwa kutoka baada ya kukaa kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Hospitali hiyo ilimsaidia mashine hiyo ya kupumulia yenye thamani ya Sh. milioni 3.5 ili kuokoa uhai wake na afya yake kuendelea kuimarika.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe jana nyumbani kwake Ukonga Majumba Sita, jijini Dar es Salaam, Awadhi anasema licha ya kupatiwa msaada huo, lakini anaishi maisha magumu.

Anasema angesaidiwa kupatiwa matibabu ya ugonjwa wake akapona ingemsaidia kuendesha familia yake kama ilivyokuwa awali.

Kwa sasa anasema kula yake ni ya shida na nyumba anayoishi ni ya kupanga ambayo anatakiwa kulipa kodi anayodaiwa.

"Kama unavyoniona hali yangu ni kuzunguka na hii mashine maishani mwangu, ningepatiwa msaada hata wa matibabu au wakaniwezesha kiuchumi ili niweze kuilea familia yangu maana kulala mwaka mzima hospitali kumenirudisha nyuma," alisema.

### UGONJWA ULIVYOANZA

Anasema Machi mwaka jana, alianza kuumwa kwa kuishiwa nguvu na kushindwa kupumua. Alikwenda Hospitali ya Amana, Ilala jijini Dar es Salaam na kuanzishiwa matibabu na baada ya muda alipelekwa Hospitali ya Mloganzila.

"Nilivyofikishwa hapo Mloganzila niliwekwa katika chumba maalum kwa kuwa hali yangu ilikuwa ni mbaya kila wakati inabadilika, pumzi inakata na nguvu inaniishia," anasimulia. Alifanyiwa vipimo mbalimbali na jopo la madktari bingwa na majibu ya vipimo vilionyesha moyo wake umehama kutoka kushoto kwenda kulia na mapafu yamesinyaa hayana uwezo wa kupumua yenyewe. "Ndio kama hivi siwezi kupumua bila mashine wakaniambia unahitaji kifaa cha kupumua maana uwezo wa kupumua bila mashine hauna," anasema.

Alipatiwa barua ya kuomba msaada, lakini kutokana na hali yake alishindwa kuipeleka kwa watu kuomba msaada na kuendelea kukaa hospitalini hapo.

Ulipokuja uongozi mpya wa hospitali hiyo aliwasilisha maombi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Dk. Julieth Magandi, ili aweze kupatiwa msaada.

"Viongozi wa hospitali hiyo walisikia kilio changu na kunipatia msaada wa hii mashine na kuruhusiwa kwenda nyumbani bila hivyo ungekuta nipo hospitali bila kujua hatima yangu ya kutoka."

Pamoja na kupatiwa msaada wa mashine hiyo pia alifutiwa deni lake la zaidi ya Sh. milioni tisa ambazo asingeweza kuzilipa kutokana na kukosa uwezo wa kifedha.

"Viongozi wa hospitali yule mama Museru na wafanyakazi wote wamenipambania, bila Mloganzila nisingekuwa hapa wamenisaidia sana kwani hiyo hela nisingeweza kuilipa nina washukuru sana kwa msaada mlionipatia."

Alikuwa anaumia kuona wagonjwa wenzake wanaondoka na wengine kufa huku yeye akiendelea kuongeza siku hospitali.

"Mimi ni miongoni mwa wagonjwa waliokaa muda mrefu hospitalini hapo najulikana hospitalini hapo hadi getini kwa walinzi, yaani kama nilikuwa nipo nyumbani maana wafanyakazi wa hospitali lazima ukutane nao kila siku."

### AMWOMBA RC PAUL MAKONDA

Anasema changamoto kubwa baada ya kurejea nyumbani ni familia kumtegemea akiwa baba wa watoto wawili kwa kuwa mke wake hafanyi kazi. "Ningeomba Mkuu wa Mkoa Paul Makonda, anipatie hata msaada niweze kufungua biashara ambayo itaniwezesha kupata hela ya kuendesha familia yangu hata wasanii ama kampuni naomba mnisaidie napitia wakati mgumu," aliomba.

Awali ililazimika kuuza baadhi ya vitu vya ndani ili kulipia matibabu yake na baadaye alishindwa kufanya hivyo ndipo hospitali ikamsamehe deni hilo.

Awadhi anasema kwa sasa anatakiwa kulipa kodi ya nyumba na gharama za umeme amependishiwa kutokana na mashine hiyo kutumia umeme kila siku. "Hii mashine inatumia umeme, ukikatika haifanyi kazi inanigharimu umeme na nyumba niliyopanga ina wapangaji wengi inakuwa changamoto katika utumiaji wa umeme inanilazimu kuongeza fedha maana ninaonekana natumia umeme mwingi kutokana na mashine hiyo kuwaka wakati wote."

Anasema umeme unapokatika inamlazimu kutumia mtungi wa gesi ambao huwa anatakiwa kuujaza kwa Sh. 25,000.

"Mashine isipofanyakazi hapa utanionea huruma hali yangu inakuwa ni mbaya zaidi sasa ikatokea nikakosa hela ya kulipia umeme au huu mtungi wa gesi, uhai wangu unaondoka haya ni maisha magumu usiombe ukakutana na hili tatizo langu."

Anasema wakati mwingi huwa anatumia dawa za kupuliza ambazo huzitumia kwa

INAENDELEA UK. 8

# Mshtakiwa aomba kortini kukiri kuua bila kukusudia

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili Joseph Mahende ya mauaji ya mke wake, Mosi Kitaleti, umeiomba mahakama kuupa nafasi ya kukiri kosa la kuua bila kukusudia baada ya kupitia ushahidi wa kesi nzima.

Kadhalika, umeiomba mahakama kuupa nafasi hiyo ili usipoteze muda wa mahakama baada ya kufanya upembuzi na ushahidi wote wa kesi hiyo.

Jana kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji, iliyoketi chini ya Naibu Msajili, Pamela Mazengo.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali, Debora Mcharo na Benson Mwakipenda.

Hata hivyo, Wakili wa Utetezi, Nehemiah Nkoko, alidai kuwa baada ya kupitia ushahidi mzima upande wa utetezi uko tayari kukiri mahakamani kosa la kuua bila kukusudia.

"Mheshimiwa tunawasilisha hoja yetu kwamba mshtakiwa yupo tayari kukiri kosa la kuua bila kukusudia ili tusipoteze muda wa mahakama," alidai Nkono.

Akijibu hoja hiyo, Mcharo alidai kuwa upande wa Jamhuri unaomba muda wa kujadili hoja za utetezi kuhusu ombi lao ili wawasilishe majibu mahakamani.

Msajili alisema kwa kuwa upande wa Jamhuri umeomba muda wa kujadili hoja za utetezi, kesi hiyo imepangwa kusikilizwa leo.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Januari 10, 2016 eneo la Kivule Matembele, Wilaya ya Ilala, mshtakiwa alimuua kwa makusudi mke wake Kitaleti.

## Wakulima korosho wakunwa udhamana mkopo

**Na Mwandishi Wetu,**
MTWARA

WAKULIMA wa korosho wilayani Tandahimba mkoani Mtwara wameishukuru serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) kwa kuwezesha upatikanaji wa dhamana ya mkopo yenye thamani ya Sh. bilioni moja wa Benki yao ya Ushirika Tandahimba (TACOBA).

TADB wamekuwa katika utekelezaji wa maagizo ya Rais John Magufuli yakuwataka kuwafikia wakulima moja kwa moja ili kuchagiza maendeleo ya sekta ya kilimo na kufanikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

Akizungumza na wakulima muda mfupi baada ya kukabidhi hundi hiyo kwa

Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba, Sebastian Waryuba, Mkurugenzi wa Fedha wa TADB, Derick Lugemala, alisema benki yake imeshaanza kuzipitia Benki za Ushirika na Kibiashara kupitia mpango wa dhamana ya mikopo ambao unalenga kuwasaidia wakulima wadogo.

"Jukumu letu ni kuchagiza ukuaji wa kilimo kwa kumpatia mkulima pesa ambazo atawekeze na mwishowe apate mafanikio katika uwekezaji huo," alisema.

Katika kutekeleza agizo la Rais la kuhakikisha wakulima wananeemeka na uwepo wa TADB, benki hiyo imefungua ofisi za kanda Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza ili kusogeza huduma zake kwa wananchi.

"Serikali imejipambanua vizuri katika dhamira yake ya kujenga uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025, hivyo kila taasisi lazima ijipambanue vyema katika kuweka mipango yake na sisi tumeshafungua ofisi za kanda ili kuwafanya wakulima watufikie kwa urahisi," alisisitiza Lugemala.

Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba, Waryuba aliipongeza TADB kwa kusogeza huduma kwa wananchi hali ambayo itachangia ongezeko la mapato. "Sasa wakulima wanaona faida za moja kwa moja za uwepo wa benki hii kwani pesa ambazo zimetolewa zitasaidia wakulima wasio na pesa kukopa kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo hali itakayochochea sana kuinua mapato hapa Tandahimba," alisema.

Zainabu Chivalavala, mkulima wilayani humo, aliishukuru benki hiyo kwa kuongeza matumaini mapya kwa wakazi wa Tandahimba.

TAARIFA KWA UMMA

Benki ya CRDB inapenda kuwataarifu wateja kuwa huduma zetu sasa zimerejea katika hali ya kawaida na ubora uliozoeleka.

Siku chache zilizopita kulitokea hitilafu kwenye mfumo wa kutolea huduma na kupelekea upatikanaji usioridhisha wa baadhi ya huduma na hivyo kusababisha usumbufu kwa wateja wetu.

Benki ya CRDB inawaomba radhi wateja, wabia na umma kwa ujumla kwa usumbufu wowote uliojitokeza na kuwahakikishia kuwa itaendelea kuboresha mifumo yake ili kuwapa huduma bora, za uhakika na salama zaidi.

Tunawashukuru wateja wetu kwa ustahimilivu waliouonyesha na kwa kuendelea kutuamini na kutufanya kuwa Benki kinara nchini Tanzania na Burundi.

Kwa maoni, ushauri au maelezo zaidi tafadhali usisite kuwasiliana nasi kupitia
**+ 255 755 19 77 00**

**Imetolewa na: Uongozi wa Benki ya CRDB**




crdbbank Plc www.crdbbank.co.tz

CRDB BANK
The bank that listens

215330301

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TCU ifanyie kazi kauli ya Majaliwa wanaosoma nje

**UTARATIBU** wa wanafunzi wa elimu ya juu kujitafutia vyuo vya nje kwa ajili ya kudahiliwa pamoja na wa serikali kuwapatia ufadhili wa nafasi za masomo ughaibuni, umechangia sana katika kupanua wigo wa nafasi za masono ya elimu ya juu.

Kimsingi, tunaweza kusema kuwa hatua hiyo imepunguza tatizo lililokuwapo la ongezeko la wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu, lisilolingana na vyuo vilivyopo nchini.

Pale wenye sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu wanapopata nafasi za masomo katika vyuo vya elimu ya juu ughaibuni, kunatoa unafuu kwa sababu wengine wenye sifa wanapata fursa ya kudahiliwa na vyuo vya nchini.

Pamoja na utaratibu kuwa mzuri na wenye manufaa, kumekuwapo na changamoto kwa wanaokwenda masomoni ughaibuni hususan wanaporejea nchini.

Changamoto ambayo wamekuwa wakikumbana nayo ni Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kutowatambua, jambo ambalo linawasababishia vikwazo na kuwanyima fursa.

Wahitimu wetu wengi waliosoma katika vyuo vya nje wamekuwa wakipata wakati mgumu kutokana na TCU kuwachukulia kana kwamba shahada zao hazitambuliki nchini. Hiyo ina maana kuwa mhusika hawezi kutumia cheti kufanyakazi nchini wala kukitumia kudahiliwa kuchukua masomo ya juu zaidi.

Kwa mfano, akitaka kusoma shahada ya pili (uzamili) shahada yake ya kwanza haiwezi kutambulika na mhitimu aliyepata shahada ya uzamili ughaibuni akitaka kudahiliwa nchini kusomea shahada ya uzamivu nchini atakwama.

Kadhalika, kuna baadhi ya wahitimu waliosomea nje na kupata utaalamu kama udaktari, uhandisi na taaluma nyingine, lakini wanaporejea nchini vyeti vyao havitambuliwi na TCU, hivyo kuikosesha serikali fursa ya kuutumia utaalamu wao.

Hata hivyo, jambo la kutia matumaini ni kuwa hata serikali imeliona tatizo hilo na kuamua kutoa maelekezo kwa TCU.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ameiagiza Tume hiyo kukaa na taasisi zinazojishughulisha kupeleka Watanzania nje ya nchi kusoma masomo ya elimu ya juu na kufanyia kazi malalamiko yao.

Amesema kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya wanafunzi hao kuwa wanaporudi nchini, tume kutovitambua vyuo walivyosoma.

Majaliwa alitoa maelekezo hayo juzi jijini Dar es Salaam, akifungua Maonyesho ya 14 ya Vyuo Vikuu yaliyoandaliwa na TCU na kuvishirikisha vyuo mbalimbali.

Majaliwa alisema kuwa alimdokeza Mkurugenzi Mtendaji wa TCU kwamba wiki mbili zilizopita alipokuwa ziarani nchini Misri, alipata fursa ya kuzungumza na Watanzania miongoni mwao ni wanafunzi wa vyuo vikuu wanaosoma nchini humo.

Alisema miongoni mwa malalamiko ni chuo kikuu kimoja ambacho hakukitaja jina kuwa kuna malalamiko kuwa Watanzania wanaosoma hapo wakimaliza na kupata vyeti vyao havitambuliki na TCU, na kuwa kuna idadi kubwa ya Watanzania wanasoma hapo. Hatua ya Waziri Mkuu kuguswa na jambo hilo na kuamua kuieleza TCU ni jambo muhimu sana, kwa kuwa Watanzania wanaopata fursa za kusoma vyuo vya nje wananyanyasika.


Hatusemi kuwa TCU isitekeleze wajibu wake kwa kufanya ufuatiliaji wa vyuo vya nje na vya ndani kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanaosoma kule wanapata elimu yenye viwango bora.

Hata hivyo, Tume isivuke mipaka kwa kuweka vigezo na taratibu ambazo zinakandamiza hata waliosoma katika vyuo bora kwa lengo la kuwakomoa.

Tunaishauri Tume kujitafakari ikiwamo kukaa na vyuo hivyo kuzungumza, kwa kuwa haiingii akilini kuona kwa nini cheti hicho hakitambuliki na kama havitambuliki kwa nini wanawapeleka Watanzania pale wakiwamo wanaopelekwa kwa udhamini wa serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hatua hizi zitarejesha, kuongeza ajira zaidi

**MKUU** wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameshaeleza nia ya kurejesha utaratibu wa kufanya biashara kwa saa 24 ikiwamo ya baa na maduka ili kuongeza mzunguko wa fedha na makusanyo.

Hivi karibuni alisema mpango wa biashara hizo na nyingine upo katika hatua za mwisho za kukamilika na kisha utazinduliwa rasmi ili kuwawezesha wakazi wa Dar es salaam kufanya shughuli zao bila usumbufu.

Anasema taratibu za kufungua biashara kwa saa 24 jijini humo zimekamilika isipokuwa baadhi ya mambo ya usalama, ambayo yanakamilishwa na Kamanda wa Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa.

Makonda anawahimiza watendaji wa wilaya zote kusimamia ukamilishwaji wa kuwa na maeneo ya vituo vya pikipiki na bajaji ili wafanyabiashara hao watambulike na kufanya kazi kwa uhuru.

Ninachotaka kujadili hapa ni kwamba utaratibu huu kama utakamilika unaweza kuongeza ajira, kwenye sehemu kama za maduka ya dawa, supa maketi, hoteli, baa na zahanati ni dhahiri idadi ya wafanyakazi itaongezeka na kuwa mwanzo wa ajira mpya.

Kuongeza muda ni jambo jema hasa kwa wanaouza vileo, hii inatokana na ukweli kwamba vibali vya ukomo wa saa sita usiku vinadaiwa kuwa ni changamoto kwa wamiliki wa baa, ambao wamewahi kusema vilisababisha wapunguze wafanyakazi.

Kuna mmiliki mmoja wa baa aliwahi kusema vibali hivyo vilisababisha apunguze wafanyakazi zaidi ya 30 na kubaki na wachache kwa vile hata mapato ya baa yalipungua.Kwa maelezo hayo inawezekana wakawapo wafanyabiashara wengi walioathiriwa na vibali hivyo, ambavyo sasa Makonda anataka viondolewe ili kuruhusu biashara kufanyika saa 24.

Mbali na wamiliki wa baa, wamachinga na wafanyabiashara wengine, hata vikundi vya burudani zikiwamo bendi vinaweza kuongeza ajira, kwa vile baadhi yake vilishapunguza wafanyakazi.

Huwa ni kawaida kwa wapenzi wa muziki wa dansi kuingia katika kumbi kuanzia saa nne au saa tano, lakini hatua ya kufunga kumbi saa sita usiku ilisababisha wengi wao kutokwenda katika kumbi hizo.

Mazingira hayo yamechangia vikundi kukosa mashabiki na hivyo kutopata mapato ya kutosha na kulazimika kupunguza wafanyakazi ili kukabiliana na hali halisi ya biashara.

Lakini sasa inawezekana wakaondokana na hali hiyo, kufuatia mpango unaondaliwa wa kutaka biashara ifanyike saa 24 huku kukiwa na ulinzi wa kutosha wa watu na mali zao.

Inawezekana Makonda ameona athari za zuio hilo na sasa ameamua kuja na njia hiyo mpya ili kuongeza ajira na pia kuongeza mapato kwa serikali.

Kwa mujibu wa Makonda, kilichokuwa kikisubiriwa ni Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akamilishe taratibu za ulinzi na kwamba Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, angezindua utaratibu huo wa kufanya biashara saa 24 mwezi Juni.

Hii yote inaonyesha ni jinsi gani serikali ilivyopania kuhakikisha biashara inafanyika katika mazingira salama huku kwa upande mwingine kuwezesha kukusanya kodi kama kawaida kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Ninadhani sasa ni wakati kwa wafanyabiashara kuchangamkia fursa hiyo ili waweze kunufaika nayo na ikiwezekana waongeze ajira kwa vijana wa kike na kiume, ambazo baadhi yao wanakiri kwamba zilipungua.

Ubunifu huo wa Makonda unaweza kuwa na manufaa kwa wafanyabiashara ikiwamo kukuza biashara zao, na kwa upande wa serikali itakusanya kodi, hivyo watendaji wa mkoa wake wafanyie kazi maelekezo waliopewa.

Miongoni mwa maelekezo hayo ni kuimarisha usalama wa maeneo, kusimamia ukamilishwaji wa kuwa na maeneo ya vituo vya pikipiki na bajaji ili wafanyabiashara watambulike na kufanya kazi kwa uhuru.

"Maana ya jiji la Dar es Salaam kuwa Jiji la kibiashara ni pamoja na kuwawezesha wafanyabiashara kufanya kazi kwa saa 24. Kwa sasa baa zinafunguliwa hadi saa sita usiku, lakini mpango wetu zifunguliwe muda wote ili serikali ipate mapato", anasema Makonda.

Anasema , mfanyabiashara afanye biashara muda wote, kama usalama upo na hapigi muziki unaosababisha usumbufu kwa wengine, na kwamba hatua hiyo ni nzuri kwa vile ni ishara ya kuwapo kwa usalama.

# Utaratibu mpya usajili, utoaji hatimiliki ardhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema itaanza kufanya usajili na utoaji wa hatimiliki za maeneo pamoja na nyaraka zote katika ngazi za mikoa ili kuwapunguzia wananchi gharama na muda wa kufuatilia katika ofisi za kanda.

Hatua hiyo ilitangazwa jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alipokuwa akifungua kikao kazi cha wataalamu wa sekta ya ardhi jijini hapa.

Alisema kuwa wananchi wamekuwa wakipata shida kupata hatimiliki zao za maeneo kutokana na ofisi nyingi kuwapo katika maeneo ya kanda pekee yake.

"Nataka hatimiliki zote zitolewe na kusajiliwa mikoani kwani watu wamekuwa wakipoteza muda na gharama nyingi za usafiri kufuatilia hati, hivyo hatuwatendei haki hawa wananchi wanyonge kwa kuwatwisha mzigo wa gharama," alisema Lukuvi.

Lukuvi alisema haitakuwa na maana kwa serikali kama itaendelea kuwapa mzigo wa gharama wananchi wake wakati wa ufuatiliaji wa hatimiliki za maeneo yao.

"Hakuna maana kusema kuwa tunawasaidia wananchi kupata hatimiliki za maeneo yao, huku gharama wanazozitumia ni nyingi... leo hii unakuta mtu anatoka Kigoma anakuja Tabora kufuata hati, lakini tofauti na nauli anatumia siku saba hadi kumi kukamilisha zoezi hilo," alisema.

Aidha, aliwaonya watumishi wa idara za ardhi nchini kuacha tabia ya kupandisha bei ya maeneo pamoja na gharama za upimaji kwa madai kuwa wanajiongezea mapato ya ndani.

Alisema bei ya viwanja lazima ziwe kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na siyo kila mtu kujipangia bei zake ambazo zinageuka kuwa kero kwa wananchi.

Pia, alizionya kampuni za upimaji ambazo zimekuwa zikijihusisha na utapeli kwa kuchukua fedha za wananchi bila kukamilisha miradi ya upimaji.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Doroth Mwanyika, alisema lengo jingine ni kupunguza migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikisababisha kudorora kwa shughuli za uzalishaji mali ikiwamo na kuondoa tatizo la kiwanja kimoja kumilikishwa kwa mtu zaidi ya mmoja.

## 5,000 wawezeshwa kusoma nje vyuo vikuu

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Global Education Link imewawezesha wanafunzi 5,000 kwenda kusoma katika vyuo mbalimbali nje ya nchi.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa Tawi la kampuni hiyo Mkoa wa Dar es Salaam, Regina Lema, wakati akizungumzia maendeleo ya miaka mitatu tangu kuanzishwa kwa kampuni hiyo mwaka 2016.

Regina alisema mwitikio wa wanafunzi kwenda kusoma nje ya nchi umekuwa mkubwa jambo ambalo limesaidia kuongezeka kwa wataalamu wengi nchini.

Alisema mwitikio huo pia unatokana na ufaulu mzuri wa wanafunzi hao waliopata nafasi ya kusoma nje ya nchi.

Alisema kampuni yao imekuwa ikiwafuatilia wanafunzi hao kuanzia hatua ya ushauri, pamoja na kupita shule mbalimbali kutoa elimu juu ya kozi gani wanaweza kusoma chuo kikuu.

Alisema kila mwanafunzi anayechagua chuo cha kusoma nje ya nchi kupitia kampuni yao wanamfanyia mchakato wa udahili, utafutaji wa visa, hati ya kusafiria pamoja taratibu nzima ya vibali vya serikali.

"Baada ya hapo sisi pia tunafanya mchakato wa kumtafutia tiketi na mara nyingi wanafunzi wetu

INAENDELEA UK. 8




## HABARI KITAIFA

# Wadau watoa ya moyoni sakata Kinana, Makamba

INATOKA UK. 2

watendaji wakuu wa chama na si Baraza la Wazee ama sivyo wangeenda mahakamani kama alivyofanya mwenzao Benard Membe, vinginevyo hawawezi kupata matokeo mazuri zaidi ya kujichafua zaidi na kuzidi kufedheheka," Dk. Bana alisema.

Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, alisema ni mapema kuyaongelea makundi yanayoibuka lakini kunahitaji uangalifu kutokana na athari zake kwa ustawi wa nchi.

Alisema suala hilo linapaswa kushughulikiwa kwa haraka kwa kuwa linamgusa Rais na haijajulikana wananchi wako upande upi katika mgogoro huo.

"Kama jambo hili litaendelea katika sura hiyo, maana yake mustakabali wa chama na taifa unakuwa haukai vizuri kwa sababu Rais ni taasisi.

"Utakuwa unagusa watu wengi unapojaribu kumvunjia heshima Rais, unawagusa Watanzania wengi, hili jambo halipendezi kuachwa liendelee, umakini mkubwa unahitajika wa namna ya kuyatazama haya makundi ili yasilete athari kwa watu," alisema.

Kiongozi huyo wa dini alitoa wito kwa pande zinazohusika, kutumia hekima na busara katika kushughulikia changamoto zilizojitokeza kati yao.

"Bahati nzuri wana vikao vyao vya chama na serikali ina taratibu zake za kuona namna ya kulishughulikia. Vyombo vya ulinzi na usalama navyo vichukue nafasi yake, kuna kauli inasema 'moto mkubwa huanza na cheche ndogo', hata vyombo vya ulinzi na usalama vione, visidharau yanayoendelea," alishauri.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, Onesmo Olengurumwa, alisema Makamba na Kinana wametoa tahadhari kwamba hali ikiachwa ikaendelea hivi kutaligawa taifa na kuna uwezekano mkubwa wa kuingia katika mazingira magumu ya amani na utulivu.

"Kinana na Makamba walimelisaidia taifa kwamba wazee wastaafu waliopo waingilie kati kwa kuwa wapo waliokwenda kwenye vyombo vya habari na mahakamani lakini hali haijabadilika.

"Kama hili la Makamba na Kinana halitaweza kutatua na kujenga mazingira ya mtu huyu kudhibitiwa kwa mujibu wa sheria ya nchi, itakuwa na tafsiri kwamba mtu mmoja asipodhibitiwa ana uwezo wa kuvunja amani na taifa likavurugika kabisa kama tulivyoona kwenye nchi nyingine.

"Kuna watu wameitwa wahaini, mawakala wa mabeberu na majina mengineyo mabaya, bado aliyetaja hayo na kuandika kwenye chombo cha habari, ameachwa na chombo anachotumia kimeendelea kuachwa bila kuchukuliwa hatua, ni kuliingiza taifa kwenye mgawanyo mkubwa. "Ni sawa na simba anayekula nyama ya mtu na akiachwa ataendelea kula, ni tabia ambayo ikiachwa ikaendelea ni jambo baya sana. Ilipaswa kuchukua hatua toka awali lakini ameendelea kuachwa."

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Anna Henga, alisema tofauti za kimtazamo zilizoibuliwa na wazee hao zilipaswa kufanyiwa kazi ndani ya chama kwa kuwa wana utaratibu wao wa chama.

"Nilitegemea walioandika barua wangeomba usuluhishi na anayewasema vibaya, ungeweza kufanyika ndani kwanza kabla ya kwenda kwa umma. Sidhani kama inaelekea mahali pazuri mpasuko kwa viongozi wakubwa kama hao," alisema.

"Inawezekana alikosea kuwasema lakini chama kingechukua hatua ikiwamo kumuonya kuliko majibizano ya barua, ni vyema kama wameshindwa kuelewana ndani, waende mahakamani.

"Nadhani wafanye usuluhishi ndani ya chama chao kwa kuwa ni kikubwa na kina mifumo ya kushughulikia mambo kama hayo. Tunahitaji amani zaidi kuliko malumbano sisi kama Watanzania," alisema.

Wakili Hudson Ndusyepo, alisema barua ya malalamiko iliyoandikiwa na Makamba na Kinana inazua maswali kisheria na kisiasa.

Alisema barua hiyo ingekosa vigezo kama ingekuwa inapaswa kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria, akibainisha kuwa kisheria hairuhusiwi kuunganisha malalamiko ya kuvunjiwa heshima kwa kuwa kila mmoja ana heshima yake binafsi.

"Kila mmoja alipaswa kuandika malalamiko yake binafsi, lakini kwa kuwa wameiandika kisiasa, pia inaacha maswali kwanini wameamua kufikisha malalamiko yao kwenye baraza hilo, huyo wanayemlalamikia ni mwanachama, ana wadhifa gani ndani ya chama hicho?" Alihoji.

Alisema hatua iliyochukuliwa na wawili hao pia inaibua hoja nyingine kwamba huenda kuna watu wanajiita wanaharakati ilhali wana nyadhifa za siri zisizojulikana kwa jamii lakini chama husika kinawatambua.

**●Imeandikwa na Enock Charles, Beatrice Moses, Romana Mallya na Salome Kitomari**

## Kiama wahalifu

INATOKA UK. 3

mpigakura kwa baadhi ya asasi za kiraia, rai yangu kwa asasi zote za kiraia zilizopata vibali hivyo kuendelea kutoa elimu hiyo kwa wananchi kwa kuzingatia mwongozo wa elimu ya mpigakura iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, na wala msijihusishe kukisemea chama chochote, elezeni umuhimu wa kujiandikisha, umuhimu wa kupiga kura, umuhimu wa kupata kiongozi uliyemchagua."

Tahadhari ya Waziri Mkuu, Majaliwa, kuhusu watakaojiandikisha zaidi ya kituo kimoja ilitokana na tungo za wimbo wa hamasa ulioimbwa na kiongozi wa kikundi cha utamaduni wa ngoma za asili aitwate 'Biusi' kabla ya hotuba yake.

Tungo hiyo ilikuwa na maneno yanayoeleza kuwa kuna watu wanadanganywa njoo jiandikishe hapa na pale, utapiga kura tu, twakuomba Waziri Mkuu, watu watakaojiandikisha zaidi ya mara moja waswekwe ndani.

**MWENYEKITI NEC**

Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu, Semistocles Kaijage, alisema tume katika kujiandaa na uboreshaji wa daftari, iliendesha zoezi la uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapigakura nchi nzima, zoezi ambalo lilifanyika mwaka jana.

Jaji Kaijage alisema, lengo lake lilikuwa ni kuona kama vituo hivyo bado vipo na kama bado vina hadhi ya kuwa vituo vya kuandikisha wapigakura kwa mujibu wa sheria.

"Na vile vile kuangalia iwapo kuna maeneo yanayohitaji kuongezewa vituo, kwa upande wa Tanzania Bara, tume iliongeza vituo vya kuandikisha wapiga kura kutoka 36,549 hadi 37,407, vituo 6,208 vimebadilishwa majina, vituo 817 vimehamishwa kutoka kijiji au mtaa mmoja kwenda mwingine na vituo 19 vimehamishwa kutoka kata moja kwenda kata nyingine," alisema.

## 5,000 wawezeshwa

INATOKA UK. 7

hutumia ndege moja kusafiri unakuta wanafunzi 50 wanasafiri kwa pamoja wakiwa na wafanyakazi wetu wanne," alisema.

Alisema wanafunzi hao baada ya kufika huko wanawapeleka hadi chuoni na wakishaanza masomo ndipo wafanyakazi hao wanarejea nchini kwa ajili ya shughuli zingine.

Alisema ili kujua anachokifanya mwanafunzi akiwa masomoni, wanamfumo maalum ambao humfuatilia kuangalia matokeo yake ya mtihani, majaribio pamoja na mwenendo mzima wa maisha yake.

"Kipo pia kitengo kingine ambacho kazi yake ni kuhakikisha wanafuatilia maendeleo ya siku kwa siku ya wale wanafunzi yaani namna wanavyofanya kazi zake darasani, kuchukua matokeo na kuwapatia wazazi na masuala mbalimbali ya kijamii wanayoyafanya huko," alisema.

Alisema pia wanao umoja wa wazazi wa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi ambao umekuwa ukituma mwakilishi kuzunguka nchi mbalimbali ambazo wanafunzi hao wanasoma kwa lengo la kuangalia mienendo ya watoto wao.


**THE NATIONAL SERVICE CORPORATION SOLE**

SUMAJKT AUCTION MART

Efficiency and Excellence

**SUMAJKT AUCTION MART CO.LTD**

**MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **ACCESS BANK TANZANIA LTD** TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA NYUMBA ZIFUATAZO KAMA JEDWALI LINAVYOONESHA HAPA CHINI.

| S/N | JINA | MAHALI | DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | FRANK FELICIAN KASHONDA | MWANAGATI-ILA017203 | NYUMBA | 22/07/2019 SAA 4:00 ASBH |
| 2 | FRANK FELICIAN KASHONDA | REAL ESTATE(HOUSE) KITUNDA-ILA029069 | NYUMBA | 22/07/2019 SAA 6:00 MCHN |
| 3 | MIRAJI YASINI MASUDI | KINYEREZI-ALTENATIVE MORTGAGE | NYUMBA | 01/08/2019 SAA 4:00 ASBH |
| 4 | WILLIAM TITUS SILAYO | MBEZI-TITLE NO.114912 | NYUMBA | 09/08/2019 SAA 4:00 ASBH |
| 5 | MAIMUNA ABDALLA MPANDA | MJI MPYA SARANGA UBUNGO MUNICIPALITY | NYUMBA | 16/08/2019 SAA 4:00 ASBH |
| 6 | BEATRICE FRANCIS KWEKA | TANDIKA | NYUMBA | 17/08/2019 SAA 6:00 ASUBH |

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mteja anatakiwa kulipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14
2) Endapo mteja atashindwa kumalizia 75% ya salio lililobaki ndani ya siku 14 hatarudishiwa kiasi alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
3) Gharama zote za kubadili **HATI MILIKI ni JUU YA MNUNUZI.**

**Kwa mawasiliano zaidi piga namba:- 0716004554 NA 0753063481**

215330802


## Mateso ya kuishi na mashine yamlazimu kuomba msaada

INATOKA UK. 4

dakika chache anapotaka kwenda chooni kujisaidia ambazo huuzwa kati ya Sh. 18,000 na 25,000. "Wakati mwingine nikiishiwa dawa hizo inanibidi nijisaidie ndani kwa vile siwezi kutoka na mashine hadi choo cha nje."

Awadhi ambaye awali alikuwa anajishughulisha na ushushaji wa mizigo katika makontena Kariakoo, anasema kwa sasa anatafuta mtu amuuzie vifaa vyake vya nyumbani kwa kuwa maisha kwake yamekuwa ni magumu.

**NDUGU WAMSUSA**

Amesema baadhi ya ndugu zake hawana mawasiliano naye.

"Ndugu zangu wengine hali zao ni ngumu hao wengine kama wamenitenga fulani, maana mawasiliano tu ni shida nashukuru upande wa mama yangu na mke wangu unahangaika japo hali zao kiuchumi sio nzuri."

Catherine Kurikana, mke wa Awadhi anasema hana biashara anayofanya kwa sababu alikuwa anamuuguza mumewe kwa muda mrefu. Nyumba waliyokuwa wanaishia awali walihama kwa sababu ya kukosa kodi na kumlazimu kuhamia maeneo ambayo wapo ndugu zake ili wamsaidie.

Anasema familia yake ndio inahangaika kuwasaidia kwa chakula ingawa wakati mwingine wanapata mitihani ya kukipata.

"Hapa changamoto kubwa ni gharama ya kodi ambayo kwa mwezi ni Sh. 80,000 pamoja na umeme, kama ningekuwa na mtaji ningeanzisha biashara ili niendeshe familia maana mwenzangu ndio kama hivi ni mgonjwa kila kitu ananitegemea mimi."

# Heche alalamikia polisi kuzuia mikutano yake

Na Enock Charles

MBUNGE wa Tarime Vijijini (Chadema), John Heche, amelilalamikia Jeshi la Polisi Mkoa wa Mara kwa kumzuia kufanya mikutano ya kisiasa na wananchi jimboni kwake.

Akizungumza na Nipashe kwa simu jana, Heche alisema Jeshi la Polisi mkoani humo limemzuia kufanya mikutano licha ya kutoa taarifa kwa jeshi hilo kila wakati anapotaka kufanya mikutano.

"Siwaelewi na hawana sababu za msingi za kunizuia mimi kama mbunge kufanya mikutano katika jimbo langu, niliongea na RPC anadai wananipa adhabu kwa kuwa kipindi Ester Matiko ametoka gerezani niliende kufanya mkutano jimboni kwake," alisema Heche.

Awali, ulisambaa ujumbe wa video kwenye mitandao ya kijamii ukimwonyesha mbunge huyo akivutana na polisi na baadaye andiko la mbunge huyo akilalamikia polisi mkoani humo.

Gazeti hili lilimtafuta Kamanda wa Polisi mkoani humo, Henry Mwaibambe, kujua ukweli kuhusu lawama hizo za mbunge kwa Jeshi la Polisi, lakini simu yake iliita bila kupokelewa na alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi alijibu kwa kifupi kuwa ni kweli mbunge huyo alikiuka taratibu lakini hakufafanua taratibu hizo.

"Ni kweli kuna taratibu alikiuka tumeshamwambia," Kamanda Mwaibambe alijibu kwa kifupi.

Akizungumza na askari kwenye ziara yake ya kikazi mkoani Tabora jana, Mkuu wa Jeshi la Polisi, (IGP) Simon Sirro, alisema hawajakataza mikutano ya ndani wala ile ya wabunge kwenye majimbo yao.

Simon Sirro alisema mikutano ya ndani ya vyama vya siasa haijapigwa marufuku kama inavyozungumzwa.

Akizungumza na askari kwenye ziara yake ya kikazi mkoani Tabora juzi, IGP Sirro alisema mikutano hiyo inaweza kusitishwa tu pale itakapoonekana kwamba kuna viashiria vya uvunjifu wa amani.

"Mikutano ya ndani halijapigwa marufuku popote ila kama kuna taarifa za tishio la usalama kwenye mkutano huo tunaweza kuzuia kwa faida ya Watanzania," alisema

IGP Sirro kuwa mikutano hiyo inaruhusiwa kunapokuwa na mazingira ya amani na kwamba wahusika wanachotakiwa kuzingatia ni kufuata sheria na taratibu zilizowekwa kila wakati.

"Tunapokuwa tumezuia mikutano ya ndani watu wazingatie sheria na watii kwa sababu askari wanakuwa na taarifa zinazoweza kusababisha vurugu sasa tunawataka wahusika watii amri za polisi," alisema IGP Sirro.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge (kushoto), akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja wa Shirika la Bima Tanzania wa mkoa huo, Hamisi Msami, kuhusu kazi zinazofanywa na shirika hilo, wakati wa Siku ya Bima, iliyofanyika jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mhadhiri UDSM afichua ushiriki mdogo wanawake kwenye siasa

Na Romana Mallya

MHADHIRI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Consolata Sulley, amesema licha ya nchi kusaini mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda na kubadili sheria na kanuni, lakini bado kuna ushiriki mdogo wa wanawake kwenye siasa.

Dk. Sulley aliyasema hayo katika mkutano ulioandaliwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) wakati akiwasilisha mada ya jinsia na uwezeshaji wa wanawake katika masuala ya siasa.

Alisema bado kuna changamoto ya wanawake kushiriki kwenye siasa na uongozi ikilinganishwa na wanaume.

"Wanawake wengi ni wapiga kura wazuri ukiangalia takwimu za wapiga kura tupo wengi. Takwimu za mwaka 2015 zinaonyesha wanawake walioandikishwa kupiga kura walikuwa ni asilimia 53, waliotia nia walikuwa asilimia 28.7, waliogombea walikuwa asilimia 19, walioshinda ubunge asilimia 9.5 na waliochaguliwa kuwa madiwani ni asilimia 5.2," alisema.

Alisema kwa takwimu hizo wanawake waliojiandikisha kupiga kura walikuwa wengi, lakini waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wa kisiasa asilimia zilishuka.

Ofisa wa Programu wa TCD, Lucy Agustino, alisema kupitia mradi uliofadhiliwa na UN Women, wamelenga kuongeza idadi ya ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi uchaguzi ujazo.

"Ipo mikakati tuliyojiwekea, moja wapo ni viongozi wa vyama vya siasa, wakiwamo wastaafu walioshika nyadhifa mbalimbali kwenye serikali na vyama vya siasa kukaa nao, tunategemea mchango na maoni yao yatasaidia kuwashawishi viongozi wa vyama vya siasa waangalie upya mifumo ya uteuzi wa wagombea," alisema.

Alisema lengo la mkutano huo uliokutanisha wadau mbalimbali vikiwamo vyama vya siasa ni kujadili kwa pamoja hatua gani ambazo zinaweza kuchukuliwa ili uteuzi wa wanawake kwenye uongozi na siasa uongezeke.

Naye, mgeni rasmi kwenye mkutano huo, Mbunge wa Vunjo, James Mbatia, alisema yapo Malengo Endelevu ya Dunia 17 yanatakiwa yatekelezwe kwa misingi ya kipaumbele na kuyataja kuwa ni kuondokana na umaskini katika dunia, njaa, afya bora na ustawi wa jamii, elimu bora kwa wote, usawa wa jinsia, majisafi na salama.

"Ili yatekelezwe lazima tuwe na mifumo inayolinda utu wa binadamu, mifumo ya wazi, inayotoa haki, inayohakikisha amani ya dunia inalindwa. Hivyo Tanzania hatuna budi kuhakikisha usawa wa jinsi kama lilivyo lengo la tano, hasa kwa kuwa na utashi wa kisiasa wa kusimamia jambo hilo likaanzia kwenye mazingira ya kielimu," alisema.

## Mbunge ataka elimu ya mkaa

Na Christina Haule, MOROGORO

MWENYEKITI wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Suleiman Sadiq Murad, ameshauri elimu zaidi kutolewa kuhusu Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa nchini (TTCS) maarufu kama mkaa endelevu, ili watu wengi wafahamu kwamba unasaidia kutunza mazingira.

Akifungua warsha ya madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kuhusu tathmini ya mradi huo unaondeshwa katika vijiji 11 katika wilaya hiyo, Murad ambaye pia ni Mbunge wa Mvomero, alisema watu wengi bado wakisikia suala la ukataji mkaa wanadhani kila mara ni kuharibu misitu kufuatia janga lililopo sasa la mabadiliko ya tabianchi wakati mradi wa TTCS umeonyesha unatunza misitu kwa mujibu wa matakwa ya kukabiliana na mabadiliko hayo.

Alisema, watu wengi wana elimu ndogo kuhusu mkaa endelevu ambapo elimu ya kutosha ikitolewa itasaidia kuondoa kupigana na kupishana maelezo juu ya utunzaji wa misitu kwa ujumla kwa kutumia uvunaji misitu wa elimu ya mkaa endelevu.

Aidha, alisema sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2014 inapaswa kutumika ili kusaidia mradi wa mkaa endelevu kuendelea katika vijiji vya Wilaya ya Mvomero sambamba na kulinda mazingira kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Murad pia alishauri mradi huo kutokana na manufaa yake kupanua wigo zaidi katika wilaya mbalimbali za mkoa wa Morogoro ili nao kunufaika na utunzaji wa mazingira, huku wakiboresha kipato kwa kutumia mkaa endelevu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Jonas Zeeland, alisisitiza TTCS kuendelea kutoa elimu mara kwa mara kwa jamii ili izidi kuufahamu mradi huo wenye kuleta tija tofauti na wanavyofikiria.

Awali Meneja Mradi wa mradi wa TTCS, Charles Leonard, alisema mapato katika wilaya hiyo yamekuwa ni kidogo sana ukilinganisha na wilaya zingine za mradi ikiwamo Morogoro Vijijini na Kilosa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya ubovu wa miundombinu ya barabara na ukosefu wa masoko ya uhakika.

# Wanafunzi 4,000 wawekwa kambini kujiandaa mitihani

**Na Sabato Kasika**

JUMLA ya wanafunzi 4,133 wa darasa la saba toka shule za msingi 106 za Halmshauri ya Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, wamewekwa katika kambi za taaluma ili kujiandaa na mitihani wa kuhitimu elimu ya msingi.

Wanafunzi hao waliwekwa kambini tangu Julai 9 na watakuwa huko hadi Septemba 10 mwaka huu, wakiwa tayari wamepata muda wa kutosha wa kufundishwa na hata kujifunza.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Rukia Muwango, hiyo ni mara ya kwanza kwa wilaya yake kuweka kambi ya taaluma na anaamini itasaidia wanafunzi kufanya vizuri kwenye mtihani huo.

"Zipo kambi 34, zimewekwa maeneo mbalimbali ya kata za wilaya ya Nachingwea...mimi nimetoa Sh. milioni moja ikiwa ni mchango wangu kwa ajili ya kufanikisha kambi hizo," alisema Muwango.

Alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu na kuwataka walimu kufundisha kwa kufuata ratiba waliojiwekea na kuwa walezi wazuri wa watoto ili kambi hizo ziwe na mafanikio.

"Lengo letu ni kutaka watoto wasipoteze muda kwa mambo yasiyowahusu, ndio maana tumewaweka katika kambi ili waweze kujiandaa vya kutosha kwa ajili ya mtihani wa mwisho," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya pia anawaomba wadau wa elimu kujitokeza kwa wingi kuunga mkono kambi hizo kwa vile bado zina upungufu wa chakula na mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya wanafunzi.

Naye Ofisa Elimu Msingi, Makwasa Bulenga, alisema wilaya ina matarajio makubwa ya kambi hiyo, kwamba zaidi ya wanafunzi 3,720 watafaulu ikiwa ni sawa na asilimia 90.

"Kimkoa, wilaya yetu imekuwa ikishika nafasi ya tatu kati ya wilaya sita za mkoa wa Lindi, lakini safari hii tunaweza kufanya vizuri zaidi kwani ni mara yetu ya kwanza kuweka kambi," alisema Bulenga.

Alifafanua kuwa katika mtihani wa mwaka jana, wanafunzi 3,611 walifanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na kwamba wavulana 1,260 na wasichana 1,409 walifaulu mtihani huo sawa na asilimia 73.91.

"Kwa Nachingwea ni mara kwanza kuweka kambi, kwani tulikwama kuanza miaka ya nyuma kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo baadhi ya watu kutoona umuhimu wa kambi hizo na hivyo kujiweka pembeni," alisema.

Ofisa elimu huyo alisema, wazazi wameshaelimishwa, mwitikio wao katika uchangiaji wa kambi za taaluma unaridhisha kwa vile hadi sasa zaidi ya asilimia 80 wamekamilisha michango yao. "Yaani mtazamo wao kuhusu kambi hizi ni chanya, kwani wengi wao wamechangia vyakula, kuanzia mahindi, maharage au mbaazi na sukari kwa ajili ya watoto wao waliopo kambini muda wa miezi miwili," alisema.

# Ujenzi kivuko cha Kayenze sasa kukamilika Novemba

**Na Mwandishi Maalum**

UJENZI wa kivuko cha Kayenze kwenda Kisiwa cha Bezi mkoani Mwanza unaogharimu Sh. bilioni 2.7 unatarajiwa kukamilika Novemba mwaka huu.

Hayo yalibainishwa juzi wakati Mbunge wa Ilemela mkoani Mwanza ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, alipotembelea kivuko hicho kuangalia maendeleo ya ujenzi.

Kwa mujibu wa Mabula, kivuko hicho chenye uwezo wa kubeba abiria 250, magari 10 na ukubwa wa tani 10 kitaondoa kero ya muda mrefu waliyokuwa wakiipata wananchi wa Kayenze na Bezi.

"Wananchi wa Kisiwa cha Bezi na Kayenze Mwaloni wamekuwa na shida ya usafiri majini kwa muda mrefu, na mimi niliahidi kuwapatia kivuko wakati wa uchaguzi mwaka 2015 na ombi langu la kujenga kivuko hicho lilipokelewa vyema na serikali toka mwaka 2016 kwa ahadi ya kujenga kivuko hicho," alisema Mabula.

Mbunge huyo alisema, kuchelewa kukamilika mapema kivuko hicho, kulitokana na changamoto kadhaa na mojawapo ni kukwama kwa vifaa bandarini kulikosababishwa na msamaha wa ushuru ambapo hata hivyo, Mabula aliahidi kushughulikia suala hilo na kufafanua kuwa Oktoba mwaka 2019 kivuko hicho kitafanyiwa majaribio rasmi kabla ya kukabidhiwa mwezi mmoja baadaye kwa ajili ya kuanza kazi rasmi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kampuni inayotengeneza kivuko hicho ya Songoro Marine Ltd, Meja Songoro, alisema ujenzi wa kivuko hicho ulioanza Januari mwaka huu uko katika hatua za mwisho mwisho na kuwa sasa kampuni yake inakamilisha kufunga mifumo ya maji, umeme, zimamoto, kufunga ingini na vifaa vya kuendeshea kivuko hicho.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Rukia Muwango, akisalimiana na baadhi ya wanafunzi walioko katika kambi ya taaluma mjini Nachingwea juzi, wakijiandaa kwa ajili ya mtihani wa darasa la saba. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Sababu wanachama 83,667 CHF kushindwa kuhuisha uanachama

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANACHAMA 83,667 wa Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa mkoani Shinyanga, wametajwa kushindwa kuhuisha uanachama wao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo hali ya kiuchumi.

Kutokana na hali hiyo, wengi walikuwa wakilipiwa na mashirika na baada ya kuachana nao wakakosa fedha.

Hayo yalibainishwa juzi na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Rashidi Mfaume, kwenye uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha wananchi kujiunga na CHF iliyoboreshwa, ambayo iliyoandaliwa na wadau wa afya HPSS kwa ufadhili wa Serikali ya Uswisi.

Alisema kumekuwapo na changamoto kwa wanachama wengi wa CHF mkoani humo kushindwa kuhuisha uanachama wao hasa wale ambao walilipiwa fedha na mashirika, na mara baada ya mashirika hayo kuacha kuwalipia nao wakakosa fedha, na kusababisha kutokuwa tena wanachama wa CHF iliyoboreshwa.


"Mwitikio wa wananchi mkoani Shinyanga kujiunga na CHF iliyoboreshwa bado upo chini sana, kutokana na wengi wao kuwa na hali mbaya ya kiuchumi, na kuwa wategemezi wa kulipiwa bima hii na mashirika, na yakisitisha tu huduma na wao ndio unakuwa mwisho wao," alisema Dk. Mfaume.

"Mkakati uliopo ni maofisa uandikishaji kutembelea kaya zilizoshindwa kuhuisha uanachama wa CHF, na kuwahamasisha kulipa fedha ili waendelee kunufaika na matibabu kwa gharama nafuu, kuhakikisha dawa na vifaa tiba vinakuwapo muda wote kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, na kutenga madirisha ya CHF," aliongeza.

Naye mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa kampeni ya CHF iliyoboreshwa, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, alitoa wito kwa wananchi na wanachama ambao wameshindwa kuhuisha uanachama wao kuwa kwenye msimu huu wa mavuno ya zao la pamba, pale watakapouza watenge fedha za kulipia CHF.

Alisema kadi ya kujiunga na CHF iliyoboreshwa inakatwa kwa shilingi 30,000, na kuhudumia watu sita kwenye kaya moja ambapo watapata matibabu ndani ya mwaka mzima, kuanzia kwenye zahanati, vituo vya afya hadi kwenye hospitali ya mkoa.

Meneja Mradi wa HPSS mkoani Shinyanga, Dk. Harun Kasale, alisema wamezindua kampeni hiyo baada ya kuona kuwapo na mwitikio mdogo wa wananchi, ambapo kati ya kaya 261,608 za mkoa huo zilizojiunga na CHF ni 25,513 sawa na asilimia 9.8.



## HABARI ARUSHA

# Waagizwa kutoa mita 2 ujenzi wa mifereji ya maji

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imeagiza wananchi wa Kata ya Mateves, kutoa eneo la mita mbili za kila upande kwa ajili ya kujenga mifereji ya maji katika barabara ya lami, inayojengwa yenye urefu wa kilomita 6.5 inayokwenda kwenye kituo kikubwa cha kupoozea umeme katika Kijiji cha Lemgur, kilichopo kata hiyo wilayani Arumeru.

Agizo hilo limetolewa jana katika Kata ya Mateves na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, wakati akizindua ujenzi wa barabara hiyo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 9.3 na kuwataka wananchi hao kutambua serikali haijatoa fedha zozote za fidia kwa ajili ya ujenzi wa hiyo barabara.

Alisema wananchi wa maeneo ambako barabara hiyo inapita wanapaswa kutambua umuhimu wa barabara hiyo na kutoa kipaumbele kwa makandarasi ili kuhakikisha inakamilika bila kikwazo chochote.

"Barabara hii ikikamilika itawapunguzia gharama za kukodisha pikipiki toka mjini na maeneo mengine hadi kijijini kwenu, wakati wa mvua za masika zinaponyesha na kusababisha utelezi na kushindwa kupita magari," alisema.

Gambo alisema serikali imetoa kipaumbele kwa mkoa huo kupeleka miradi mikubwa ya maendeleo ikiwamo ya maji kwa kuwapatia zaidi ya Sh. bilioni 586 na sasa kujenga kituo kikubwa cha kupoozea umeme cha zaidi ya Sh. bilioni 116 kinachojengwa kijijini Lemgur katika Kata ya Mateves.

Alisema katika ujenzi wa kituo hicho, wananchi wa vijiji 22 toka maeneo mbalimbali nchini watanufaika na umeme wa kituo hicho, unakopita na kati ya hivyo Arusha vijiji tisa vitanufaiaka kikiwamo kinachojengwa.

"Umeme wa kituo hiki ni mkubwa wa kilovoti 400 ambao utatoka mkoani Singida kupitia Manyara na Arusha upande wa Tanzania hadi Isinya upande wa Kenya na laini yake itakuwa na urefu wa kilomita 510.7 na 414.7 zitakuwa upande wa Tanzania (Singida hadi Namanga na kilomita 96 zitakuwa Kenya - Namanga hadi Isinya).

Vile vile, alionya wananchi kuacha kujihusisha na migogoro katika mradi huo na makandarasi asilazimishwe kutoa ajira kwa vijana au mtu yeyote bila ridhaa yake mwenyewe.

"Tunapokuwa na umeme wa uhakika tunakuwa na uhakika wa Tanzania ya viwanda sababu umeme upo na haukatiki, hivyo kila mmoja atoe kipaumbele na ushirikiano wa mradi huu kuanzia barabara hadi ujenzi wa kituo hiki cha kupoozea umeme," alisema. Meneja wa Shirika la Umeme (Tanesco) Mkoa wa Arusha, Mhandisi Herin Mhina, alisema mradi huo wa kuunganisha umeme kati ya Kenya na Tanzania ni mkubwa wa kimkakati wa serikali ambao unahusisha ujenzi wa laini kubwa ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida kupitia Manyara hadi Arusha.

Alisema ujenzi wa laini, mradi utahusisha upanuzi wa vituo vya kupoozea umeme vya Dodoma na Singida na ujenzi wa kituo kipya cha kupoozea umeme chenye uwezo wa Kilovoti 400 kinachojengwa Arusha (Lemgur).



Mkazi wa Arusha akijiandikisha katika daftari la wapigakura kwa kutumia mashine ya BVR, Shule ya Msingi Levolosi, Mkoa wa Arusha jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Shule yakabidhiwa mradi wa maji mil. 200/-

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHULE ya Msingi Sekei katika Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, imekabidhiwa mradi wa maji wenye thamani ya Sh. milioni 200, uliojengwa kwa ufadhili wa Shirika lisilo la kiserikali la Walter Boy's kutoka nchini Marekani.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kukabidhi mradi huo, katika Shule ya Msingi Sekei, Mratibu wa Mradi wa Shirika la World Serve International Tanzania, Elyne Kingu, alisema, lengo la mradi huo, ni kutoa huduma ya maji kwa wanafunzi wa shule za msingi za Naurei, Sekei na shule mpya ya sekondari Kiutu, baada ya kupokea ombi kutoka kwa uongozi wa kijiji cha Naurei.

Alisema katika kipindi kifupi cha kukamilika kwa mradi huo, tayari matokeo chanya yameanza kuonekana, kutokana na mabadiliko ya usafi wa mazingira unaonekana wazi, pia kuwa na uhakika wa afya za wanafunzi, hususani watoto wa kike kujistiri wakati wa siku zao za hedhi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha DC, Dk. Wilson Mahera, alilishukuru shirika hilo kwa ujenzi wa mradi wa maji ambao utapunguza uhaba wa maji kwenye shule hiyo.

Mahera aliahidi kuusimamia vizuri mradi huo, ili uweze kujiendesha na kuwa endelevu pamoja na kuhudumia jamii inayoizunguka eneo hilo la shule.

Alisema mradi huo, ukisimamiwa vizuri utaongeza idadi ya watu, kupata maji kwa kuwa na uwezo wa kuzalisha lita 20,000 kwa siku kutoka kwenye chanzo hicho. Alieleza kuwa, kazi iliyofanywa na shirika hilo, inapaswa kuungwa mkono na inaendana na sera ya serikali ya kuhakikisha ifikapo mwaka 2020, asilimia 80 ya watu vijijini wanapata majisafi na salama, pamoja na utekelezaji wa uchumi wa viwanda kuelekea wa kati, ifikapo 2025.

Mkurugenzi wa Maji Shirika la 'Water Boys', Nicole Woods, alisema amefurahishwa kuona wanafunzi wanafurahia huduma ya maji na kuishukuru Serikali ya Tanzania kwa kukubali kufanyakazi na shirika hilo.

Alishauri mradi huo, utumike kwa lengo lililokusudiwa la kutoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi, pamoja na kuweka mipango imara ya kusimamia mradi huo ili uwe endelevu kwa maslahi ya vizazi vijavyo.

"Nilipokuja kwa mara ya kwanza hapa shuleni, hakukuwa na maji, watoto waliteseka, leo nimefurahi kukuta maji yanatoka na wanafunzi

wanafurahia huduma ya maji, ninaishukuru serikali kwa kukubali kufanyakazi na sisi, jambo la muhimu ni mradi huu kutunzwa na kutumika kwa malengo yaliyowekwa," alisema Nicole.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Sekei, Adam Sambo, alisema toka kukamilika kwa mradi huo, hali ya usafi wa mazingira ya shule hiyo, imebadilika tofauti na hapo awali na wanafunzi wamekuwa na furaha kutokana na kuwa na uhakika wa afya zao.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema, baada ya kupata mradi huo, wameotesha vitalu vya maua na mboga zitakazoatumika kwa ajili ya chakula cha walimu na wanafunzi, na kujifunza elimu ya kujitegemea.

"Awali tulipata shida ya kupata maji katika eneo letu la shule, tulishindwa kupata majisafi na salama kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi shuleni, hatukuwa na maji ya kunywa ya kupikia na hata ya kunawa mikono, baada ya kutoka chooni pia hali ya watoto wa kike kujisitiri wakati wa hedhi ilikuwa ni shida, lakini sasa huduma hii itasaidia wanafunzi wetu kuwa katika mazingira rafiki na salama," alisema Sambo.

Alisema fedha za mradi huo, zimetumika katika shughuli za uchimbaji wa visima vitatu na viwili vilifanikiwa kupata maji, tangi la lita 60,000 na pampu zinazotumia umeme wa jua, pamoja na vituo vinane vya kuchota maji.

# Wanafunzi wahimizwa kujiandaa vyuo vikuu

**Na Woinde Shizza,**
ARUSHA

WANAFUNZI wa sekondari nchini, wametakiwa kujiandaa vema katika masomo ya vyuo vikuu, watakavyochaguliwa kujiunga, ili wawe na uelewa wa masomo watakayochukua.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alitoa rai hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alipokuwa kwenye ufunguzi wa maonyesho ya Chuo cha Uhasibu kwa wanafunzi wa shule za sekondari 18 za Wilaya ya Arusha iliyofanyika jijini Arusha.

Mwaisumbe alisema kujiandaa mapema kunasaidia wanafunzi hao kuzoea mazingira ya masomo ya elimu ya juu, kwa kuwa wakifanikiwa wanapata uzoefu wa fani mbalimbali zinazotolewa na vyuo hivyo.

Alihimiza Chuo cha Uhasibu kuendeleza maonyesho hayo kwa lengo la kuwaandaa vijana kufikia ndoto zao za kitaaluma na wasiishie kwenye Wilaya ya Arusha pekee, bali waende mbali zaidi.

Awali Mkuu wa Chuo cha Uhasibu, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema maonyesho hayo yana lengo kubwa la kuwapa nafasi vijana, waliopo sekondari kidato cha nne na sita, kwa ajili ya kujiandaa kuchukua kozi anayopenda itakayomsaidia kufikia ndoto zake.

Alisema maonyesho hayo yatawasaidia wanafunzi hao, kukutana na wataalamu na wakufunzi wa chuo hicho, pamoja na wanafunzi kujionea taaluma mbalimbali zinazotolewa na chuo hicho na kuamua katika elimu yao.

Prof. Sedoyeka alisema, mwisho wa maonyesho hayo, wanatarajia kupata wanafunzi wengi watakaopenda kujiunga na mafunzo chuoni hapo kama lilivyo lengo la chuo hicho na uwapo wake unategemea wanafunzi kujiendesha.

Maonyesho hayo pia yamelenga namna ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo, kwa lengo la kuwasaidia vijana kujiajiri na kutotegemea kuajiriwa, jambo litakalosaidia azima ya serikali ya uchumi wa kati wa viwanda.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, wakati akiwasili katika uwanja wa KIA, kwa ziara ya kikazi ya siku nne mkoani Kilimanjaro. **PICHA: OWM**

# Wauguzi wadaiwa kushiriki ukeketaji

**Na Mary Mosha, SIHA**

WADAU na watetezi wa haki za wanawake wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wameomba serikali kuangalia na kudhibiti mila na desturi zinazowakandamiza wanawake na watoto hasa ukeketaji.

Lengo la kufuatilia mienendo hiyo ikiwa kupunguza madhara ya kupoteza damu nyingi kwa wanawake hasa wakati wa kujifungua, yanayotokana na kuchanika kwa kovu lililotokana na kukeketwa.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti baadhi ya kinamama hao walisema, matatizo ya ukeketaji kwa wilaya ya Siha bado ni kitendawili kisichoteguka kwa vile wanajamii hao kuwakeketa watoto wadogo.

Evaline Moleli, kutoka kata ya Karansi, alisema wapo baadhi ya wauguzi katika hospitali za mkoani Kilimanjaro ambao wamekuwa wakipewa fedha ili kuwakeketa watoto wenye umri chini ya miaka mitatu.

Alisema hali hiyo inasababisha matatizo makubwa hasa ya kupoteza damu nyingi na pia wakati wa kijifungua wanawake wenye makovu hutoka damu nyingi na hata wengine kupoteza maisha.

Safina Mohamed, mmoja wa wananchi, alisema miongoni mwa mila na desturi zinazowaadhiri na kuathiri mwanamke katika baadhi ya makabila ni ukeketaji ambao umekuwa ukifanyika kwa njia za siri katika vituo vya afya na zahanati.

"Tunaiomba serikali ya asasi na kiraia kuungana katika kuelimisha hasa jamii za wafugaji na kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kufanya vitendo kama hivyo," alisema Safina.

Msele Emanuel, alisema bado elimu ni ndogo kwa wanajamii juu ya masuala ya ukeketaji na madhara yake ili kuepukana na matatizo kwa vizazi vijavyo.

Mratibu wa Mtandao wa mashirika yanayopinga ukeketaji (Nafgem) Tanzania, France Selasini, alikiri kuwapo kwa ukeketaji katika Wilaya ya Siha, hasa katika kata za Naibili, Karansi, Lekrumuni, Orkolili, Ngarinairobi na Donyomoro na kusema kuwa unaofanywa kwa siri mkubwa na wanafanyiwa watoto wadogo ambao hawawezi kujieleza.

"Katika Wilaya ya Siha tatizo hili bado ni kubwa ambalo serikali inapaswa kuliangalia kwa umakini katika kuhakikisha wanaweka sheria kali zitakazowabana wahusika watakaobainika kuingia kwenye makosa mbalimbali yakiwamo ya ukatili kwa kinamama na watoto," alisema Selasini na kuongeza kuwa;

"Tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha mpango maalumu wa kuielimisha jamiii juu ya ukeketaji na kuanzisha mpango maalumu wa kutoa elimu kila mara ili kuhakikisha wanakubali kubadilika... pia adhabu kali zitolewe juu ya wote watakaobainika kutenda vitendo hivyo,"

# 'Elimu itolewe zaidi kuikabili tezi dume'

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wakazi wa mkoani Kilimanjaro wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwa na utoaji elimu endelevu kuhusu saratani ya tezi dume, ili kuhakikisha wanaume wanajitokeza kwa wingi katika kupima afya zao.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, Sebastiani Msofe, alisema bado wananchi hawana elimu ya kutosha juu ya saratani ya tezi dume hali inayowafanya kuchelewa kufika kwenye matibabu jambo ambalo hupelekea kupoteza maisha.

Alisema bado katika jamii kuna imani potofu juu ya tezi dume hali ambayo serikali ikiingilia kati katika kutoa elimu katika kila mikutano ya vijiji, kata na viongozi wa dini watumie mimbari zao vyema elimu itaweza kufika kwa wakati.

"Tunaiomba serikali kutoa agizo kwa wataalamu kuanzia ngazi za vijiji kufika kwa kila mkutano wa kijiji, kata, wilaya na hata mkoa kutoa elimu ya afya ya kuzungumzia magonjwa ya saratani hasa tezi dume ili kuleta afueni kwa wanaume," alisema Rafael Elisante na kuongeza:

"Ikiwa viongozi wa vijiji, tarafa, kata wilaya na mkoa watapewa agizo la kuhakikisha wanaweka wanafikiwa na agenda ya afya katika mikutano ambayo halmashauri itatuma mtaalamu wa afya kufika na kuelezea magonjwa ya saratani, itasaidia kubadilisha maisha ya Watanzania na kupata taifa la watu wenye afya bora ambapo wataweza kuleta maendeleo," alisema Elisante. Grace Lucas ni mwananchi wa Wilaya ya Siha akizungumzia saratani hiyo, alisema katika baadhi ya makabila wamekuwa wakiogopa kwenda kupima na hata wakigundulika kuwa na saratani hiyo wamekuwa wakikaidi kutumia dawa.

Hali hiyo ambayo imekuwa chanzo cha vifo vya mara kwa mara kwa wanaume, inaweza kudhibitiwa iwapo kutakuwa na programu ya elimu endelevu.

Kwa upande wake daktari bingwa wa magonjwa ya saratani ya tezi dume katika Hospitali ya Rufani ya KCMC, Nicholous Ngowi, alisema bado mwamko ni mdogo kwa jamii hivyo ikiwa serikali italichukulia hilo kama agenda kuu katika mikutano yake litaweza kuisaidia jamii.

Alisema watu wanaopata ugonjwa huo mara nyingi ni kinababa wenye umri kuanzia miaka 40 ikiwa katika familia ya kuna ugonjwa huo na 50 ikiwa kwenye ukoo huo hakuna historia ya ugonjwa huo.

"Ni kweli kuwa mwamko bado ni mdogo, wananchi hawana elimu ya kutosha, lakini kwa kushirikiana na serikali na mashirika binafsi tutaweza kuwasaidia wanaume wengi na kuokoa maisha yao kwani saratani yoyote ikiwahiwa inatibika," alisema Dk. Ngowi.

# Kamati ulinzi ndiyo dawa kudhibiti uhalifu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KUANZISHWA kamati za ulinzi na usalama zitakazofanya doria katika maeneo mbalimbali ya Kata ya Shirimatunda iliyoko Moshi Mjini kutasaidia kupunguza na kukomesha vitendo vya wizi vinavyoshamiri.

Hayo yalibainishwa jana na Diwani wa Kata ya Shirimatunda, Francis Shio, katika mkutano wa maendeleo na wananchi wa kata hiyo.

Shio alisema, suala la wizi katika Kata ya Shirimatunda limezidi kushamiri kutokana na hali ya uchumi kubadilika ambapo watu wanarahisisha maisha kwa kujipatia kipato kwa njia ya wizi jambo ambalo limesababisha kutoweka kwa hali ya usalama.

"Hali ya uchumi kwa sasa imebadilika, na mfumo wa maisha ni lazima ubadilike. Watu wanajitafutia kipato kwa njia za wizi. Ni lazima wananchi mjitoe kuanzisha kamati za usalama ili kukomesha wimbi la wizi linaloimaliza kata yetu," alisema Shio.

Aidha, diwani aliwataka wananchi kutojenga katika hifadhi za barabara ili kuepuka usumbufu na hasara ya kubomoa majengo hayo wakati wa kupisha ujenzi wa miundombinu ya barabara na huduma nyingine za kijamii.

Mkaguzi wa Polisi David Gabriel, kutoka Kanda ya Moshi Magharibi, aliwataka wananchi kuacha itikadi za vyama na dini na kuwahimiza kuwa pamoja katika kuhakikisha usalama unapatikana katika maeneo yao.

Alisema suala la ulinzi ni nyeti kwani kusipokuwa na usalama katika jamii husika wananchi watashindwa kujihusisha na shughuli za kimaendeleo.

Kwa upande wake Joseph Mushi, ambaye ni mwananchi wa kata hiyo alisema wizi umekithiri katika kata hiyo na kusema kuwa ikiwa watapewa mwongozo sahihi wa namna ya kuanzisha kamati hizo za ulinzi na usalama zinaweza kutokomeza matukio ya uhalifu.



Ukurasa 18

## Uwekezaji wa kilimo, ufugaji unavyoiweka dunia hatarini



Ukurasa 14

## MAJERUHI BODABODA

# BUFE

Ijumaa Julai 19, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Uchumi China waporomoka baada ya miaka 27

Ukurasa 15



# TARI Ilonga kumaliza shida ya mafuta nchini

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TANZANIA imekuwa ikiagiza wastani wa tani 400,000, za mafuta ya kula kila mwaka kutoka nje ya nchi . Hali hiyo ni kutokana na kuwepo kwa uzalishaji mdogo wa mbegu za mafuta unaotokana na sababu mbalimbali zikiwamo mazao yanayokamuliwa mafuta kutolimwa kwa wingi.

Kwa mujibu wa takwimu ya Wizara ya Viwanda na Biashara, inakadiriwa kuwa mahitaji ya mafuta kitaifa ni tani 500,000, huku uzalishaji pia ukikadiriwa kuwa tani 180,000 .

Kiwango hicho cha mafuta kinatokana na zao la alizeti, michikichi, ufuta na mazao mengine ya mbegu yanayozalishwa nchini.

Kati ya tani hizo zinazozalishwa hapa nchini asilimia 50 husindikwa katika viwanda vikubwa vilivyopo Mwanza, Dar es Salaam na Singida wakati asilimia 50 nyingine husindikwa katika viwanda vidogo vidogo vilivyopo katika mikoa inayozalisha mazao hayo.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Ulaya ni ukurasa mpya, Ugiriki ikibadili serikali

Ukurasa 20

UCHUMI

# MAJERUHI BODABODA

• Gharama za matibabu mzigo usiobebeka • Hutibiwa kwa sera y
msamaha • Bingwa asema hufikia hata milioni 3/=




Majeruhi wakipatiwa msaada baada ya ajali ya boda boda. **PICHA: MTANDAO**

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

USAFIRI wa pikipiki nchini licha ya kurahisisha safari na kutoa ajira kwa vijana umeendelea kuwa changamoto.

Hiki ni chanzo cha vifo na majeruhi na huchangia kuwapo umaskini na uharibifu wa mali kwenye jamii mbalimbali kwa kuwa zinahusika sana na ajali za barabarani.

Kwa mujibu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, kwa mwaka 2017 kulikuwa na ajali za pikipiki 1,459 ambazo zilisababisha vifo 728 na majeruhi 1,090.

Aidha, kwa mwaka 2018 ajali za pikipiki zilipungua ambapo zilikuwa ajali 876 na kusababisha vifo vya watu 366 na majeruhi 994.

**MZIGO WA TIBA**

Waziri ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema mzigo mkubwa wa matibabu ya majeruhi wa ajali hizo umekuwa ni mzito kwa serikali kwa kuwa wanatibiwa kupitia Sera ya Afya ya mwaka 2007 ambayo inatoa msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo.

> **"Matibabu kwa wanaovunjika miguu, mikono na majeraha vichwani ni kati ya Sh.500,000 hadi 3,000, 000 na hutegemea na kiwango cha mvunjiko.**



Majeruhi wa boda-boda baada ya ajali. **PICHA: MTANDAO**

Majeruhi wa ajali hizo ambaye amelazwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, Petro Sang'a, anasema matibabu ya mivunjiko wa mifupa inayotokana na ajali ni changamoto hasa kwa watu wenye vipato vya chini.


Anasema matibabu ya mguu wake hadi sasa yamegharimu zaidi ya Sh. milioni 1.2 ambazo amechangiwa na ndugu na jamaa zake.

"Kutokana na gharama za matibabu kuwa kubwa ndugu na jamaa wamekuwa wakinichangia, na pia nimelazimika kukata Bima ya Afya ya Jamii ili-

A

a





yoboreshwa (CHF) ya Sh. 30,000 ambayo inanisaidia kwa matibabu madogo madogo," anasema dereva huyo wa boda boda.

Sang'a alipata ajali mwezi Aprili mwaka huu ambapo mguu wake ulivunjika mara mbili, jambo lililosababisha kushindwa kufanya shughuli zake licha ya familia kumtegemea.

Akizungumza na Nipashe, anabainisha kuwa kwa takriban miezi mitatu yupo kitandani bado akiuguza majeraha hali ambayo imemrudisha nyuma kimaendeleo.

"Gharama nilizotumia na kuchangiwa na ndugu ningeweza kufanya mradi mwingine mdogo ambao familia ingekuwa ikipata kipato kama ningekuwa na bima kubwa ya afya yenye uwezo wa kubeba matibabu yote, kuna umuhimu kama serikali ikitunzishia bima ya afya ya aina hii,"anasema

Majeruhi mwingine Adri Sahagagili, anasema amepata ajali ya pikipiki ambayo imesababisha mguu kuvunjika mara tatu hadi sasa matibabu yamekula zaidi ya Sh.milioni 2.1 kutibu mguu wake.

"Ajali yangu nilipata mwezi Aprili, mwaka huu. Mimi nilikuwa naendesha pikipiki lakini taa zilikuwa si nzima sikuweza kuliona gari lililokuwa limeharibika katikati ya barabara hivyo nikaligonga na kunisababishia kuvujika mguu," anasema.

#### MAONI YA DAKTARI

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma ambaye pia ni Daktari Bingwa wa Upasuaji, Ajali na Mifupa, Dk. Ernest Ibenzi, akizungumzia gharama anasema.

"Matibabu kwa wanaovunjika miguu, mikono na majeraha vichwani ni kati ya Sh.500,000 hadi 3,000, 000 na hutegemea na kiwango cha mvunjiko."

Anasema kwa wasio na uwezo wa kumudu gharama hizo hutibiwa kwa utaratibu wa msamaha ambapo serikali hurejesha gharama zao kwenye hospitali husika.

"Serikali hutoa msamaha wa muda lakini huku mgonjwa akiendelea kutibiwa, huu msamaha si bure serikali hurejesha fedha hizi kwa kuzirudisha kwenye hospitali, anasema gharama hizo ni pamoja na vyuma wanavyowekewa waliovunjika miguu ambapo kwa mfupa wa paja chuma chake kinagharimu Sh. milioni 1.5."

Dk.Ibenzi anasema kwa wale wanaotakiwa kubadilishiwa nyonga gharama yake hufikia kiasi cha Sh. milioni 2,000,000 hadi 3,000,000.

"Hawa majeruhi ambao mivunjiko sio mikubwa wanakaa hospitali kwa siku saba, lakini wale ambao wamevunjika sana wanakaa hadi miezi sita hospitali, mwenye shida ya kichwa anatibiwa hadi apate fahamu, kwa hiyo unaona ajali hizi zinasababisha kushindwa kuendelea na shughuli zao za kiuchumi," anasema.

Vile vile, mtaalam huyo anasema bei halisi ya miguu bandia ni kati ya Sh.milioni 1.5 hadi 3,000,000.

#### MAJERUHI 50

Mtaalamu bingwa huyo anasema kwa siku hospitali hiyo inapokea majeruhi wa ajali ikiwemo za pikipiki 50 ambapo kati yao zaidi ya 30 hulazwa.

Mganga huyo anasema kila siku wanafanya upasuaji kwa majeruhi 12 hadi 17 wa ajali za barabarani.

Dk.Ibenzi anasema ni vyema madereva kuchukua tahadhari na kufuata sheria ya usalama wa barabarani kwa kuwa madhara ya mwendokasi ni makubwa kwenye afya zao.

"Kama huo mpango ambao Wizara ya Afya inatarajia kuuleta wa bima kwa watu wote utakuwa suluhisho kwenye gharama za matibabu ya ajali na pia magonjwa yasiyo ya kuambukiza yana gharama kubwa pia, ni vyema mpango huu ukianza watu wakate bima za afya,"anasema.

#### BIMA YA AFYA

Waziri ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Ummy Mwalimu, anasema tangu usafiri wa bodaboda kuruhusiwa kubeba abiria mwaka 2010 serikali imekuwa ikiingia gharama kubwa kutibu wagonjwa wa ajali huku asilimia kubwa wakitibiwa kwa fedha za umma.

"Nipo kwenye mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Ndani, tunataka kupeleka muswada bungeni ambao utalazimisha kila anayeendesha bodaboda moja ya masharti lazima uwe na bima ya afya hii itaweza kusaidia wengi kuepuka ulemavu unaoweza kuzuilika na kupunguza mzigo wa serikali," anasema.

#### SHIRIKA LA AFYA

Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Afya Duniani(WHO), iliyotolewa mwaka 2018, inaonyesha kila mwaka takriban watu milioni 1.35 hufariki dunia kwa sababu ya ajali ya barabarani.

Kati ya watu zaidi ya milioni 20 na 50 wanapata majeruhi yasiyo ya mauti, na wengi wanapata ulemavu kutokana na majeraha yao.

Ripoti inasema majeraha ya ajali za barabarani husababisha hasara kubwa za kiuchumi kwa watu binafsi, familia zao, na mataifa kwa ujumla.

Hasara hizi zinatokana na gharama ya matibabu pamoja na upotevu wa mali kwa wale waliofariki au walemavu na majeruhi yao huku nchi nyingi zikigharamika kutokana na ajali hizo kwenye ukuaji wa pato la taifa(GDP) kwa asilimia tatu.

# Uchumi China waporomoka kwa kasi baada ya miaka 27



Ukanda wa viwanda wa Umoja wa Ulaya na China. **PICHA: MTANDAO**

KWA mara ya kwanza katika miaka 27 iliyopita, uchumi wa China umepungua kasi ya ukuaji wake katika robo ya pili ya mwaka.

Kuanzia mwezi Mei mpaka Juni mwaka huu, uchumi wa taifa hilo kubwa duniani ulikuwa kwa asilimia 6.2 ikilinganishwa na mwaka mmoja uliopita.

Matokeo hayo yanalingana na vile ilivyotarajiwa. Serikali ya China inajitahidi kuchochea ukuaji wa uchumi kwa mwaka huu kwa kupunguza kodi pamoja na kubana matumizi.

China pia ipo katikati ya vita vya kibiashara baina yake na Marekani ambavyo vimeumiza hali ya biashara na ukuaji wa uchumi.

Data rasmi zilizotolewa na Ofisi ya Takwimu ya China zinaonyesha kuwa kasi ya ukuaji imeshuka kutoka asilimia 6.4 ya mwanzoni mwa mwaka.

Rais wa Marekani Donald Trump, aliandika kupitia ukurasa wake wa twitter kuwa ushuru wa kibiashara kutoka Marekani "umeathiri pakubwa" uchumi wa China.

Mamlaka za China zinasema takwimu hizo zinaonyesha hali ngumu ya kimazingira ndani na nje ya nchi.

"Uchumi umekuwa katika ustawi wa kutegemewa katika nusu ya kwanza ya 2019, lakini kuna nguvu kubwa ya kwenda chini kadri siku zinavyosonga," inaeleza Ofisi ya Takwimu ya nchi hiyo.

#### UCHAMBUZI

Andrew Walker, mwandishi wa biashara, anasema takwimu hizi zinaonyesha kwa namna gani jinsi ugomvi wa kibiashara baina ya China na Marekani ulivyokuwa na athari. Ukuaji umeshuka kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na hali ambayo ingekuwapo kama kusingekuwa na ugomvi baina ya mataifa hayo.

Picha ya muda mrefu ni kuwa, uchumi wa China utaendelea kuwa imara japo utashuka kasi yake.

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa China katika miongo mitatu iliyopita mpaka kufikia mwaka 2010 ilikuwa ni asilimia 10. Lakini ilikuwa ni jambo la wazi miongoni mwa wachumi na hata baadhi ya viongozi waliozungumza nchini China walisema kuwa ukuaji huo usingelibaki hivyo milele.

Lengo lilikuwa ni kuhakikisha uchumi hautegemei zaidi uwekezaji na biashara ya nje badala yake kukuza vipato na matumizi ya raia. Hatua, imepigwa katika eneo hilo, japo uwekezaji bado unachangia pakubwa uchumi wa Uchina.

Kuna hatari zake hata hivyo, la zaidi ni madeni makubwa ya kampuni. Mamlaka zilichochea kampuni kukopa kwa kasi baada ya uchumi wa dunia kuyumba. Hiyo ilichangia pakubwa kuzuia anguko la ghafla la uchumi lakini ikaongeza hatari ya kifedha kwenye madeni.

#### ATHARI DUNIANI

Ukuaji wa uchumi ukiyumba nchini China unazalisha hofu kwengineko na mfumo mzima wa kidunia.

Edward Moya, mtaalamu wa uchumi kutoka taasisi Oanda, anasema takwimu hizo za kiuchumi "zinaonyesha kuwa kuyumba kwa ukuaji wa uchumi wa China ni suala endelevu na masoko yategemee fedha zaidi za mikopo kutoka Benki Kuu ya China ili kuchochea ukuaji wa uchumi."

Mgogoro wa kiuchumi baina ya China na Marekani pia ni suala lengine la kuliangalia na athari zake zipo wazi sasa.

"Vita ya kibiashara ina athari kubwa sana kwenye uchumi wa China, na hakuna suluhu yeyote inayotarajiwa basi tutarajie kuona uchumi ukishuka zaidi," anasema.

Japo pande zote mbili zilikubaliana kurudi kwenye meza ya mazungumzo walipokutana katika mkutano wa G20 nchini Japani, wametwangana ushuru katika bidhaa mbalimbali na kuumiza uchumi wa dunia.

#### AFRIKA IKOJE?

Afrika ni bara ambalo linategemea pakubwa biashara na Uchina.

Ni nchi moja tu ambayo haina ushirikiano wa kibiashara na China ambayo ni eSwatini au zamani Ufalme wa Swaziland.

China ndiyo taifa lenye ushawishi mkubwa kibiashara Afrika baada ya kuipiku Marekani zaidi ya miaka 10 iliyopita.

Kwa ujumla thamani ya biashara baina ya China na Afrika kwa mwaka 2017 ilifikia kiasi cha Dola bilioni 170 kutoka Dola bilioni 10 mwaka 2000.

Ni dhahiri kuwa iwapo hali ya kusuasua kwa uchumi nchini China itaendelea basi Afrika nayo itaathirika pakubwa. **BBC**

BIASHARA

# TARI Ilonga kumaliza shida ya mafuta

## • Yalenga kuzalisha tani 500,000 za ufuta kuondoa tatizo



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa kilimo Tanzania (TARI), Dk Geofrey Mkamilo, kushoto (anayenyoosha mikono), akizungumza kuhusu pilipili hoho kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, mbele (wa pili kulia), wakati alipotembelea vipando vya mazao vilivyopo katika kituo cha TARI Ilonga. **PICHA ZOTE: ASHTON BALAIGWA.**

**INATOKA UK.13**

Kutokana na uzalishaji mdogo wa mafuta hapa nchini Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania(TARI) Ilonga, iliyopo wilayani Kilosa mkoa wa Morogoro ,imeamua kuvaa njuga kwa kuhakikisha inaisaidia kupunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje na badala yake kuongeza kasi ya uzalishaji wa ndani.

Mtafiti wa Ilonga akizungumzia mkakati wa uzalishaji wa zao la alizeti, ili kupunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi, mtalaamu Frank Reuben, anasema wameanza kuongeza uzalishaji wa mbegu za alizeti zilizothibitishwa ubora ili wakulima nchini waweze kuzalisha kwa kiwango kikubwa cha mafuta ya kula .

Anasema kuwa kupitia mkakati huo watafiti wa TARI Ilonga, wamepewa jukumu la kuzalisha mbegu hizo za alizeti ikiwemo ya sasa ya rekodi iliyoboreshwa na kutumiwa na wakulima kuzalisha mafuta na kuongeza uzalishaji huku wakiendelea kufanya utafiti wa mbegu nyingine ili kuweza kuingizwa sokoni .

Mtafiti huyo wa alizeti nchini anasema kuwa tayari katika kipindi cha mwaka 2019 wameshazalisha mbegu mama ya alizeti aina hiyo ya rekodi tani 37.8 ambazo zimeanza kusambazwa kwa wakulima katika mikoa inayolima zao la alizeti .

Anasema kupitia uzalishaji wa mbegu hizo jumla ya hekari 18,500,zitapandwa zao hilo la alizeti katika mikoa mbalimbali ambayo kwa sasa imekuwa ikizalisha zao hilo ili kuweza kuchangia kuongezeka kwa uzalishaji kiwango cha mafuta nchini katika mikoa iliyokewa mkakati huo ikiwemo Singida,Dodoma na Morogoro.

> **“Kwa sasa wana miradi 11 iliyopo katika mikoa 15 na kwamba miradi mitatu inahusisha zao la mahindi katika mikoa nane ili kuongeza thamani ya nafaka.**



Mtafiti wa mbegu za alizeti nchini,Frank Reuben wa TARI, Ilonga (katikati mwenye kofia), akitoa maelezo ya mbegu mama ya alizeti inayoonekana kwa nyuma . Reuben anazungumza na watalaam wa ugani kutoka kata mbalimbali za Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro.

Reuben anasema kuwa mbegu hiyo ya rekodi ambayo imesafishwa na kuboreshwa kutoka iliyokuwa mbegu ya zamani imesambazwa kwa wakulima na uzalishaji wake umeonyesha mafanikio makubwa ambapo hekari moja inatoa kilo zisizopungua kati ya 600 mpaka 800.

Mtafiti huyo wa alizeti anasema kuwa kwa sasa mbegu ya alizeti ya rekodi ndiyo inachukua asilimia 85 katika soko na ndiyo inayochangia asilimia 90 ya uzalishaji wa alizeti nchini na kuchangia asilimia 70 ya mafuta yanayozalishwa hapa nchini.

Akizungumzia kuhusu takwimu za uzalishaji wa zao la alizeti nchini anasema kuwa umekuwa ukiongezeka ambapo mwaka 2012/16 uzalishaji ulikuwa tani 500,000 wakati mwaka 2017/18 zilifikia tani 768,188 na mwaka 2018/19 tani 820,905 zilizalishwa na kwamba mkakati wa 2020/22 ni kuzalisha tani 500,000 ambazo zitazalisha mafuta ya alizeti tani 600,000 na hivyo kumaliza tatizo la upungufu wa mafuta nchini.

Anasema kuwa ili kufanikisha mkakati huo wa uzalishaji wa mafuta ya alizeti kufikia tani 600,000 ifikapo mwaka 2020/22 na kuondokana na changamoto ya mafuta TARI Ilonga imejipanga kutoa utafiti mwingine wa mbegu za alizeti itakayokuwa na ubora kuliko mbegu yoyote iliyoko sokoni kwa sasa ili kuongeza uzalishaji maradufu.

"Sisi watafiti hivi sasa tunaendelea kuumiza vicha kwa ajili ya mbegu nyingine nne za alizeti zitakazokuwa na uzalishaji mkubwa pengine zozote zilizopo sokoni. Tunataka kuongeza kasi ya uzalishaji wa mafuta wa ndani ili kuondokana na kutumia fedha nyingi kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi," anaeleza Reuben.

### WAKULIMA WAELEZA

Mmoja wa wakulima wa alizeti na mzalishaji wa mafuta Khalifan Hamadi, kutoka kata ya Magomeni wilayani Kilosa, anasema mbegu ya alizeti ya rekodi iliyofanyiwa utafiti na kuboreshwa na TARI Ilonga imeleta mafanikio makubwa katika uzalishaji wa zao hilo na hivyo kuwaongezea mapato yanayotokana kuuza kwa wanaokamua mafuta ya kula.

Anasema kuwa mbegu ya alizeti ya rekodi imeweza kuwasaidia kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti mara nne zaidi ya uzalishaji wa awali ambapo kabla ya matumizi ya mbegu hiyo walikuwa wakipata gunia saba kwa hekali moja.

Anasema sasa wameona umuhimu wa kuwepo kwa taasisi hiyo ya utafiti wa kilimo licha ya kuzalishiwa mbegu mbalimbali lakini pia wamekuwa wakisaidiwa kupata ushauri na utalaam wa kilimo bora cha alizeti tofauti na awali walikokuwa wakipanda kwa mazoea , bila kutumia mbegu bora na hivyo kukosa mavuno ya kutosha.

Aidha, mkulima Lethisia Semwenda ,ambaye pia hulima mahindi na mpunga kwa mda mrefu anasema sasa ameanza kushawishika baada ya kuona mavuno ya alizeti yameongezeka kwa wakulima wenzake hivyo katika msimu ujao anakusudia kuanza kulima kilimo hicho kwakuwa kimeonyesha kina faida kiuchumi baada ya kuuza au kukamua mafuta.

### KUSAIDIA WAKULIMA

Taasisi ya kuendeleza mifumo ya kimasoko katika kilimo iliyo chini ya Serikali ya Dernmak, Ireland na Sweden kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania imeamua kuwasaidia wakulima wadogo ,vijana na wanawake ili kuongeza fulsa katika mnyororo wa thamani wa mazao matatu kufanya kilimo biashara na chenye tija.

Meneja usimamizi, maarifa na mawasiliano wa taasisi hiyo, Al-Aman Mutarubukwa,anasema kupitia mradi huo, wamelenga kuyasaidia makundi hayo kwenye mazao ya alizeti,mahindi,maharage na mbaazi ili waongeze mnyororo wa thamani kuanzia uzalishaji, usindikaji na masoko ndani na nje ya nchi.

Anasema kwa sasa wana miradi 11 iliyopo katika mikoa 15 na kwamba miradi mitatu inahusisha zao la mahindi katika mikoa nane ili kuongeza thamani ya nafaka.

Mutarubukwa anasema kwa zao la alizeti,mbaazi na maharage miradi hiyo ipo katika mikoa ya kusini ikihusisha Mtwara na Lindi, Manyara, Mbeya, Njombe, Iringa, Dodoma na Singida na tayari makundi hayo yamenza kunufaika.

Anasema kupitia mpango huo wamelenga kubadilisha mifumo ya usambazaji na mifumo bora ya mbegu bora ya alizeti ambapo kwa miaka mitatu iliyopita hakukuwa na mbegu bora sokoni na taasisi hiyo kwa kushirikiana na kampuni ya uzalishaji mbegu ya alizeti ya ndani na nje wameingiza mbegu chotara zilizoboreshwa na kuwasambazia wakulima ambao wameongeza uzalishaji ili kupata tija.

“ Kwa miaka miwili iliyopita wakulima walikuwa wakitumia mbegu zilizozoeleka na kutoa mavuno kidogo wastani wa magunia matatu kwa hekari lakini baada kuleta mbegu za chotara mavuno yameongezeka yamefikia wastani wa gunia 15-18,"anasema Mutarubukwa.

Mutarubukwa, anataja ushirikiano kuwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti ya TARI, wameboresha mbegu yarekodi ya alizeti na kuweza kuongeza uzalishaji kwajili ya kukidhi mahitaji ya viwanda vya kutengeneza mafuta ya kula.

### MKURUGENZI MKUU

Mkurugenzi TARI Dk Geofrey Mkamilo, anasema kuwa kabla ya kuanzishwa kwake Ilonga kilikuwa kituo cha Utafiti na kiliweza kuzalisha mbegu za alizeti wastani wa tani 2.3 ambazo zilikuwa zikitumika kwajili ya mashamba yake lakini kwa mwaka wa kwanza baada ya kuundwa kwa taasisi hiyo uzalishaji wa mbegu umeongezeka na kufikia tani 7.5.

Dokta Mkamilo, anasema mkakati wa TARI ni kuwa ifikapo mwaka 2020 /22 wazalishe mbegu za alizeti tani 1.5 ambazo zitakuwa na uwezo wa kutoa mafuta wa kutoa mafuta ya kula ya alizeti tani 600,000 na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa wa uagizaji wa mafuta kula kutoka nje ya nchi.

Mkurugenzi huyo Mkuu wa TARI anasema mabadiliko hayo makubwa yaliyofanywa inatokana na kuongezewa majukumu ya kuzalisha mbegu kwa wingi wa mazao mbalimbali ili kuwauzia wakulima waweze kuzalisha mazao yatakayotumika kama malighafi ili kusaidia juhudi za serikali katika kujenga uchumi wa viwanda hapa nchini.

Anasema kuwa kupitia mpango huo, TARI imelenga kuwabadilisha wakulima kutoka kilimo cha kujikimu na kwenda katika kilimo biashara ili kuongeza uzalishaji kwa taifa na hivyo kuwepo kwa uhakika na usalama wa chakula.

Mkamilo,anasema kuwa watalaam wa utafiti kutoka taasisi 18 nchini wamewekewa mkakati maalumu wa kuhakikisha wanazalisha teknolojia za mbegu bora za kisasa na zenye ukinzani na magonjwa kwa mazao ya kimkakati likiwemo zao la alizeti linalozalishwa Ilonga kwa ajili ya kutatua changamoto ya upungufu wa mafuta nchini.

Anasema chini ya mkakati huo wa miaka mitano teknolojia za mbegu za kisasa zitakazozalishwa ambazo zitakuwa na ukinzani na magonjwa zitasambazwa na kumfikia mkulima kwa muda mfupi na kuuziwa kwa bei ya chini ili kuwasaidia kutumia teknolojia hizo kuongeza uzalishaji.

### KUSAMBAZA MBEGU

Mkurugenzi wa TARI Ilonga, Dk Joel Meriyo, anasema kuwa wameanza kwa vitendo mkakati wa kusambaza kwa wakulima

**INAENDELEA UK.20**

# Biashara katika picha



Wachuuzi wa mishikaki wakifanya shughuli zao barabarani katika Mtaa wa Nyamwezi, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**



Mchuuzi wa ndizi akisubiri wateja pembeni ya Barabara ya Morogoro, eneo Manzese, jijini Dar es Salaam jana, licha ya kuwepo changamoto ya jua kali. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Kijana akiwa amebeba stuli akisaka wateja ili ajipatie kipato, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

BIASHARA



# Uwekezaji wa kilimo, ufugaji unavyoiweka dunia hatarini



Kilimo kinachohitaji maji kwa wingi na ekari nyingi za ardhi ni changamoto kwa dunia ya sasa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

KILIMO na ufugaji ndiyo namna kuu ya kupata chakula na nchi kujitosheleza kwa chakula. Sekta hizo ndizo mwanzo wa kazi za uzalishaji viwandani na ufunguo wa uchumi hasa ule usio na teknolojia za kisasa pengine katika mataifa yanayoendelea.

Licha ya kwamba kilimo na ufugaji ndiyo mwanzo wa viwanda mathalani vya chakula, viatu, mavazi, samani, dawa na karibu kila bidhaa zinazotumiwa na binadamu, inaonekana sasa kuwa na kitisho kipya.

Wataalamu wanaonya kuwa uwekezaji huu unaohusisha ufugaji wanyama na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ni kitisho kipya cha mazingira na watu duniani kutokana na shughuli hizo kutumia maji mengi na maeneo makubwa ya ardhi tena yenye rutuba.

Ili kuzalisha, kilimo kinahitaji maji mengi na ardhi ya kutosha lakini ongezeko la joto duniani linasababisha uhaba wa maji (ukame) na magonjwa yanayoshambulia mifugo na mazao mashambani na kupunguza tija licha ya kuongeza gharama.

> **Kuku na bata hawahitaji maeneo makubwa ya kulishia ikilinganishwa na ng'ombe hivyo ni jukumu la wataalamu kusisitiza uzalishaji wa wanyama wadogo.**

Kufuati hali hiyo, Umoja wa Mataifa (UN) unawahamasisha watu kubadilika na kutumia zaidi vyakula vya mimea kama nafaka, protini, mboga na matunda yanavyozalishwa mashambani badala ya kupendelea ulaji wa nyama, maziwa, jibini na samli unaotokana na mifugo.

UN inaeleza kuwa maji ni muhimu kwa kilimo na ufugaji lakini pia vyote viwili huhitaji ardhi nyingi na ya kutosha ili kuzalisha, ndiyo maana inaona kuwa ili kuiokoa dunia na njaa, uhaba wa nishati na athari za mabadiliko ya tabianchi ni lazima kuachana na ulaji wa nyama na kugeukia matumizi ya vyakula vya mimea.

Mwelekeo huo mpya wa mfumo ulaji wa unaeleza kuwa ifikapo mwaka 2050 idadi ya watu duniani itafikia bilioni 9.1 hivyo ni wazi kuwa mazoea ya kula nyama kwa wingi na bidhaa za maziwa hayatakuwa endelevu si kwa mataifa maskini wala yaliyoendelea kiuchumi.

Itahitajika ardhi kubwa zaidi na maji mengi pia ili kulisha mifugo kadhalika na kwenye kilimo pia ili kuzalisha chakula cha kulisha idadi hiyo kubwa ya watu duniani.

Jitihada hizo zinamaanisha kutumia viuatifu , kemikali na mbolea ili kuzalisha kwa tija.

Ripoti ya Shirika la UN la Mazingira UNEP inasema: "Gharama za kilimo zinatarajiwa kuongezeka zaidi kutokana na matumizi ya pembejeo lakini kuzalisha mifugo na kuchakata bidhaa za nyama ....kwa hiyo kupunguza ulaji wa vyakula hivi unaweza kuwa mbadala."

Bidhaaa za nyama zinasababisha madhara zaidi. Majani na virutubisho vya kulisha wanyama navyo ni sawa na kuteketeza misitu ili kupata nishati.

Wanasayansi wa mazingira, wanasema kubadilisha mlo na kuachana na nyama ni muhimu kwa kuwa wanyama hawa wanamaanisha matumizi makubwa ya ardhi ya malisho, maji ya baridi (yasiyo na chumvi), dawa za kuwatibu jambo ambalo ni sawa na uzalishaji wa kilimo unaohitaji mbolea za viwandani, viatilifu, maji na ardhi ya kutosha.

Kilimo ambacho kinahusisha ufugaji wa wanayama, ndege na uzalishaji wa mazao ya maziwa mtindi na mabichi, jibini na samli kinahitaji asilimia 70 ya maji baridi lakini pia uzalishaji huo unatumia karibu asilimia 38 ya ardhi duniani.

Kadhalika kilimo hicho huchangia asilimia 19 ya gesi zinazolishaji 'greenhouse' nyumba zinazotumiwa kwenye kilimo huko ULaya.

Nchi zinazoendelea kama Tanzania ambazo kasi ya ongezeko la watu wake ni kubwa zinalazimika kutojiingiza kwenye mitindo ya uzalishaji na ulaji kama ilivyo kwa nchi zilizoendelea badala yake zinatakiwa kubadilika.

Kutokana na changamoto hii nchi maskini zinalazimika kufuata taratibu zake za kuziwezesha kupata chakula na mahitaji muhimu ya msingi ya maendeleo badala ya kuiga masuala ya kimagharibi.

Nchi hizi zina jukumu la kutengeneza teknolojia zitakazozinufaisha kwa mfano matumizi ya teknolojia ya nishati jadidifu (renewable energy), kilimo cha umwagiliaji na matumizi bora ya ardhi.

Hata hivyo kuna haja ya kupunguza mifugo badala ya kuwa na idadi kubwa ya wanyama ambao hula nyasi kwenye maeneo makubwa na kutumia maji mengi lakini hawana tija kwa mkulima na taifa pia.

Lakini wafugaji wazingatie kuwa hakuna haja ya kuwa na ng'ombe wengi au mifugo mingi, badala yake ufugaji wa ndege na wanyama wadogo unaweza kuwa na tija zaidi.

Kuku na bata hawahitaji maeneo makubwa ya kulishia ikilinganishwa na ng'ombe hivyo ni jukumu la wataalamu kusisitiza uzalishaji wa wanyama wadogo kama sungura na ndege.

BIASHARA

# Mila, desturi zinavyohusishwa na uhaba wa samaki Tanganyika

**Na Mwandishi Wetu**



Wavuvi katika Ziwa Tanganyika. **PICHA: MTANDAO**

JE ni kweli uhaba wa samaki katika Ziwa Tanganyika unatokana na kupuuza mila na desturi, ni suala ambalo wavuvi wanalijadili na wale wenye imani kuwa kuzipuuza tamaduni hizo ndiyo mwanzo wa uhaba wa kitoweo hicho.

Nchini Tanzania uvuvi hunufaisha zaidi ya watu milioni nne, huku wakazi wa mkoa wa Kigoma walioko upande wa magharibi, wakiutegemea kama shughuli kuu inayoendesha maisha yao kiuchumi.

Hata hivyo, shughuli hiyo katika eneo hilo kwa sasa inaenda kombo kutokana na uhaba wa samaki kwenye ziwa Tanganyika huku baadhi ya wavuvi wakiamini kupuuzwa kwa mila na desturi ni moja ya sababu inayochangia uhaba wa samaki.

Jitihada ya kusaka samaki ni kubwa japo mavuno ni madogo. Wanawake wanafika ufukweni asubuhi na mapema kuchuuza samaki lakini upatikanaji ni adimu.

Miezi kadhaa iliyopita wavuvi walikuwa wakipata zaidi ya ndoo 20 za samaki, lakini kwa sasa mambo ni tofauti.

Wanawake wanafika ufukweni asubuhi na mapema kuchuuza samaki lakini upatikanaji ni adimu. Huku wavuvi wengine wameamua kuachana na kazi hii na kuingia kwenye kilimo huku baadhi yao wanaona kuzipa kisogo mila na desturi ndiyo huchangia uhaba wa samaki katika ziwa hili.

Dunia Rashid ni mvuvi katika eneo hili anasema: 'Tunaweza kuchukua mwaka mzima tunavua samaki kama dagaa na samaki wakubwa wakubwa. Basi wale waliokuwepo, wazee wametoweka, wamebaki vijana wadogo, shughuli hawaziwezi kuzifanya."

Wazee wa kimila wanasema asiyesikia la mkuu huvunjika mguu, wanainyooshea vidole teknolojia kama chanzo cha vijana wengi kuachana na mila na desturi ambazo huamini ndiyo njia pekee ya mafanikio.

Machifu au viongozi wa kitamaduni walikuwa wanafanya matambiko, wanaomba dua kwa Mwenyezi Mungu kutumia mambo ya asili, na kweli Mungu alikuwa anatoa jibu.

Moshi Haruna ambaye ni mvuvi, anawaelemisha wavuvi wenzake dhidi ya kuamini kuwa mila ndio husababisha uhaba wa samaki

Mboga zilikuwa zinavulika na kupatikana, anasema mzee Muhsini Mmbanga.

Katika mkusanyiko mkubwa mvuvi mwingine katika eneo hili anawaelemisha wavuvi wenzake dhidi ya kuamini kuwa mila ndiyo husababisha kushindwa kupata mavuno ya samaki.

'Wale wanaoendekeza mila, wanaamini kwamba bila ya mila hawawezi kupata. Ila sisi ambao hatuamini mila tunaamini, Mungu anatoa kulingana na vile anaona awalisheje binadamu.

Kwa wa mila wanakula, na sisi ambao hatuamini mila tunakula na tunaishi' anaeleza Haruna.

Mamlaka za serikali zinazoshughulikia uvuvi katika ziwa hili, zinasema uhaba wa samaki kwa msimu huu sio jambo la kiimani.

Edimund Kajuni, Ofisa wa vuvi Kigoma anasema: "'Kwa uhalisia ni kwamba katika ziwa Tanganyika tuna misimu mitatu ya uvuvi. Kuna kipindi ambacho ni msimu mb'aya, ambao ndio msimu tuliopo hivi sasa unaoanza mwezi wa tano Mei hadi wa Julai' anaeleza Ofisa Uvuvi Kigoma.

> **Wale wanaoendekeza mila, wanaamini bila ya mila hawawezi kupata.**

Imani potofu, dhana duni za uvuvi ni moja ya sababu zinazotajwa kurudisha nyuma sekta ya uvuvi nchini Tanzania.

Baadhi wanaona jitihada zaidi zinahitajika kuifanya sekta hii iweze kuinufaisha jamii na kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa. **BBC**

# TARI Ilonga kumaliza shida ya mafuta nchini

**INAENDELEA UK.17**

teknolojia za mbegu za kisasa za alizeti, mkikunde na mazao ya nafaka kama mahindi,mtama na uwele ili kuwasaidia wakulima kuondokana na kilimo cha mazaea na kulima kisasa ili kuzalisha malighafi zinazotokana na mazao ya kilimo kwajili ya kulisha viwanda.

Anasema watafiti wa TARI Ilonga,tayari wameanza kuwakusanya watalaam wa kilimo

na ugani kutoka katika kata zote kwa kuanzia Wilaya ya Kilosa na baadae kwenda katika wilaya nyingine katika mkoa wa Morogoro .

Lengo ni kuwapa mafunzo maalumu ya kuhusu teknolojia za mbegu za kisasa ili kwenda kutoa elimu kwa wakulima kwa kuwaelezea na kuwafundisha ili waweze kuzitumia ili kuongeza uzalishaji.

Dk Meriyo, anasema kuwa mpango huo utawafanya watafiti wa TARI Ilonga kuwafuata wakulima katika kata zote kwa kuanzia na Wilaya hiyo, kuwafundisha wakulima kuhusu kilimo bora cha kisasa na chenye kutumia teknolojia za mbegu za kisasa ili waweze kubadilika na kuachana na kilimo chenye mazoea na kufanya kilimo cha kibiashara ili kuwa na uhakika wa chakula na ziada.

Akizungumzia kuhusu mkakati wa zao la alizeti, anasema kuwa pamoja na TARI Ilonga kupewa majukumu ya kuzalisha mbegu za kisasa za alizeti ili kuongeza uzalishaji wa mafuta hapa nchini teknolojia zote za mbegu za kisasa zinazofanyiwa utafiti zikikamilika na kuzalishwa mbegu zitasambazwa haraka kwa wakulima katika mikoa inayolima zao hilo kwa wingi.

**MRATIBU WA UTAFITI**

Mratibu wa Utafiti Kanda ya Mashariki kutoka TARI Ilonga, Meshack Makenge, anasema jukumu

kubwa kwao ni kuzalisha mbegu za teknolojia ya kisasa na kuzisambaza kwa wakulima ili waweze kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija na cha kibiashara kwa ajili ya kulisaidia taifa liweze kuwa na uhakika na usalama wa chakula.

Makenge ambaye ni Mtafiti wa Kitaifa wa Mikunde anasema kuwa TARI Ilonga pia imepewa jukumu la kuzalisha mazao ya mikunde kama choroko, maharage, dengu na mbaazi ,mazao ya nafaka kama mahindi, mtama na uwele pamoja na mazao ya mbegu za mafuta kama alizeti na mazao ya mizizi kama mihogo na viazi lishe na kuhakikisha teknolojia hizo zinawafikia wakulima.

Anasema kuwa katika mpango wa serikali wa kuelekea uchumi wa viwanda,TARI Ilonga imejipanga

kikamilifu kuhakikisha inakuwa injini ya kuwepo kwa viwanda hivyo na kwa sasa wameamua kuwasaidia wakulima kulima kwa kutumia mbegu za teknolojia ya kisasa ili kuweza kuzalisha malighafi zinazohitajika katika viwanda hivyo vilivyoanza kujengwa hapa nchini.

**UMWAGILIAJI**

Ofisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Wilaya ya Kilosa Elina Danstun , anasema mkakati wa wilaya hiyo katika msimu ujao wa kilimo ni kuongeza uzalishaji wa chakula na ziada ili kusaidia mpango wa Serikali katika kuelekea uchumi wa viwanda hivyo mafunzo ya teknolojia hizo watayafikisha moja kwa moja kwa wakulima.

UCHUMI

# Ulaya ni ukurasa mpya, Ugiriki ikiondoa serikali, sera za kijamaa

**Na John Kimbute**



Waziri Mkuu wa Ugiriki, Kryakos Mitsotakis, aliyeapishwa karibuni. **PICHA MTANDAO.**

VIONGOZI wakuu wa Umoja wa Ulaya (EU), ambao sasa wako mbioni kuacha madaraka kupisha viongozi wengine walioteuliwa katika mkutano wa hivi karibuni wa Baraza la Mawaziri la EU hawajapata nafasi ya wazi ya kusherehekea matokeo ya uchaguzi nchini Ugiriki.

Serikali ya mwelekeo wa ujamaa imeondolewa madarakani na kupisha chama chenye mwelekeo wa kihafidhina, New Democracy, katika mazingira yanayokalimisha kukwama kwa ukinzani kwa sera za soko huria barani Ulaya, ambako mkasa wa deni la Ugiriki kwa taasisi za fedha za EU umekuwa ukitawala.

Kuna wakati wapiga kura wa Ugiriki walikuwa wanaambiwa adui yao mkuu ni Waziri Mkuu wa Ujerumani Angela Merkel au Kansela Merkel katika cheo rasmi.

Nje ya mataifa yote ya Ulaya, deni la Ugiriki hasa kwa taasisi za fedha za EU mahitaji ya ushirikiano kati ya nchi zinazoshikilia deni la Ugiriki, hasa Ujerumani na Ufaransa kutokana na mabenki husika katika deni hilo kuwa zaidi ya nchi hizo.

lilikuwa ni mtihani wa uendeshaji wa taasisi za kimataifa kidemokrasia katika suala la madeni. Madai makubwa kisiasa nchini humo, kama ilivyokuwa kwa Afrika na baadhi ya nchi zinazoendelea ilikuwa ni kufutwa kwa madeni, wakati sehemu kubwa ni ya kibiashara.

Haikuwa mikopo ya serikali yenye gharama nafuu ila ya mabenki ya biashara, ikabidi Ugiriki ipewe mikopo ya kitaasisi kulipa madeni, ijifunge mkanda.

Moja ya mistari ya kiitikadi iliyokuwa inasumbua katika uwanja wa siasa, vyombo vya habari na mijadala ya kitaaluma ni:

'Utumwa wa deni la Ugiriki: Wananchi watalipa,' inayomaanisha kuwa wenye fedha, au baadhi wangewaita mafisadi, hawana wasiwasi, ni watu wa chini ambao wataumia Serikali ikikaza mkanda ipangue huduma za jamii, ajira sekta ya umma, na kuongeza kodi.

Mjadala katika maandamano 'yasiyoisha' na mikutano ya hadhara hadi kufikia 2012 ikawa ni kutafuta njia ya kuwalipisha mabepari, wenye mabenki na waliokuwa wanapeleka hesabu feki serikalini kuhusu malipo ya kandarasi tofauti.

Ila tatizo kubwa zaidi lilikuwa serikali yenyewe, kuwa ndani ya mfumo wa sarafu moja barani Ulaya bila kufuata mipangilio ya sera, ikajaza deni.

Kiitikadi wananchi walikuwa wanaitetea serikali kwa mfano kuhusu kiwango cha ajira katika sekta ya umma, na hata usahihi kwa hesabu za serikali katika maeneo kadhaa kama hifadhi ya jamii (kukosa kazi, akiba ya uzeeni au pensheni 'endelevu' kwa misingi kuwa hayo ni masuala ya wananchi wa Ugiriki kuamua, kupitia serikali yao na Bunge.

> **"Ila tatizo kubwa zaidi lilikuwa serikali yenyewe, kuwa ndani ya mfumo wa sarafu moja barani Ulaya bila kufuata mipangilio ya sera, ikajaza deni.**

Tatizo ni kuwa baada ya kufanya maamuzi hayo, tofauti kati ya mapato na matumizi ya Ugiriki inakuwa sehemu ya mizania ya malipo barani Ulaya kutokana na Ugiriki kuwa katika mfumo wa sarafu moja.

Bila ulinganishi mapato na matumizi (deni la taifa lisizidi asilimia tatu ya pato la taifa) sarafu inaanza kupwaya.

Unaweza kusema kuwa Ugiriki imetumia takriban miaka 10 tangu mjadala huo uanze hadi uchaguzi mkuu 2012 na hadi sasa. Ni mara ya kwanza chama chenye mrengo wa ujamaa kilichofaidika na wimbi la uzalendo dhidi ya kujifunga mkanda na kulipa madeni ya mabenki ya Ujerumani, Ufaransa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kimepoteza kura kwa kiasi cha kuwa na uhakika watu hawana imani nacho.

Walipoteza kwanza viti uchaguzi Bunge la Ulaya. Wachunguzi wa habari wanasema kuwa suala la madeni linachangamsha hisia nchini Ugiriki kutokana na historia yale, kwani imebaki kama ilivyokuwa enzi za karne sita kurudi nyuma kabla ya millennia Ukristo kuanza.

Kuwaondoa watu katika utumwa wa madeni ni moja ya vianzio chanya vya fikra ya demokrasia Uyunani ya kale, na pale serikali za kisasa zinapokataa matakwa ya mabenki na mashirika ya fedha, au nchi wahisani kubinafsisha na kupunguza matumizi serikalini, dhana hiyo inainuliwa kama kielelezo cha tatizo.

Kumbe ni vitu viwili tofauti kwani utumwa wa deni ni wa mtu binafsi anayepoteza mali zake kulipa deni na hasa kutokana na riba, wakati nchi haipotezi mali zozote ila zinatoka sekta ya umma kuwa binafsi.

Taarifa nyingine zinaeleza kuwa Yanis Varoufakis, aliyekuwa Waziri wa Fedha wakati wa misukosuko mikubwa zaidi kuhusiana deni la Ugiriki mwanzoni mwa muongo huu, alishaona tangu mapema mwaka jana kuwa chama cha ujamaa (Kisoshalisti,Syriza) hakitaweza kuendelea na harakati za kupambana na sera za uimla kuhusu madeni.

Akajiunga na chama cha mrengo wa kushoto zaidi lakini kimekuwa kikishindwa katika chaguzi; kilifikia tu asilimia tatu inayotakiwa ya kura zote (uwakilishi wa uwiano) kiendelee kuwa sehemu ya Bunge la Ugiriki.

Ina maana makada wa Ujamaa wanajiunga katika mapinduzi, wakati Ujamaa wenyewe unazidi kukataliwa.

Invyoelekea ni kuwa kulikuwa na uingiliaji kati wa kina katika mwelekeo wa kutatua matatizo ya madeni wakati IMF ilipochukua nafasi zaidi, lakini baadhi ya wataalamu wanasema yako maeneo ilikwepa kufanya ilichokifanya Argentina miaka iliyopita.

Moja ya maeneo chanya ilikuwa ni kutofautisha kati ya kutokuwa na fedha (yaani mzunguko hafifu wa fedha, hivyo kusababisha uchumi kuzorota) na kutokulipa madeni (suala la muda mrefu zaidi).Licha ya kuwa ni mjadala mrefu, Argentina ni nchi inayojitegemea kwa bajeti yake na sarafu, wakati Ugiriki iko katika mfumo mpana zaidi.

Washirika wa Ugiriki wanakuwa na sauti ambayo wale wa Argentina hawana, kwani ni sekta binafsi inadaiwa madeni wakati Ugiriki yaliendana na hesabu za serikali.

Nguvu ya ziada iliyosaidia kubadilisha upepo nchini Ugiriki ni mkwamo wa jumla wa sera za kijamaa barani Ulaya na kuingia madarakani kwa serikali za kizalendo zenye mwelekeo wa taifa lenye nguvu, siyo lililogubikwa na madeni.

Ujio wa serikali ya Rais Donald Trump nchini Marekani pia uliisaidia Ugiriki kujiegemeza zaidi kwenye mwelekeo wa kiliberali kwani uhusiano wake na Marekani ulikuwa unaimarika, huku uhusiano wa Marekani na Uturuki, mshindani wake wa jadi, ukizorota.

Kimsingi ni kuwa baada ya Waziri Mkuu Alexis Tsapiras (wa kijamaa) kuanza kutekeleza matakwa ya 'troika,' utatu wa kusimamia madeni ya Ugiriki (Tume ya Ulaya, Benki Kuu ya Ulaya na IMF) alishaanza kuhama sera hizo; mabadiliko Ulaya na Marekani 2017 yalileta mwamko mpya wa kuachana na Ujamaa, kufuata sera za kiliberali kuondoa vizuizi vilivyobaki.

Mwaka 2017 ulileta mabadiliko makubwa kuhusu nafasi ya Ugiriki miongoni mwa nchi za Umoja wa Kujihami wa Nchi za Ulaya na Marekani (NATO) , kwani Ujerumani iliieleza rasmi Uturuki iache ndoto zake za kujiunga ua Umoja wa Ulaya.

Kuingia madarakani kwa Rais Emmanuel Macron huko Ufaransa pia kulileta msukumo kwani mwelekeo wa kupinga uliberali ulizidi kupoteza umaarufu na pia uhusiano wa nchi hizo mbili kukua zaidi.

Ukawa ndiyo wakati utawala wa Trump unaweka mikakati ya kujenga uwepo wake Bahari ya Mediterranean kwa nguvu zaidi ikijiandaa kuweka mkazo zaidi kwa vikwazo dhidi ya Iran na kuichunga kwa karibu Uturuki, na hata Russia.

Rais Trump akatoa mpango wa mabilioni uwekezaji sekta ya nishati Ugiriki, huku IMF na EU zikikubaliana msaada mpya (mkopo) dola bilioni 101 baada ya Bunge kupitisha kodi mpya.

Hivyo serikali mpya, ikianza ubinafsishaji Tsapiras alioukwepa, deni la taifa litapungua zaidi.





Waziri wa Madini, Dotto Biteko na maofisa madini kutoka wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wakikagua daftari la kutunza kumbukumbu za madini la mmoja wa wanunuzi wa madini, Sitta Kishepu, ambaye hununua kutoka kwa wachimbaji wadogo. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mbaroni kwa kumiliki gobole, laini 5 za simu

**Na Grace Mwakalinga,**

MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia Enock Wilson (28), mkazi wa Kitongoji cha Misungwiji wilayani Chunya kwa tuhuma za kumiliki gobole kinyume cha sheria.

Vilevile, jeshi hilo linamshikilia Galson Mgema (46), mkazi wa Mtaa wa Shewa, Kata ya Mwakibete mjini Mbeya kwa tuhuma za kumiliki na kutumia laini tano za simu zikiwa na usajili wa majina ya watu wengine kutapeli.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, ilieleza kuwa Julai 15, mwaka huu, majira ya saa tisa mchana, katika Kitongoji cha Misungwiji, Kata ya Matwiga, Wilson ambaye ni mkulima, alikamatwa nyumbani kwake kwa kosa la kumiliki silaha kinyume cha sheria na taratibu za nchi.

Kamanda Matei alidai taarifa za mtuhumiwa kumiliki silaha hiyo zilitolewa na wasamaria wema na Jeshi la Polisi lilifanya jitihada za kumkata.

"Tunarajia kumpeleka mtuhumiwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika. Natoa rai kwa wananchi kuacha tabia ya kumiliki silaha bila kibali cha serikali ili kulinda usalama kwa wananchi wanaowazunguka," Kamanda Matei alieleza katika taarifa yake hiyo.

Kuhusu Mgema, Kamanda Matei alidai kuwa mtuhumiwa alikuwa anatumia laini hizo za Kampuni ya Mawasiliano ya Tigo kuwatapeli watu kwa kuandika ujumbe wa "tuma pesa kwa namba hii".

Alisema upelelezi unaendelea kuhusu tuhuma za kufanya makosa ya mtandao ili afikishwe kortini kujibu tuhuma zinazomkabili.

# Ataja kilichoikwamisha Kyela

**Na Grace Mwakalinga,**

KYELA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, Dk. Hunter Mwakifuna, amewataka watumishi na madiwani wote wa wilaya hiyo kuachana na tofauti zilizojitokeza awali na kusababisha kukwama kwa shughuli za maendeleo.

Dk. Mwakifuna aliyasema hayo wakati wa kikao maalum cha Baraza la Madiwani kilichokuwa na lengo la kujadili changamoto mbalimbali zinazoikabili halmashauri.

Alisema Wilaya ya Kyela ilikumbwa na misukosuko na misuguano baina ya watumishi wa halmashauri na madiwani wakilalamikia baadhi ya viongozi kutumia vibaya madaraka yao.

Alisema hali hiyo imekwamisha jitihada za serikali za kuleta maendeleo ya wananchi.

"Halmashauri yetu haikuwa na utulivu kwa muda kidogo sababu ya kutoelewana kwa viongozi, serikali iliingia kati sasa hali ni shwari, madiwani na watumishi wa halmashauri wameondoa tofauti zao na wamejipanga kuwatumikia wananchi," Dk. Mwakifuna alisema.

Alisisitiza madiwani na watumishi wa halmashauri kusimamia miradi ya maendeleo ambayo ilikwama kutokana na migogoro iliyokuwapo na kuunga mkono jitihada za serikali.

# Vyama ushirika vyataja sababu uzalishaji duni mazao

**Na Grace Mwakalinga,**

MBEYA


VYAMA vya ushirika vimesema kuchelewa kufikishwa kwa pembejeo za kilimo katika maeneo yao kumekuwa changamoto inayosababisha wakulima kutopata mazao ya kutosha.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku mkoani Shinyanga, Emmanuel Cherehani, aliyasema hayo wakati wa kikao cha wadau wa tumbaku nchini.

Cherehani alisema changamoto ya kuchelewa kwa pembejeo za kilimo, zikiwamo mbegu, imechangia wakulima kupata mazao machache.

"Ili mkulima apate mavuno mengi lazima aende sambamba na mabadiliko ya hali ya hewa hasa msimu wa kilimo, sasa changamoto ya kuchelewa kwa pembejeo za kilimo inakwamisha mkulima kulima mazao kwa wakati, tunaomba serikali na wadau wengine kuangalia namna nzuri ya ugawaji pembejeo," Cherehani alisema.

Aliongeza kuwa wakati wa ugawaji pembejeo za kilimo, vyama vya ushirika viachiwe jukumu la kugawa pembejeo kwa kuwa wao wanahusika na watambua vyema misimu ya kilimo.





## TIRA yaagizwa kufuatilia kampuni za bima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA), kanda ya kati kufuatilia kampuni za bima zinazofanyakazi kibabaishaji ili ziweze kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Vile vile serikali imeitaka TIRA, kutoa elimu kuhusu faida watakazopata wananchi baada ya kujiunga na mfuko wa bima ili kuwarahisishia kupata matibabu haraka hata wakiwa hawana pesa mkononi.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge, wakati wa maadhimisho ya siku ya bima, Kanda ya Kati yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma.

Dk. Mahenge alisema, TIRA inapaswa kuwa mstari wa mbele kuzifuatilia kampuni hizo ambazo zinachelewesha fidia kwa wananchi ikiwamo kuwadanganya wananchi katika utoaji huduma hizo, kwa sababu zinachafua tasnia ya bima hapa nchini.

"Naomba mzifuatilie kampuni zinazofanya kazi kiubabaishaji tunahitaji kuona watu wanaofanyakazi kiufasaha ili kuwashawishi wananchi wajiunge na mfuko wa bima kupitia kampuni mbalimbali," alisema Dk. Mahenge.

Alisema lengo la serikali ni kuona kila mmoja anakuwa na bima hususani ya afya ambayo ni muhimu kwa kila mmoja kuwa nayo.

Akizungumzia suala la elimu kwa wananchi kuhusu kuwa na Bima ya Afya, alisema bado elimu hiyo haijawafikia walengwa kutokana na kuwa mwitikio wa maadhimisho hayo umekuwa mdogo tofauti na matarajio ya waandaaji.

"Naomba muongeze bidii katika utoaji elimu kwa wananchi kuwa na bima ya afya kwa sababu itasaidia kupunguza vifo vinavyotokana na jamii kukosa pesa ya matibabu," alisema Dk. Mahenge.

Alisema wana kila sababu ya kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wote waweze kuchukua Bima ya Afya katika kampuni mbalimbali ambazo zinahusika na utoaji wa huduma hiyo iwe kwa vikundi au mtu mmoja mmoja.

Vile vile, alizishauri kampuni zinazotoa huduma ya bima kutoa Bima ya Afya kwa sababu ni muhimu kwa jamii.

Naye Meneja wa TIRA Kanda ya Kati, Stella Rutaguza, alisema lengo la maadhimisho hayo ni pamoja na kuunga mkono juhudi za serikali kuinua uchumi kupitia bima zinazokatwa na wananchi.

Alisema kaulimbiu ya mwaka huu 'Kata bima inua uchumi wako na taifa', inalenga kuishawishi jamii kumiliki bima za afya, ikiwamo ya majanga na vyombo vya moto.

# Kitengo kuangalia upya usanifu mikataba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeunda kitengo cha usanifu ambacho kitasaidia kuangalia upya usanifu wa mikataba na gharama zinazowekwa na makandarasi kabla ya ujenzi wa miradi ya maji, ili kuziba mianya ya ubadhirifu katika sekta hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma wakati wa mkutano na mameneja wa ngazi ya mkoa na wilaya wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Jumaa Aweso, alisema lengo la kuanzisha kitengo hicho ni pamoja na kuwa miradi mingi ya maji imekuwa na gharama kubwa tofauti na uhalisia wa kazi yenyewe jambo ambalo linachangia kucheleweshwa kukamilika kwa miradi hiyo.

Naibu Waziri huyo alisema kwa sasa wizara hiyo ina timu ambayo itakuwa ikiangalia gharama za miradi inayokwenda kutekelezwa ili ziweze kuendana na uhalisia wa kazi yenyewe inayofanywa.

Aweso alisema tayari wizara ina mpango wa kutekeleza miradi ya maji kwa force account ili kuachana na makandarasi wajanja wajanja wasio waaminifu katika ujenzi wa miradi ya maji jambo ambalo litachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza ubadhirifu katika miradi inayokwenda kutekelezwa. "Mnatakiwa mkafanye kazi kadiri ya uwezo wenu lengo ni kuiboresha sekta ya maji mijini na vijijini," alisema Aweso.

Alisema baada ya kikao hicho serikali isingependa kusikia changamoto ya maji vijijini na mijini na kuongeza kuwa wanapaswa kuleta nidhamu katika utendaji kazi kwenye maeneo waliopangiwa ili kuisimamia sekta ya maji kwa weledi.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Kitila Mkumbo alisema ili kufikia malengo waliojiwekea ni lazima watenge fedha kwa ajili ya kukarabati miradi ya maji ya zamani ambayo haifanyi kazi na mipya ili iweze kutoa huduma bora ya maji kwa wananchi wa vijijini na mijini. Prof. Mkumbo alisema pamoja na changamoto zinazoikabili sekta hiyo lazima bajeti ya fedha iwekwe ili waweze kukarabati miradi hiyo jambo ambalo upatikanaji wa maji kuongezeka kwa asilimia kubwa kwa upande wa mijini na vijijini.

"Ni lazima mameneja mlioteuliwa katika ngazi zote mfanye kazi kwa bidii kwa sababu tunahitaji kufikia malengo tuliojiwekea ya kuongeza asilimia za upatikanaji maji mijini na vijijini ifikapo 2020," alisema Prof. Mkumbo.

Alisema mameneja mnapaswa kushirikiana katika utendaji wenu wa kazi ikiwamo kufanya kazi vizuri jambo litakaloweza kutimiza azma iliowekwa na serikali. Alisema kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Taasisi ya Takwimu ya Taifa, upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama nchini kwa hivi sasa ni asilimia 85, lakini wao wanataka hadi ifikapo 2020 wafike asilimia 95 na vijijini ifike asilimia 84.

Alisema wafanyakazi waliopewa jukumu katika vitengo hivyo wanafanyakazi kubwa ya kuhakikisha wanafikia malengo yao ili wananchi waweze kupata huduma bora ya maji hapa nchini.




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akizungumza wakati wa kufungua kikao kazi cha siku tatu kwa wataalamu wa sekta ya ardhi pamoja na wadau mbalimbali uliofanyika jana jijini Dodoma. Aliagiza usajili na hatimiliki za ardhi kuanza kutolewa mikoa yote ifikapo Oktoba mosi, mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kunambi awaonya wanaouza hifadhi za misitu

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, ametoa onyo kwa viongozi wa mitaa wanaouza maeneo ya hifadhi za misitu pamoja na wananchi ambao wananunua viwanja ambavyo havijapimwa wala kupangwa kuacha kwa kuwa maeneo hayo yapo katika mpango kabambe wa jiji 2019/39.

Kunambi aliyaeleza hayo jijini hapa wakati alipokuwa akizungumza na wenyeviti wa mitaa, madiwani na wapima ardhi ambao wanatarajiwa kusimamia upimaji na urasimishaji maeneo.

Alisema kumekuwa na tabia ya wananchi kununua viwanja ambavyo havijapimwa na kudai kwamba kwa kufanya hivyo ni sawa na kununua mbuzi kwenye gunia kwa kuwa jiji limetenga maeneo kwa ajili ya misitu yakiwamo hayo ambayo wanauziwa.

"Yeyote ambaye anauziwa ardhi ambayo haijapimwa asije kulalamika ajue ameuziwa mbuzi kwenye gunia, maeneo yanauzwa na jiji, kuna maeneo tumetenga kwa ajili ya misitu, sio kwamba nimepanga mimi hapana ni wanaohusika, nunua viwanja maeneo ambayo yanatambulika," alisema Kunambi. Vile vile, Kunambi alisema jiji limejipanga kupima zaidi ya viwanja 200,000 katika awamu hii.

"Tangu Desemba 2017 tumepima viwanja zaidi ya 100,000 wenzetu waliotuachia ndani ya miaka 43 wamepima viwanja 69,000 sasa tunaenda kupima viwanja 200,000 huu ni uwezo wa kipekee kabisa unaweza kusema sio uwezo wa kibinadamu, hakuna miujiza hapa, tunafanya kazi kwa mambo matatu, fikra chanya katika maendeleo, kujitoa na uzalendo," alisema.


Alisema upimaji viwanja na kurasimisha maeneo mapya utafanyika katika mitaa 23 na kata 15, huku kampuni 15 zikipewa tenda ya kupima maeneo hayo.

Hata hivyo, Kunambi alitoa angalizo kwa wapimaji hao na kuwataka kuangalia namna ya kuweka mifumo bora ya kupima pamoja na kuzingatia sheria za mipango miji.

Akizungumzia kuhusu kero za ardhi, mkurugenzi huyo alisema mpaka Desemba mwaka huu, watakuwa wamemaliza kutatua kero mbalimbali zilizojitokeza.

"Tumerithi zaidi ya migogoro 5,000 kutoka CDA ukichanganya na yetu mpaka Desemba tutakuwa tumeimaliza, kwa kuwa mpaka sasa tumetoa viwanja mbadala 3,400 vyenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni nne," alisema Kunambi.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Nzuguni, Aloyce Lwena, alitoa ushauri kwa jiji kusimamia zoezi hilo bila ya kumwonea mtu.





Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, akimsaidia mwananchi kuchota maji katika Kata ya Mwada, wilayani Babati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Watoto wanaodhalilishwa hawapati ushauri nasaha'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA wa ushauri nasaha kutoka katika kituo cha mkono kwa mkono Hospitali ya Mnazi Mmoja, Suhaila Abdullah Salim, amesema watoto wengi wanaofanyiwa vitendo vya udhalilishaji wanakosa huduma ya ushauri nasaha.

Aliyasema hayo katika kikao cha kujadili masuala ya udhalilishaji wa kijinsia kwa kamati ya kupambana na vitendo hivyo ya Wilaya ya Magharib B Unguja, kilichoandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa) Ofisi ya Zanzibar.

Alisema wazazi wanapofika na watoto wao waliofanyiwa udhalilishaji katika hospitali hiyo hutakiwa kupangiwa siku ya mtoto wake kupewa ushauri nasaha, lakini huwa hawawapeleki.

Alisema mtoto anayefanyiwa udhalilishaji huathirika kisaikolojia na anahitaji huduma ya ushauri nasaha.

Alieleza kuwa athari ambazo wanaweza kuzipata watoto waliodhalilishwa na kukosa huduma za ushauri nasaha baadaye hulipiza kisasi kwa kufanya kitendo cha ubakaji au ulawiti.

"Tuiombe jamii kuona kuwa huduma ya ushauri nasaha ni muhimu kama zilivyo huduma nyingine hivyo ni vyema kuhakikisha watoto wanawapeleka katika vituo vya afya kwa ajili ya kupata ushauri nasaha kama wanavyopewa maelekezo na wataalamu," alisema.

Pia alisema hivi sasa kuna wimbi kubwa la watoto kujiingiza katika mapenzi wakiwa bado na umri mdogo hali ambayo inasababisha kuongezeka kwa vitendo vya ubakaji.

Alieleza kuwa baadhi ya watoto wanaofanyiwa udhalilishaji huficha na hawatowi taarifa kwa wazazi wao kwa sababu wanaowafanyia vitendo hivyo ni watu wao wa karibu katika familia.

"Baadhi ya watoto wamekuwa wanaficha kutoa taarifa kwa sababu ya hofu maana wengi wao wanafanyiwa vitendo vya udhalilishaji na watu wao wa karibu," alisema.

Kadhi wa Mahakama ya Mwanakwerekwe, Othman Ame Choum, alisema kuwa bado usiri umetawala katika jamii hali ambayo inasababisha ongezeko la vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alieleza kuwa kuna migogoro mingi katika ndoa na kusababisha kuwapo kwa wimbi la talaka na watoto kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji ikiwamo kutelekezwa.

# RC: Mwenge umeleta umakini kwa viongozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema ujio wa Mwenge wa Uhuru umeongeza umakini wa viongozi na watendaji wa taasisi mbalimbali za mkoa huo.

Alisema ili kuhakikisha Mwenge huo unakuwa na tija kwa jamii, viongozi wanaokabidhiwa dhamana wanapaswa kuzingatia miongozo na taratibu ili kufanikisha utekelezaji wa kazi na miradi.

Ayoub aliyasema hayo katika harakati za kukimbiza Mwenge huo ambao upo katika mkoa wake na kuzindua miradi tisa ndani ya mkoa huo.

Aliwahakikishia wakimbiza Mwenge kuwa miradi yote tisa itakayotembelewa imekidhi vigezo vilivyowekwa.

"Mwenge huu utakimbizwa katika wilaya zote tatu na kuifikia miradi tisa yenye thamani ya Sh. bilioni 8.465," alisema Ayoub.

Akisoma taarifa ya makabidhiano ya Mwenge huo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kusini Unguja, Fatma Mohammed, alisema ulipokuwapo mkoani humo ulikimbizwa kwa umbali wa kilomita 160 na kutembelea miradi 10 katika sekta za maji, afya pamoja na kutoa elimu ya rushwa na malaria.

"Katika mkoa wetu, Mwenge uliweka mawe ya msingi, kukagua na kuzindua miradi inayoendana na ujumbe mahsusi wa mwaka huu unaohimiza kutunzwa na kuendeleza vyanzo vya maji na ushiriki wa serikali za mitaa kwa wenzetu wa Tanzania Bara," alisema Fatma.

Akitoa ujumbe wa Mwenge katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Magharibi 'B', kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Mzee Mkongea Ali, aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuendeleza vita dhidi ya rushwa, umaskini na maradhi ili kuhimiza maendeleo ya taifa.

Alisema iwapo wananchi watachukia vitu hivyo, viongozi na watendaji wa sekta ya umma na binafsi watawajibika kikamilifu.

Alisema Mwenge wa Uhuru umeasisiwa mwaka 1961 kwa lengo la kuleta ukombozi wa Tanganyika na Zanzibar, lakini baada ya uhuru falsafa hiyo imeendelezwa na kuwa chombo cha kuhimiza maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

"Tutakapochukia rushwa na uhujumu uchumi, adui maradhi na umaskini utaondoka pole pole jambo ambalo litachangia kasi ya maendeleo ya wananchi," alisema.

Akiwa katika kituo cha afya Fuoni, alipokea taarifa ya hali ya malaria katika Wilaya ya Magharibi 'B' mbali ya kuhimiza matumizi sahihi ya vyandarua kama kinga dhidi ya malaria, aliwataka kina baba kujenga tabia ya kuhudhuria kliniki sambamba na wenza wao ili kujua maendeleo ya afya za watoto wao.

"Niwapongeze wanaume wenzangu ambao mmekuja na wake zenu kwa kuwa kufanya hivyo kunaongeza umakini juu ya afya za watoto na kuongeza uwezo wa uzalishaji mali," alieleza Mkongea.

Siku ya kwanza ya mbio hizo katika mkoa huo, ulikagua ukarabati wa tangi la kuhifadhia maji na pango la Chomoani liliopo Dimani na kukagua ujenzi wa shule ya maabara ya sayansi inayojengwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliyopo Kisauni.

# Waziri aagiza ujenzi kukamilika kwa wakati

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka makandarasi wa majengo ya "School hubs" kuhakikisha wanakamilisha majengo hayo kwa wakati waliokubaliana na katika kiwango kilicho bora.

Akizungumza katika ziara ya kuangalia ujenzi wa majengo hayo ikiwamo ya Kisauni na Mwera Regeza mwendo, alisema serikali haitomfumbia macho mkandarasi yeyote atakayejenga miundombinu chini ya kiwango.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha majengo yote yanakua katika kiwango bora ili huduma zinazotolewa hasa za kielimu zitolewe katika mazingira salama.

Vile vile, aliwataka makandarasi hao kuwa wawazi katika kila sehemu yenye upungufu ili kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa muda waliokubaliana.

Aliwataka kuweka utaratibu wa kujenga uzio majengo yote ya "School hubs" ili kuyalinda mazingira ya jengo kutokana na uvamizi wa watu pamoja na vifaa vitakavyokuwamo ndani ya majengo.

Naye mmoja wa makandarasi wa majengo hayo, Sililo Mateyas, alimhakikishia waziri huyo kuwa watajenga majengo hayo katika ubora na kuyakabidhi kwa wakati.

Jumla ya School hubs 24 ambazo zitasaidia kwa ajili ya kufundishia masomo ya Sayansi, Hesabu na Kiingereza, zinajengwa zikiwamo 14 kwa Unguja.

## Katapila ya kisasa yazinduliwa Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa sekta ya ujenzi nchini sasa wamepata ahueni baada ya kuanzishwa kwa katapila ya kisasa zaidi yenye ufanisi zaidi na yenye kupunguza gharama za uendeshaji kwa kiasi kikubwa.

Uzinduzi wa katapila hiyo ulioandaliwa na Mantrac Tanzania, mawakala wa uuzaji wa katapila walioidhinishwa, ulifanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na makandarasi, waendeshaji wawakilishi kutoka Kampuni ya Caterpillar na wadau wengine kwenye sekta ya utalii. Akizungumza kwenye hafla hiyo jana, Gary Martin, Mtaalamu Mwandamizi wa Masoko wa Caterpillar, alisema kwamba katapila hizo - New Generation Hydraulic (NGH) Caterpillar ambazo ni mpya katika soko la Tanzania na zitaleta mapinduzi kwenye sekta hiyo kutokana na ukweli kwamba ni nzuri kiuchumi na zenye ufanisi mkubwa.

Alibainisha kwamba Mantrac Tanzania Limited wameingia kwenye mkondo wa mageuzi ya viwanda, kwa kuhakikisha kwamba hakuna kupoteza muda katika utekelezaji wa maelekezo ya serikali kwa ajili ya kuigeuza Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Alisema NGH Caterpillar hupunguza muda wa kazi kwa nusu na wakati huo huo kupunguza matumizi ya mafuta kwa asilimia 25, huku kukiwa na ongezeko la uzalishaji kwa asilimia 45. "Imechukua miaka mitano kubuni mashine hii, na ilibuniwa baada ya mapendekezo kutoka kwa wateja," alisema. Mmoja wa wateja ambaye amenunua mashine hiyo mpya, Eliya Makundi kutoka Sunlight Construction Company, alisema kwa kuchukua mashine hiyo mpya, ameweza kuokoa zaidi ya Sh. milioni 20 kwa mwezi kutoka kwenye faini za barabarani.

Alisema kwamba awali, walikuwa wakikabiliwa na faini kubwa kutoka kwa Tanroads kutokana na kuzidisha uzito kwa kuwa walikuwa wakikadiria tu uzito walizobeba, lakini mashine hizi mpya zina uwezo wa kupima kwa usahihi na uhakika kiasi kinachotakiwa.

Makundi alibainisha kwamba wakati huu ambapo nchi imeingia kwenye kazi kubwa za ujenzi, makandarasi wanaweza kuvuka ushindani kwa kununua mashine mpya hizo zinazofanya kazi katika kasi ya kushangaza na wakati huo huo unaokoa fedha na muda lakini zikiwa na ufanisi mkubwa. Mkandarasi mwingine, Fenny Elisha wa Sumaco Engineering kutoka Singida, alisema ameagiza moja ya mashine hizo mpya kwa sababu wanajua zitakuwa na faida katika kazi za kila siku.

# Waziri akiri msongamano mkubwa magerezani

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

SERIKALI imekubali kuwapo kwa changamoto ya mrundikano wa wafungwa na mahabusi katika magereza nchini likiwamo Gereza Kuu la Butimba jijini Mwanza, ambalo linahudumia wafungwa na mahabusi zaidi ya 2,000.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, alisema hayo juzi katika mkutano wa waandishi wa habari jijini Mwanza, baada ya kumaliza ziara yake ya siku 10 ya kutembelea magereza katika mikoa ya kanda ya Ziwa na kusikiliza kero na malalamiko mbalimbali ya wafungwa na mahabusi magerezani.

"Nilikuwa na ziara ya siku kumi na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Biswalo Mganga, tumetembelea magereza katika mikoa ya Mara, Simiyu, Shinyanga na Mwanza, na kusikiliza kero na malalamiko ya wafungwa na mahabusi magerezani, kutokana na msongamano mkubwa.

Miongoni mwa magereza yenye msongamano ni Gereza la Butimba linalohudumia zaidi ya wafungwa na mahabusi 2,000 isivyo kawaida.

Waziri Mahiga alisema kuwa majengo ya magereza mengi nchini yamezidiwa uwezo wa kuhudumia wafungwa na mahabusi, hivyo kuwapo kwa mrundikana mkubwa unaoweza kuhatarisha maisha yao.

Alisema magereza yaliyopo yamejengwa zamani tangu enzi za wakoloni wakati idadi ya watu wakiwa wachache.

"Majengo mengi nimeona yamejengwa miaka ya 1942,1948,1958, enzi za ukoloni pamoja na upungufu wa mahakama hazitoshelezi kuanzia za mwanzo," alisema na kuongeza:

"Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu na Rufani pamoja na upungufu wa wafanyakazi wa mahakama hizo."

Alisema magereza mengine aliyotembelea katika ziara hiyo ni la Wilaya ya Tarime ambalo lina idadi kubwa ya wafungwa na mahabusi 500 zaidi ya uwezo wake, Gereza la Mugumu –Serengeti, Bunda, Kahama, Bariadi, gereza la mkoa wa Shinyanga pamoja na gereza kuu la Butimba jijini Mwanza ambalo alisema kuwa alisikiliza kero na malalamiko ya wafungwa na mahabusi zaidi ya saa saba.

Dk. Mahiga alisema kero na malalamiko mengi ya wafungwa na mahabusi alizokumbana nazo ni wafungwa wengi na mahabusi kubambikiwa kesi na maofisa wa serikali wakiwamo polisi, wananchi wenyewe kwa wenyewe kubambikiana kesi za uongo za jinai pamoja na ucheleweshwaji wa kusikilizwa kesi mahakamani unaotokana na upelelezi kutokamilika kwa wakati.

Alisema malalamiko mengine aliyokutana nayo gerezani ni wizi wa kuku, simu za kiganjani na vitu vidogo vidogo.

Alisema wamo wazee vikongwe wa miaka 70, 80 hadi 90 ambao wengine wameshtakiwa na serikali katika Wilaya ya Serengeti kwa kosa la kuingia kwenye Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na kuokota kuni.




Msimamizi wa Idara ya Vipuri wa Mantrac Tanzania, Matiko Bugumia, akitoa maelezo kuhusu vipuri wakati wa uzinduzi wa katapila mpya ijulikanayo kama New Generation Hydraulic jijini Dar es Salaam. Uzinduzi huo ulifanywa na Mantrac Tanzania kwa kushirikiana na Kampuni ya Caterpillar. **MPIGAPICHA WETU**

# Kamati yabaini upungufu barabara za Tarura

**Na Hamisi Nasiri, MTWARA**

KAMATI maalum iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, imebaini hali ya upungufu katika utekelezaji wa ujenzi wa barabara za mijini na vijijini zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) katika Halmashauri za Masasi na Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Byakanwa amewaagiza mameneja wote wa Tarura ambao wamefanya vibaya katika ujenzi wa barabara zao kupitia upya orodha ya majina ya makandarasi walioko kwenye maeneo yao ili kubaini viwango vya ubora wa utendaji wao kwa kuwa ndiyo imekuwa kikwazo cha utendaji kazi wa barabara hizo.

Byakanwa aliyasema hayo katika kikao cha Bodi ya Barabara kilichohudhuriwa na wajumbe mbalimbali.

Alisema mapema mwaka huu aliunda kamati maalumu ya ukaguzi wa barabara zote zilizojengwa na wakala wa barabara za Tarura katika Halmashauri ya Wilaya za Masasi, Masasi Mji na Manispaa ya Mtwara Mikindani na matokeo ni kwamba tume imebaini upungufu katika barabara zilizojengwa na Tarura za halmashauri hizo.

Byakanwa alisema aliamua kuunda kamati hiyo baada ya kutilia shaka ubora wa baadhi ya barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Alisema kufuatia upungufu huo, kila barabara ambayo imebainika kujengwa chini ya ubora unaotakiwa ni lazima ujenzi huo urudiwe upya ili kuzifanya barabara hizo ziwe katika ubora ambao unahitajika, na kuwa utekelezaji huo ufanyike haraka.

"Tuna wajibu wa kuhakikisha fedha za serikali zinatumika kama ilivyokusudiwa kama mkandarasi hafanyi kazi ipasavyo na kwa ufanisi hakuna haja ya kuendelea kufanya kazi na mkandarasi kama huyo ni bora akakatishwa mkataba wake ili asiendelee kuharibu barabara," alisema Byakanwa.

Byakanwa alisema Tarura Wilaya ya Nanyumbu ni mfano wa kuigwa na kutokana na hilo wakala za halmashauri zingine za mkoa wa Mtwara iwapo kila meneja atafanya kazi kama iliyofanywa na meneja wa Nanyumbu barabara zote zitakuwa zikijengwa kwa ubora zadi.

Alisema kuanzia sasa na kuendelea serikali haitamvumilia meneja yeyote wa Tarura na mkandarasi wake ambao watakuwa wakifanya kazi za barabara kwa kiwango cha chini na kuisababishia serikali hasara ya fedha inazozitumia.

HABARI KIMATAIFA

## Uturuki yajiengua mpango wa ndege

**NEW YORK** Marekani

MSEMAJI wa Ikulu ya Marekani, Stephanie Grisham, amethibitisha kuiondoa Uturuki, katika mpango wa kunufaika na ndege za kivita za kisasa chapa F-35 kwa mataifa ya jumuiya ya kujihami ya NATO.

Hii ni baada ya Uturuki kuamua kununua makombora kutoka Urusi chapa S-400.Taarifa ya ikulu ya Marekani imesema makombora hayo ya Urusi, hayawezi kutumiwa pamoja na ndege za kivita za F-35 za Marekani.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki, Mevlut Cavusoglu, ameuita uamuzi huo wa Marekani kuwa usio wa haki, na kwamba hatua ya Marekani ya kuiondoa nchi yake kwenye mpango huo haikuzingatia sababu za msingi. **DW**

## Mrithi wa May aipa angalizo EU

**LONDON,** Uingereza

MGOMBEA wa nafasi ya Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amesema Umoja wa Uaya utabeba sehemu ya lawama, iwapo nchi yake itaondoka kwenye Umoja huo bila ya makubaliano.

Akizungumza katika kampeni ya mwisho mjini London, kabla ya kutangazwa kwa mshindi wa nafasi hiyo wiki ijayo, Johnson amesema atatafuta majadiliano na Umoja wa Ulaya, juu ya masharti mapya ya kujiondoa katika umoja huo.

Hata hivyo amesema, iwapo Umoja wa Ulaya hautakuwa tayari kubadilisha makubaliano yaliyopo, nchi yake haitakuwa na namna nyingine zaidi ya kujiondoa kwa masharti mengine.

Viongozi wa umoja wa Ulaya, wamewahi kusema mara kadhaa kuwa hawatojadiliana tena juu ya mpango wa Uingereza wa kujitoa ulioleta msuguano na waziri mkuu wa Uingereza aliyetangaza kujiuzulu Theresa May, ingawa ulikataliwa na wabunge zaidi ya mara tatu. **DW**

## Ebola DRC yashtua jumuiya kimataifa

**KINSHASA,** Congo

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeutangaza mlipuko wa homa ya ebola katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kuwa dharura ya afya ya umma inayotia wasiwasi jumuiya ya kimataifa.

Msemaji wa shirika hilo, Tedros Adhanom Ghebryesus, amesema ni wakati wa dunia nzima kujifunza na kuimarisha juhudi zao maradufu, kupambana na ugonjwa huo.

Aliongeza kuwa dunia haina budi kufanya kazi kwa pamoja na Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo, ili kutokomeza janga hilo na kujenga mifumo bora ya kiafya.

Ebola, ambayo imekuwapo kwa mwaka mmoja mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, imedhibitiwa pakubwa katika maeneo mbalimbali lakini siku chache zilizopita kuliripotiwa kisa cha kwanza cha mtu aliyepata virusi vya ugonjwa huo katika mji wa Goma. **DW**

# Makombora ya Urusi tishio muungano NATO

**MOSCOW,** Urusi

JUMUIYA ya kujihami ya nchi za Magharibi (NATO) imesema makombora ya Urusi ni hatari na kwamba muda unakwisha wa kuunusuru mkataba muhimu wa Urusi na jumuiya hiyo ,Katibu Mkuu wa muungano wa Nato, Jens Stoltenberg, ameambia BBC.

Stoltenberg ameahidi kuwa zitachukuliwa hatua 'zilizopangwa na za kujilinda ' kama Urusi haitarejea katika utekelezaji wa mkataba ifikapo Agosti 2, mwaka huu ambao ni muda wa mwisho uliowekwa.

"Lazima tujiandae kwa ajili ya dunia kutokana na makombora zaidi ya Warusi," amesema Kiongozi wa Muungano wa kujihami wa nchi za magharibi-NATO.

**Mkataba wa udhibiti wa matumizi ya nuklia umekuwa muhimu katika udhibiti wa silaha kwa karne kadhaa na sasa tunashuhudia kukiukwa kwa mkataba.**

Makubaliano ya 1987 yaliyosainiwa baina ya Marekani na Muungano wa Usoviet USSR yalipiga marufuku makombora ya masafa mafupi na marefu.

Rais Trump alitangaza kuwa Marekani itaacha utekelezaji wa majukumu yake chini ya mkataba juu ya vikosi vya masafa ya nyuklia mwezi Februari, akiishutumu Urusi kwa kukiuka mkataba huo.

Urusi inakana madai hayo, lakini ilisitisha kwa muda utekelezaji wa majukumu yake ya mkataba huo muda mfupi na baadae kutangaza mipango ya kutengeneza mfumo wa silaha za nyuklia.

Katika mahojiano ya kina na BBC, Stoltenberg anasema makombora ya Urusi ambayo anasema ni ukiukaji wa wazi wa mkataba yanauwezo wa kinyuklia, kutumika popote, ni magumu kuyatambua, na yana uwezo wa kuifikia miji ya Ulaya katika kipindi cha dakika chache.

"Hili ni tatizo kubwa. Mkataba wa udhibiti wa matumizi ya nuklia umekuwa muhimu katika udhibiti wa silaha kwa karne kadhaa na sasa tunashuhudia kukiukwa kwa mkataba," alisema.

Huku kipaumbele kikiwa ni kuirejesha Urusi kuheshimu kanuni za mkataba , Stoltenberg alisema hakuna ishara zozote kuwa nchi hiyo itafanya hivyo. **BBC**



Makombora ya masafa marefu ambayo Urusi inadaiwa kuipatia Uturuki hatua ambayo Marekani ilikasirishwa nayo. **PICHA BBC.**

# Mchakato waanza kuwatambua walioambukizwa na mwanamke

**KAMPALA,** Uganda

MAMLAKA za Uganda ziko kwenye mchakato wa kuwatambua watu ambao huenda wameambukizwa na mwanamke mmoja ambaye alionyesha kuwa na dalili za ebola kwenye soko la Uganda juma lililopita, kabla ya baadae kupoteza maisha mjini Beni katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Kwa mujibu wa afisa wa afya wa wilaya, mwanamke huyo alitapika sokoni hapo eneo la Mpondwe lililo kwenye mpaka wa Uganda alhamisi juma lililopita kabla ya kurejea DR Congo na kupoteza maisha kutokana na Ebola.

Alisema kuwa alivuka mpaka kuingia Uganda akitokea Congo kupitia njia ya mpaka isiyo rasmi.WHO na wizara ya afya nchini Uganda zimethibitisha kuwa mwanamke huyo, muuza samaki alipoteza maisha kutokana na virusi vya Ebola.

Takribani wachuuzi wa samaki 600 na wabadilishaji wa fedha katika soko la mpaka wa Mpondwe wametambulika na watapatiwa chanjo.

Mwezi Juni, kulikuwa na vifo vya watu wawili vilivyothibitishwa kusababishwa na virusi hivyo magharibi mwa Uganda, karibu na mpaka. Tangu wakati huo hakukuwa na ripoti nyingine yeyote kuhusu kuwapo kwa ugonjwa huo nchini humo.

Tukio la hivi karibuni limeongeza hatari ya ugonjwa huo kusambaa Uganda, lakini mamlaka zinasema hazitafunga soko la mpakani kwa sasa.

Zaidi ya watu 6,000, wengi wao wafanyakazi wa afya, wamepatiwa chanjo nchini Uganda tangu mwezi Novemba mwaka 2018.

Tangu mlipuko wa Ebola kutokea Congo, zaidi ya watu 2,000 wameripotiwa kuwa na virusi na watu zaidi ya 1,500 wamepoteza maisha. **BBC**



Meneja Mwandamizi Kitengo cha Biashara, Wogofya Mfalamagoha (katikati), Meneja wa Kanda ya Mashariki, Baraka Ladislaus (kulia) wakimkabidhi cheti mmoja ya wateja wa Benki ya NMB, Paul Kihwili, kwenye kongamano lililoandaliwa na benki hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# TPSF yampongeza JPM

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imesema Rais John Magufuli, amefanya mabadiliko makubwa sekta binafsi kwa kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara na kutoa fursa ya kufanyika makongamano yanayoleta mabadiliko ya kichumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akielezea kuhusu jukwaa la biashara la pamoja baina ya Tanzania na Uganda, linalotarajia kufanyika nchini kwa siku tatu kuanzia Septemba 3, mwaka huu.

Akizungumzia kuhusu mkutano huo wa mwezi Septemba, Simbeye, alisema utafanyika jijini Dar es Salaam na kukutanisha wadau wa sekta binafsi wa nchi hizo mbili lengo likiwa ni kutafuta fursa na ubia wa kibiashara.

"Tunaamini mkutano huu utafungua fursa zaidi kati ya Tanzania na Uganda kama mnakumbuka ipo miradi mikubwa ambayo inatekelezwa na nchi hizi hivyo tutajadili namna ambavyo wadau wetu wa kibiashara watakavyonufaika nayo," alisema.

Simbeye aliwataka wadau wa sekta binafsi kuhakikisha wanajiandikisha kuhudhuria mkutano huo kwa sababu hakuna gharama zozote wanazotakiwa kutoa.

"Mara kwa mara mmewasikia viongozi wetu wakizungumza bila sekta binafsi hakuna maendeleo endelevu ndio maana sekta binafsi tumekuwa mstari wa mbele kushirikiana na serikali kuandaa makongamano kama haya ambayo tunahakikisha yataleta faida baadaye.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, wanataka kuona mahusiano yenye nguvu baina ya nchi hizo yakitafsiriwa katika biashara kwa manufaa ya pande zote mbili. Alisema biashara zilizofanyika mwaka 2015 kati ya nchi hizo zilikuwa za Sh. bilioni 178, mwaka 2018 zilikuwa za Sh. bilioni 358.






# Ushahidi anayedaiwa kuua mke kuendelea

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepiga kalenda kusikiliza ushahidi wa utetezi wa Godfrey Nkwambi, anayekabiliwa na kesi ya kumuua kwa makusudi mke wake Bahati Hussein, hadi Julai 24, mwaka huu.

Kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa utetezi jana katika mahakama hiyo iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji, iliyoketi chini ya Naibu Msajili, Pamela Mazengo.

Hata hivyo, upande wa utetezi umeomba muda wa kujiandaa na ushahidi wao. Msajili Mazengo alisema kesi hiyo itasikilizwa ushahidi wa utetezi Julai 24, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Upande wa Jamhuri unaongozwa na Wakili wa Serikali, Erick Shija.

Mapema mahakamani hapo, watoto wawili wa marehemu akiwamo mtoto wa miaka 10, wakati mama yake anauawa alikuwa na miaka mitano, alidai mahakamani alimwona baba yake wa kambo (mshtakiwa), akimnyonga mama yake Bahati.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Juni 21, 2014 eneo la Ulongoni, Nkwambi alimwua kwa makusudi mke wake Bahati. Mshtakiwa alifunguliwa mashtaka na kufikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam.

# Mahakama yatoa hati ya kukamatwa raia Moldovan

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imetoa hati ya kukamatwa raia wa Moldovan, Vadim Burin, anayekabiliwa na tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kula njama, kuingiza nchini, kusimika mitambo ya mawasiliano ya simu za kimataifa bila leseni ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 41.7.

Mbali na Burini, mshtakiwa mwingine aliyesomewa mashtaka yake jana ni dereva wa Uber, Msafiri Msayi mkazi wa Kivule, jijini Dar es Salaam.

Washtakiwa wote wawili, walisomewa mashtaka katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Monika Mbogo, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali, Batilda Mushi. Mushi alidai katika shtaka la kwanza siku na mahali tofauti jijini Dar es Salaam washtakiwa walikula njama kutumia mtandao isivyo halali.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Mei 15, mwaka huu, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere washtakiwa kwa pamoja waliingiza nchini vifaa vya elektroniki vya mawasiliano bila leseni kutoka TCRA.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa washtakiwa walisimika mifumo ya elektroniki bila leseni ya TCRA.

Wankyo alidai shtaka la nne, kati ya Mei 15 na Juni 10, mwaka huu, katika Hoteli ya Sea Cliff, walitumia vifaa vya mawasiliano kwa lengo la kupokea na kutoa bila kuwa na kibali cha TCRA.

Shtaka la tano, ilidaiwa Mei 15, mwaka huu, katika Hoteli ya Sea Cliff iliyopo Masaki, jijini Dar es Salaam, washtakiwa waliendesha mtandao wa mawasiliano ya kimataifa bila leseni ya TCRA.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kati ya Mei 15 na Juni 10, mwaka huu kwa lengo la kukwepa malipo ya mawasiliano ya kimataifa waliunganisha mawasiliano hayo huku wakijua ni kinyume cha sheria.

Shtaka la saba, ilidaiwa kuwa siku na tarehe za shtaka la sita Hoteli ya Sea Cliff washtakiwa walitumia laini za simu 173 za mtandao wa Halotel na 37 za Vodacom, ambazo hazijasajiliwa huku wakijua ni kinyume cha sheria.

Wankyo alidai katika shtaka la nane, washtakiwa wameisababishia serikali na TCRA hasara ya Sh. 41,710,800.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri ulidai kuwa wanaomba hati ya kukamatwa mshtakiwa wa kwanza Burin, upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika uliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008

**PLOT NA NYUMBA VINAUZWA**

Ploti na nyumba vinauzwa mtoni kijichi wilaya ya temeke. Ploti ni mbili kwa moja ni nzuri na kubwa saana kwa matumizi yote ya kibiashara na makazi. Mawasiliano: 0688 640101

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

### KUPOTEA KWA CHETI



115330002

**ZAITUNI MAULIDI BOKI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1188/0024 kilichotolewa na **NELUKA SEKONDARI** mwaka 2016 pamoja na cheti cha kuzaliwa.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: MBA/RB/131541/2019.**

### KUPOTEA KWA CHETI




215329302

**Yoktan Obadia** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0914-0128** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2007 katika shule ya Sekondari Muyama na cheti cha Ualimu chenye **namba E0544-0213** kilichotolewa na chuo cha Ualimu Kabanga mwaka 2011.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: KGT/RB/4054/2017**

### KUPOTEA KWA CHETI



115329302

**Amani Abedi** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1093-0033** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2005 katika shule ya sekondari Eldersgate.

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: 991088854013**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe: 18/07/2019

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 20/07/2019 kampuni ya Builders & Limeworks Co. Ltd itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka SAME kuelekea ARUSHA, gari hilo lenye namba za usajili **T170 BAP/ T515 ALG**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | ................... | 17.0m |
| Upana | ..................... | 3.5m |
| Kimo | ..................... | 4.55m |

3. Njia itakayotumika: **SAME** hadi **ARUSHA** Kupitia KIA, gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115329702

### TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**KAHAMA IMPORT AND EXPORT COMMERCIAL AGENCY** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SUNLG yenye namba za usajili **T 365 BRU. Engine NO 156FMIB0002720** na CHASIS NO LTZPCJLN2B0000358.

Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kwenye kituo chochote cha polisi

TAARIFA YA POLISI
**KHM/RB/565/019.**

115330902

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TARIME**
**RUFAA. NA 28/2019**
**ERENESTI ORWANDA.........................MLETA RUFAA**
**DHIDI YA**
**OTIENO OLIECH..................MJIBU RUFAA**
**Mjibu rufaa OTIENO OLIECH popote ulipo.**

Fahamu kwamba mleta rufaa ameleta rufaa dhidi yako, kesi ya ardhi na 28/2019.

Hivyo basi kama unakusudia kupinga sababu hizo unatakiwa ulete majibu yako, na uwepo barazani wewe binafsi, wakili wako au muwakilishi anayekubalika kisheria, tarehe 29/07/2019 siku ambayo shauri limepangwa kutajwa.

Endapo hautatekeleza haya shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa baraza hili leo tarehe 2/7/2019

115329802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI MOROGORO**
Usimamizi wa mirathi No;138/2019

Ombi la SIMBA RAJABU MATITU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SIMBA SAID MATITU**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/07/2019.

11529602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;144/2019

Ombi la **JACKSON SELACK MBWILO** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SELACK JEREMIA MBWILO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 31/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/07/2019.

115329502

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.43 OF 2019**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**BRYTON SIMON MWILIKO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MTEMI ERICK BRYTON MWILIKO**

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased 's estate are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of petition for letters of administration is made to the above named petitioner.


Objections (if any) to the grant should be filed on or before Day of 1th August , 2019.

The will if any of the said deceased to be deposited and open for inspection of the Court.

Dated 15th This day of July,2019.

115329902

### CHETI KIMEPOTEA



215328502

**MOSES B. SAMWEL** wa Buzuruga, Mwanza. Anatangaza kupotelewa na Cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne chenye **Index Number S.2270/0119** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2015 katika Shule ya Sekondari Mkituntu.
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilicho karibu.
Taarifa ya Polisi: **MW/RB/6550/2018**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2019

(Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA 30.06.2019 | ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.03.2019 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 5,016 | 5,657 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,819 | 14,055 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 27,741 | 28,396 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 23,218 | 27,692 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 103,323 | 98,585 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,515 | 1,903 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,206 | 1,242 |
| **16** | **Jumla ya Mali** | **177,838** | **177,530** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 3,561 | 1,272 |
| 18 | Amana za Wateja | 130,884 | 134,886 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 137 | 89 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 44 | 73 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 23 | 20 |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,340 | 1,126 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **136,989** | **137,466** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **40,849** | **40,064** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 998 | 941 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 24,718 | 24,203 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,794 | 1,009 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,339 | 3,911 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **40,849** | **40,064** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 15,338 | 6,527 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,148 | 6,567 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,897 | 2,362 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22.97% | 22.57% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.84% | 6.50% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 78.37% | 74.20% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 58.10% | 55.53% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 86.75% | 87.12% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.26% | 2.00% |
| (vii | Ongezeko la Mali | 0.17% | 2.00% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 .06. 2019

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO YA MWAKA SASA 30.06.2019 | ROBO YA MWAKA LINGANISHI 30.06.2018 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 30.06.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,551 | 3,504 | 7,049 | 6,880 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,174 | 1,126 | 2,283 | 2,361 |
| **3** | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,378** | **2,378** | **4,767** | **4,519** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 569 | (133) | 779 | 326 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **785** | **597** | **1,154** | **1,076** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 160 | 51 | 327 | 208 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 623 | 540 | 824 | 860 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 3 | 6 | 4 | 8 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba:** | **1,443** | **1,234** | **2,616** | **2,526** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 557 | 403 | 1,135 | 762 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 234 | 137 | 250 | 190 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 652 | 693 | 1,231 | 1,573 |
| | 7.4 Other Provision | - | - | - | - |
| **8** | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,151** | **1,874** | **2,526** | **2,743** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 366 | 362 | 732 | 725 |
| **10** | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **785** | **1,512** | **1,794** | **2,018** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **785** | **1,512** | **1,794** | **2,018** |
| **13** | Idadi ya Waajiriwa | **49** | **50** | **49** | **50** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 79 | 151 | 179 | 202 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 4 | **4** | **4** | **4** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.80% | 0.59% | 2.03% | 2.35% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 7.72% | 2.62% | 8.92% | 10.47% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 45.60% | 30.01% | 44.17% | 30.01% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6.18% | 1.24% | 6.26% | 4.94% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO ILIYOISHIA 30.06.2019

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO YA MWAKA YA SASA 30.06.2019 | ROBO YA MWAKA ILIYOPITA 31.03.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 30.06.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 30.06.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1,151 | 1,375 | 2,526 | 2,743 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | | | | |
| | -Hasara katika Mali | 617 | 260 | 877 | 445 |
| | -Prior Period Adjustment | - | - | - | (639) |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (5,307) | (222) | (5,529) | (2,216) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (4,002) | 2,728 | (1,274) | (698) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 3,526 | 215 | 3,741 | 3,811 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (8,689) | 4,901 | (4,700) | (9,157) |
| | -Kodi Iliyolipwa | (366) | (366) | (732) | (725) |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | 437 | (911) | 437 | 1,707 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **(12,634)** | **7,980** | **(4,654)** | **(4,730)** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | (13) | (13) | (26) | (5) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | 656 | (5,029) | (4,373) | 6,737 |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (ainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **643** | **(5,041)** | **(4,399)** | **6,732** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | | - | - | - |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV** | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **(11,991)** | **2,938** | **(9,053)** | **2,002** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 34,245 | 31,307 | 31,307 | 37,328 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **22,255** | **34,245** | **22,255** | **39,330** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2019

(Kiasi Kwa Shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapa | - | - | 1,794 | - | - | - | 1,794 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 646 | (646) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (62) | - | 62 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **26,512** | **3,338** | **999** | **-** | **40,849** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | 10,000 | - | 22,271 | 4,068 | 781 | - | 37,120 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,147 | - | - | - | 2,147 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 84 | (84) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (156) | - | 156 | - | - |
| Mengineyo | - | - | (212) | - | - | - | (212) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2019**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir (Mkurugenzi Mtendaji) | | 12th July, 2019 |
| Deogratias Edward Ndushi Mkuu wa Fedha | | 12th July, 2019 |
| Mwita Mohamed Mwita (Mkaguzi wa Ndani) | | 12th July, 2019 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni | | 12th July, 2019 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava | | 12th July, 2019 |

215331502

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YAJIANDAA KUMSAJILI CEBALLOS

●●● Klabu hiyo pia yawasilisha ofa mpya ya tatu ya kumwania Tierney...

**LONDON,** England

KATIKA kuanza kutekeleza uamuzi wake wa kuimarisha kikosi chake kwa ajili ya msimu mpya, Arsenal imeanza mchakato wa kuwania saini ya Dani Ceballos kutoka Real Madrid kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu.

**Kikosi hicho kinachofundishwa na Unai Emery kimepeleka ofa ya pauni milioni 32 kwa Gremio ili kumsajili winga Soares.**

Pia wamefikia makubaliano na St Etienne kwa ajili ya kumsajili William Saliba, beki huyo ambaye anaweza kurejea kwa mkopo.

Klabu hiyo ya London Kaskazini pia inarejea kusisitiza ofa wake ya kumwania beki wa Celtic na Timu ya Taifa ya Scotland, Kieran Tierney.

Emery pia bado hajafikia uamuzi wa mwisho wa kusajili winga mwingine wa kuitumikia timu hiyo katika kipindi hiki cha majira ya joto kwa ajili ya kuhakikisha anawapa nafasi nzuri ya kucheza nyota wake wawili, Pierre-Emerick Aubameyang na Alexandre Lacazette.

The Gunners imeweka wazi pia nia yake ya kuhitaji huduma ya winga wa Crystal Palace, Wilfried Zaha ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 80, lakini klabu zote mbili zimetofautiana kwa kiasi kikubwa kuhusu thamani ya nyota huyo na Arsenal sasa inajipanga kumsajili mchezaji Mbrazil anayeichezea Everton.

Arsenal inajiandaa kuwasilisha ofa nyingine mpya ya tatu ya kuwania saini ya Tierney ya dau la pauni milioni 25, baada ya ile iliyopita kukataliwa na Celtic.

Huku ikiwahakikishia mashabiki wake itasajili wachezaji wenye uwezo mkubwa ili kupata matokeo mazuri, Arsenal jana ilifanikiwa kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Bayern Munich uliochezwa huko Los Angels.

Granit Xhaka ambaye anatarajiwa kuwa nahodha mpya wa Arsenal kuchukua nafasi ya Laurent Kosciency alifunga bao la kwanza huku lile la ushindi likipachikwa na mshambuliaji chipukizi, Eddie Nketiah.

## ZISIKUPITE

### MADRID YAJIONGEZA

REAL Madrid inajipanga kuzindua "kampeni ya kusaka pauni milioni 200" kwa kuwauza washambuliaji, Gareth Bale (30) na James Rodriguez (28), ili kupata fedha za kumnunua kiungo wa Manchester United Mfaransa Paul Pogba (26). ***(Marca, via Sun)***

### RAIOLA AIGOMEA UNITED

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola amepuuza hesabu zinazoandaliwa na Manchester United ili kumrejesha kiungo huyo kwa klabu ya Juventus. ***(AS)***

### NEYMAR AWAITA UNITED

NEYMAR (27) amefungua milango kwa Manchester United kumsajili baada ya kuona kuwapo kwa sintofahamu katika mchakato wake wa kutaka kuondoka Paris St-Germain. ***(Mundo Deportivo, via Sun)***

### WILLIAN ATAKIWA BARCA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, anatarajia kufanya uamuzi juu ya hatima ya Mbrazil Willian kama atapewa mkataba mpya au la baada ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 kubakisha miezi 12 tu kwenye mkataba wake wa awali. Barcelona inatajwa kumwania mchezaji huyo kwa dau la pauni milioni 30. ***(Express)***

### BRUCE APEWA FUNGU

KOCHA wa Newcastle United, Steve Bruce, anatarajia kutumia zaidi ya pauni milioni 90 kwa ajili ya kufanya kuimarisha kikosi chake katika kipindi hiki cha dirisha la usajili wa majira ya joto. ***(Sky Sports)***

### SHEARER ALIMKATAA BRUCE

STRAIKA wa zamani wa Newcastle United, Alan Shearer, amesema kuwa alimwambia Steve Bruce asikubali kusaini mkataba wa kuifundisha klabu hiyo. Bruce anatajwa alikuwa katika nafasi ya 11 ya orodha ya makocha waliokuwa wanatakiwa kutua kwenye timu hiyo. ***(Sun)***

### UNITED YAPEWA ANGALIZO

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, ameionya Manchester United kuwa wameweka muda maalumu wa kumaliza kujadili uhamisho wa beki wao wa kati, Harry Maguire (26), huku wakiweka wazi kwamba hawataki beki huyo aondoke. ***(Star)***

### ZANIOLO AGOMBEWA

MANCHESTER United imeweka wazi kwamba imeingia kwenye vita ya kuwania saini ya kiungo wa Roma, Nicolo Zaniolo, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Mirror)***

### LUKAKU AJIPA MATUMAINI

STRAIKA wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, anaamini yuko kwenye nafasi nzuri ya kuondoka Manchester Utd na kujiunga na Inter Milan. ***(Times - subscription required)***

### LLORENTE MAMBO SAFI

STRAIKA Mhispania, Fernando Llorente, ambaye mkataba wake na Tottenham umemalizika, anajiandaa kutua kwa Fiorentina inayoshiriki Serie A. ***(Mail)***

### EMERY AAHIDI MAKUBWA

KOCHA Unai Emery anasisitiza kuwa Arsenal itahakikisha inakamilisha mchakato wa kusajili wachezaji wenye ubora watatu au wanne kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu England. ***(Independent)***

# HABARI MICHEZO

## UDSM yaviita vyama vya michezo

**Na Renatha Msungu**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kimevitaka vyama na mashirikisho mbalimbali ya michezo kushirikiana nao kwa lengo la kukuza na kuendeleza sekta hiyo hapa nchini.

Wito huo umetolewa jijini Dar es Salaam jana na Mkuu wa Idara ya Michezo na Viungo wa chuo hicho, Dk. Steven Mabagala, wakati wa sherehe ya kukabidhi vyeti kwa wanafunzi 25 wa UDSM ambao walihitimu kozi ya ukocha wa riadha ngazi ya kwanza inayotambuliwa na Shirikisho la Riadha la Kimataifa (IAAF).

Dk. Mabagala alisema riadha wameonyesha njia kwa kupata elimu ambayo ni njia ya kufikia mafanikio yatakayoisaidia nchi kukuza mchezo huo.

Aidha, aliwataka wahitimu wa kozi hiyo, kuwafundisha watoto mchezo wa riadha na kutoweka kabatini vyeti hivyo na badala yake wavitumie kwa maslahi ya taifa.

"Kozi mliyoshiriki isiwe mwisho, bali mpanue wigo zaidi ya mliyoyapata katika elimu inayotambulika na IAAF," alisema Dk. Mabagala.

Alipongeza kozi hiyo kwa kueleza kwamba, imetolewa wakati mwafaka na kuwataka wahitimu hao kuwafundisha watoto kwa sababu hiyo ni kozi ya kitaaluma zaidi.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Wilhelm Gidabuday, alisema elimu waliyoipata wanafunzi hao ni sehemu ya historia kwa sababu ya umuhimu wake.

## Ligi ufukweni yafikia patamu

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI ya ufukweni hatua ya nane bora inatarajia kuanza leo kwa timu za Kundi A, Mburahati kukutana na Kijitonyama kwenye ufukwe za Coco jijini Dar es Salaam.

Hatua hiyo ambayo imepangwa katika makundi mawili, inatarajiwa kumalizika Julai 27 mwaka huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Salum Madadi, alisema kuwa mechi nyingine ya hatua hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Prisons dhidi ya Friends kutoka Mkwajuni jijini.

Madadi alisema kuwa wanatarajia kushuhudia ushindani kwenye ligi hiyo kama ilivyokuwa katika hatua ya awali.

Alitaja mechi nyingine itakayochezwa ya Kundi B itakuwa ni kati ya Buza dhidi ya Friends Rangers ya Magomeni, huku Kisa itaumana na Vingunguti.

Naye Meneja wa Soka la Ufukweni, Baraka Kizuguto, alisema kuwa mashindano hayo yatasindikizwa na burudani mbalimbali huku kiingilio kikiwa ni bure.

# TAIFA STARS YATABIRIWA MAKUBWA FAINALI CHAN

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa makipa wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Saleh Machupa, amesema ana matumaini makubwa kuwa timu hiyo inafanya vema katika mechi yake dhidi ya Kenya (Harambee Stars), itakayochezwa Julai 28 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Taifa Stars itaikaribisha Harambee Stars katika mechi ya kwanza ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), na timu hizo zitarudiana wiki moja baadaye jijini Nairobi, Kenya.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Machupa, alisema wachezaji wa Stars ambao wengi wao walishiriki katika fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon), wameshapata uzoefu na hivyo wataingia kuwakabili Harambee Stars wakiwa vema zaidi. Machupa alisema kuwa Watanzania wanakiamini kikosi hicho kuelekea michuano hiyo na wanawaomba mashabiki kuendelea kuwashangilia ili kuongeza hamasa ya kufanya vema katika mechi mbalimbali.

"Matumaini yangu Taifa Stars itafanya vizuri zaidi, wachezaji wamejifunza mambo mengi kwenye fainali za Afcon, licha ya kuwa timu iliondolewa katika hatua ya makundi, lakini ukweli uzoefu wameupata," alisema.

Aliongeza kwamba anamshukuru Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, kwa kumpa nafasi hiyo na kueleza kuwa ndoto ya muda mrefu sasa imetimia.

Aliahidi atahakikisha wanawaimarisha viwango magolikipa wa timu hiyo kama ambavyo inatarajiwa.

Kocha huyo aliwahi pia kukinoa kikosi cha Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 20 ( Ngorongoro Heroes).

Kaimu Kocha Mkuu wa Stars, Mrundi Ndayiragije, alimteua Machupa na Suleiman Matola wa Polisi Tanzania kuiongoza timu hiyo inayowania tiketi ya kushiriki fainali za CHAN kwa mara ya pili, ya kwanza ikiwa ni mwaka 2008.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na michuano ya COSAFA itakayofanyika kuanzia Agosti Mosi hadi 11, mwaka huu, nchini Afrika Kusini. **PICHA: TFF**

# *Ruvu kutangaza kikosi chake leo*

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa "Maafande" wa Ruvu Shooting ya Mlandizi mkoani Pwani leo unatarajia kutangaza kikosi chao walichokisajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2019/20, imeelezwa.

Ruvu Shooting itafungua pazia la msimu mpya kwa kuwakaribisha Yanga, mchezo utakaochezwa Agosti 28 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, msemaji wa timu hiyo, Masau Bwire, alisema kuwa kikosi chake kimesajili wachezaji wa hapa nchini na inawaamini wana uwezo wa kufanya vema kwenye ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Bwire alisema kwamba bado klabu yao inaamini kuwa Tanzania ina wachezaji wenye vipaji na wenye uwezo wa kutwaa taji la Ligi Kuu Bara kama watajituma na kupambana kwenye mechi zao zote za ligi hiyo yenye kushirikisha timu 20.

"Kesho (leo) tutangaza kikosi chetu cha maangamizi ambacho kitaanza msimu kwa kuumana na Yanga katika msimu mpya wa Ligi Kuu, ila naweza kusema kuwa hatujasajili mchezaji yoyote kutoka nje ya nchi, tunaamini Tanzania kuna wachezaji wengi wazuri," alisema Bwire.

Kiongozi huyo alitamba kwamba msimu huu wataingia wakiwa wenye ushindani, kwa sababu wamesajili kikosi imara na chenye uwezo wa kukabiliana na ushindani kutoka kwa timu zote zitakazoshiriki ligi hiyo.


"Tunawaambia wajiandae, msimu huu tumesajili kikosi tofauti na vikosi vyote ambavyo tumewahi kusajili," Bwire alisema.

Aliongeza kuwa timu yao inaendelea na mazoezi chini ya kocha wao mpya, Salum Mayanga, ambaye ametua akitokea Mbao FC ya jijini Mwanza.

Michezo

Ijumaa Julai 19, 2019

Nipashe



Arsenal yajiandaa kumsajili Ceballos UKURASA 30

# Silaha Simba hazikamatiki

## ●●● Kocha afunguka bado hakuna mchezaji mwenye uhakika wa namba katika...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI wachezaji wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakifanya mazoezi ya aina mbalimbali ili kujiimarisha, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Aussems, amesema kuwa bado hakuna mchezaji mwenye uhakika wa kupata namba kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

**Kikosi hicho kimekuwa kikifanya mazoezi ya viungo "gym", uwanjani wakiwa na mipira na wakati mwingine bila ya kuchezea mipira.**

Nyota hao ambao walianza kambi hiyo iliyoko kwenye mji wa Rustenburg nchini humo Afrika Kusini, wamekuwa wakitumia vifaa vya kisasa ambavyo vinatumiwa na timu zilizoendelea katika mataifa ya Ulaya, wakati wa maandalizi ya msimu mpya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema kuwa kila mchezaji wa Simba anaonyesha bidii kwenye mazoezi yanayoendelea kwa sababu anataka kujihakikishia nafasi kwenye kikosi hicho.

Aussems, ambaye msimu uliopita aliipeleka Simba katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, alisema kwamba anafurahia kuona hali hiyo na kingine ni ukaribu wa wachezaji wake wapya na wa zamani, jambo ambalo alitarajia lingechukua muda.

"Tuna siku chache tangu tuanze mazoezi, na kumbuka tumekuja kwa makundi tofauti, lakini ukiwaangalia wachezaji, huoni tofauti, kila mmoja anafanya vema katika kila zoezi analoambiwa kufanya, tuko kama kundi, tunafanya kila kitu kinachotakiwa, ili tukitoka hapa tuwe imara na tayari kushindana," alisema Aussems.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa anaamini baada ya kupata mechi za kujipima nguvu, ndiyo atapata "picha" ya kikosi chake cha kwanza kitakavyokuwa.

Naye Mratibu wa timu hiyo, Abbas Ally, aliliambia gazeti hili kwamba wachezaji wote ni wazima na wanafurahia mazingira ya kambo yao.

"Wachezaji wote wako salama, viongozi pia tuko sawa, tunaendelea kukamilisha mazungumzo na kati ya siku mbili hizi, tutafahamu tunaanza kucheza na timu ipi, bado pia tunaiweka miili tayari kukabiliana na ushindani," Ally alisema.

Taarifa nyingine kutoka Simba zinasema kuwa tayari klabu hiyo imeshapata vibali vya kuishi na kufanya kazi nchini vya wachezaji wake wote wapya wa kimataifa ambao imewasajili.

Simba itaanza kutetea ubingwa wake wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kucheza dhidi ya JKT Tanzania, Agosti 23 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini wakati Yanga yenyewe itaanza kampeni zake Agosti 28 dhidi ya Ruvu Shooting kutoka Mlandizi mkoani Pwani.




Mshambuliaji mpya wa Barcelona, Antoine Griezmann akiwa amevaa jezi namba 17 ambayo ataitumia katika timu yake hiyo mpya ambayo imemsajili kwa dau la pauni milioni 108 akitokea Atletico Madrid. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga yafikiria makundi Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha Yanga kikiwa kinaendelea na mazoezi yake mkoani Morogoro, uongozi wa timu hiyo ya jijini Dar es Salaam umesema kuwa lengo lao kuu ni kuona wanafika hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.



Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela (pichani), alisema kuwa wamejipanga kufika hatua hiyo au zaidi, licha ya timu yao kupata tiketi ya kushiriki michuano hiyo wakiwa katikati ya mchakato wa usajili.

Mwakalebela alisema kuwa wanaamini watafanya vema kwa sababu baadhi ya wachezaji wao wana uzoefu na mashindano kutokana na kushiriki wakiwa na timu nyingine.

"Tutacheza kwa kuangalia malengo yetu, tunajua tunatakiwa tucheze ligi na wakati huo huo mechi za mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Mwakalebela.

Aliongeza pia wanaendelea vema na maandalizi ya tamasha la Siku ya Mwananchi ambalo litafanyika Agosti 4 mwaka huu kwa kushuhudia mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

## Azam: Tutalinda heshima

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema kuwa watashuka uwanjani kuwavaa AS Maniema ya Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) katika mchezo wa hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Kagame ili kulinda heshima ya Tanzania.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, alisema kuwa wanajua mchezo huo utakuwa mgumu, lakini tayari wameshawasoma wapinzani wao na wamejipanga kuwakabili.

"Mchezo wa nusu fainali huwa ni mgumu, ni mchezo unaohitaji tahadhari, unahitaji kujilinda zaidi kwa sababu hauna marudio, tumejiandaa vizuri ili kuipa heshima timu yetu na nchi yetu, vijana wote tuliokuwa nao hapa wako vizuri," alisema Cheche ambaye ni Msaidizi wa Mrundi Etienne Ndayiragije.

Mechi nyingine ya hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya KCCA ya Uganda dhidi ya Green Eagles kutoka Malawi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >